# Nipashe

Jumatano Januari 15, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580128

www.ippmedia.com

The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710




## Waziri avunja bodi ushirika, aagiza viongozi kukamatwa

UKURASA 3



Kimataifa

siasa

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

Fumbo linalowatesa Waingereza mwanamfalme kuhamia uraiani

OLE WENU NDUGU!

Mangula na marufuku yenye mwangwi kitaifa

Visasi vinavyotawala i tangu siku kuangushwa Boeing ya Ukraine

BURIANI QABOOS AL SAID Ukurasa 19

UKURASA 13

# Unadhimu upinzani bungeni moto mkali

**ALIYEPEWA** mikoba ya Lissu aachia ngazi, afunguka mazito ndani ya Chadema, Mbowe ang'aka...*Endelea ukurasa wa 2*



## MAGUFULI AWAPA MTIHANI MZITO MABALOZI WAPYA

UKURASA 2

Mabalozi wapya (kutoka kushoto), Meja Jenerali mstaafu, Gaudence Milanzi (Afrika Kusini), Dk. Modestus Kipilimba (Namibia), Prof. Emmanuel David Mwaluko Mbennah (Zimbabwe) na Dk. Benson Bana (Nigeria), wakila kiapo cha uadilifu kwa utumishi wa umma mbele ya Kamishna wa Maadili, Jaji mstaafu Haroid Nsekela, baada ya kuapishwa na Rais John Magufuli, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play  Download on the App Store


# Mtoto adaiwa kunajisiwa hadi kufa akichota maji

UKURASA 9

MICHEZO GONJWA LINALOITESA SIMBA NI HILI HAPA UK. 32 | MAONI, KATUNI UK.6

**HABARI KITAIFA**

# Kiti cha Lissu kaa la moto Chadema

**Na Salome Kitomari**

NI miezi sita imepita tangu Tundu Lissu apoteze nafasi ya ubunge. Kurejea kwake nchini bado ni mtihani kutokana na kile anachodai kuwapo shaka ya usalama wake.

Wakati mbunge huyo wa zamani wa Singida Mashariki akiendelea kuishi ughaibuni tangu usiku wa kuamkia Septemba 8, 2017 aliosafirishwa kwenda Kenya baada ya kushambuliwa kwa risasi jijini Dodoma, lingine limeibuka.

Ni kwamba; kwa muda wote ambao Lissu alikuwa ughaibuni Kenya na Ubelgiji kwa ajili ya matibabu ya kibingwa, Mbunge wa Rombo, Joseph Selasini, alikuwa anakaimu nafasi ya Mnadhamu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ambayo mtaalamu huyo wa sheria (Lissu) alikuwa anashikilia.

Hata hivyo, jana kwenye mitandao ya jamii kulisambaa barua iliyotiwa saini na Selasini Januari 13 mwaka huu, akieleza kujiuzulu nafasi hiyo.

Lakini, Selasini mwenyewe alishangaa namna barua yake ilivyovuja, akiiambia Nipashe kuwa barua hiyo aliandika kwenda kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Freeman Mbowe, na nakala kwa Spika, Job Ndugai na Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai.

"Nashangaa aliyeweka mtandaoni (barua yangu), nimepeleka kwa Mbowe, Spika na Katibu wa Bunge, sasa sijui kwanini wamepeleka huko," Selasini alilalamika.

Mbunge huyo mzoefu aliongeza: "Mimi sitaki kugombana na chama. Wapo wanaohoji kwanini sikumwambia (Mbowe) kwa mdomo kabla ya kuandika barua, lakini niliwahi kumwambia kwa mdomo.

"Kitaaluma, mimi ni mtawala, wapo wanahoji kwanini nimeandika barua bila kuandikiwa, lakini kwa kawaida ukikaa kwenye ofisi, ukafanya kazi vizuri na kukubalika, maana yake jamii ya eneo hilo imekubali wewe ufanye.

"Ofisi ya mnadhimu siyo ofisi ya chama, kanuni ipo inayomwongoza kushika nafasi hiyo na mnadhimu na Kiongozi wa Kambi wana ofisi yenye mali za Bunge zinazowawezesha kufanikisha kazi zao.

"Kwa muda wote niliokuwa kwenye ofisi hiyo, nimeshirikishwa kwenye vikao, sasa naondokaje bila kuwaambia wenye ofisi kwamba naondoka na mali zote ziko salama?" Selasini alihoji.

Mbunge huyo aliweka wazi kuwa uongozi wa Bunge umekuwa ukisisitiza kuwa unamkaribisha kwenye vikao vyake rasmi kwa sababu tu unamheshimu, vinginevyo asingeshirikishwa kwa kuwa hakuna uteuzi rasmi wa kushika nafasi hiyo.

"Ofisi hii ina mafao, sasa nayapataje wakati sina barua? Nimeandika barua kwa nia njema kabisa, wala sina sababu mbaya yoyote, lakini, sitaki kugombana na chama changu," alisisitiza.

**BARUA YENYEWE**

Katika barua yake hiyo yenye kichwa kinachosomeka 'Nafasi ya Mnadhimu wa Chama Bungeni', Selasini anamweleza Mbowe sababu za uamuzi wake wa kutotaka nafasi hiyo tena.

Selasini anaanza kwa kumshukuru Mwenyekiti huyo wa Chama cha Demokrasia na

INAENDELEA UK. 8



Mshtakiwa Abuu Kimboko akiwa chini ya ulinzi wa askari Polisi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana, baada ya kusomewa mashtaka ya uhujumu uchumi ikiwamo kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya aina ya Heroine. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# JPM awapa mtihani mabalozi wapya

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS John Magufuli amewapa mtihani mabalozi wapya wanne aliowaapisha jana, baada ya kuwataka kuripoti kwenye vituo vyao vya kazi ndani ya wiki moja.

Jana, Rais Magufuli aliwaapisha mabalozi hao aliowateua hivi karibuni kuiwakilisha Tanzania katika nchi za Afrika Kusini, Namibia, Zimbabwe na Nigeria.

Walioapishwa ni Meja Jenerali (mstaafu) Gaudence Milanzi anayekuwa Balozi wa Tanzania Pretoria-Afrika Kusini, Dk. Modestus Kipilimba anayekuwa Balozi wa Tanzania Windhoek-Namibia, Prof. Emmanuel Mbennah anayekuwa Balozi wa Tanzania Harare-Zimbabwe na Dk. Benson Bana anayekuwa Balozi wa Tanzania Abuja-Nigeria.

Baada ya kuwaapisha, Rais Magufuli aliwataka kuripoti katika vituo walivyopangwa ndani ya wiki moja au mbili kuanzia jana na akawasisitiza kwenda kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria, kwa kuzingatia maslahi ya taifa hasa kiuchumi na kuwawezesha Watanzania kupata ajira katika fursa zilizoko katika nchi hizo.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, aliwataka mabalozi hao kufuatilia maeneo yote ambayo Rais Magufuli alikubaliana na marais wenzake alipotembelea nchi hizo hivi karibuni.

Prof. Kabudi pia aliwataka mabalozi hao kuitangaza vyema Tanzania ambayo kwa sasa inapiga hatua kubwa katika maeneo mengi.

Hafla ya kuapishwa kwa mabalozi hao ilifanyika Ikulu jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Kabla ya kuwaapisha mabalozi hao, Rais Magufuli aliongoza kikao cha Baraza la Mawaziri kilichofanyika Ikulu jijini.

# Bosi WB akunwa mafanikio Tasaf

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI Mkazi wa Benki ya Dunia, Bella Bird, ameipongeza Serikali ya Tanzania kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini, unaosimamiwa na Mfumo wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), kwa juhudi zake za kukomesha umaskini huku akishauri uendelee kuboreshwa na kutunzwa.

Mkurugenzi huyo ambaye anaondoka nchini baada ya kuteuliwa kufanya majukumu makubwa zaidi, ameitaja Tasaf kama moja ya silaha kubwa za kumaliza umaskini na kuboresha maisha ya Watanzania.

Akizungumza katika hafla ya kumuaga jijini Dar es Salaam jana kwenye ofisi za Tasaf, Bird alionyesha kufuruhishwa kwake na namna Serikali ya Tanzania ilivyosimamia vizuri miradi ya kutokomeza umaskini na namna ilivyotekeleza kwa ufanisi mpango huo wa kunusuru kaya maskini katika awamu zote za uwapo wake.

"Kabla ya kuondoka Tanzania, ninataka niongee kitu kimoja kuhusu Tasaf; kwa miaka zaidi ya minne niliishi hapa, nimeshuhudia faida nyingi kutokana na utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini.

"Tasaf ni silaha nzuri na kubwa ambayo Tanzania inayo kwa ajili ya kupambana na umaskini, hivyo ningeomba iendelee kuimarishwa na kuboreshwa," alishauri.

Kwa mujibu wa Bird, katika ufafiti uliofanyika hivi karibuni, kama kusingekuwa na Tasaf nchini, kiwango cha umaskini kingeongezeka kwa asilima mbili.

"Hivyo, kwa muktadha huo basi, tunaona ni jinsi gani mfuko huu ulivyokuwa na manufaa kwa nchi katika kupigana na wimbi la umaskini," alisifu.

Alisema kuwa tangu kuanza kutekelezwa kwa mpango huo, maisha ya Watanzania wengi maskini yamebadilika kwa kiwango kikubwa.

Mkurugenzi Mkuu wa Tasaf, Ladislaus Mwamanga, alimshukuru mwakilishi huyo wa Benki ya Dunia kwa mchango wake mkubwa katika kuhakikisha miradi ya mfuko huo inatekelezwa kwa ufanisi.

"Umekuwa mtu mwema sana kwetu, miaka hii yote tuliyokaa na wewe, umetusaidia sana katika juhudi zetu za kupambana na umaskini, umekuwa mstari wa mbele kuongea hata na wadau wa maendeleo kutoka sehemu mbalimbali ili Tasaf ipate pesa ya kutosha kutekeleza miradi," alipongeza.

Mwamanga alimwomba Bird kuwa balozi mzuri wa Tanzania na Tasaf huko anakokwenda.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo (kulia), akikabidhi kadi ya Bima ya Afya kwa Khadija Mustafa, katika uzinduzi wa kampeni za uhamasishaji wananchi kujiunga na vifurushi vya bima ya afya, jijini Arusha jana. Wa pili kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Anne Makinda na Mkurugenzi Mkuu wa mfuko huo, Benard Konga. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Waziri avunja bodi ushirika, aagiza viongozi kukamatwa

**Na Erasto Mgeni,** NJOMBE

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, ameagizwa kuvunjwa kwa bodi ya chama cha ushirika wa wakulima wa chai Lupembe Mvyulu, na kuagiza viongozi waliouza mali za ushirika huo kukamatwa haraka.

Alisema wapo viongozi waliotajwa kwenye ripoti tatu za ushirika waliouza magari, mashine na mali nyinginezo, wakamatwe wahojiwe na kuonyesha mali za wana ushirika zilipo.

"Viongozi wote wanaondolewa kwenye uongozi, viongozi wote wa bodi wachukuliwe kuonyesha mali zilipo, Mkuu wa Mkoa na vyombo vya ulinzi wafanye uchunguze wa mali na kama zimeuzwa bila utaratibu aliyehusika awajibike," alisema.

Aidha, alisema vyama vyote vya Amcos vya vijiji vifanye uchaguzi upya chini ya usimaizi wa uongozi wa mkoa na Tume ya Ushirika ili wapatikane viongozi halali, na uundwe uongozi mpya na kupata uwakilishi wa bodi mpya ili kiwanda kianze kazi.

"Yeyote anayehusika kwenye tuhuma za kuhujumu kiwanda hiki asiruhusiwe kugombea nafasi yoyote ya uongozi," alisema Bashe.

"Wanaowakilisha ushirika siyo viongozi halali wanaotakiwa kuwa bodi ya wakurugenzi, taarifa ya uchunguzi ya vyombo vya ulinzi na usalama na ya tume ya ushirika ni kweli viongozi waliongoza na kufunga kiwanda na kukisimamia kukiwa na mali nyingi, baadhi wameuza mali na fedha hazikuingia kwenye akaunti," alisema na kuongeza;

"Wameuza shamba la miti, vyuma chakavu na magari, orodha ni ndefu ya mali zilizouzwa, nasema wazi hapa Bodi ya Mvyulu inafutwa na viongozi waliotajwa kwenye ripoti wakamatwe na vyombo vya ulinzi."

Aidha, Naibu Waziri huyo aliagiza mwekezaji wa kiwanda cha chai cha Igombola kurejeshwa kuendesha kiwanda hicho na kufanyakazi zake bila kusumbuliwa.

Awali, wananchi hao walisema kuwa vyama vya Amcos vilivyopo ni vya wanafamilia, na kwamba havitambuliki kwenye vijiji. Walidai pia wamerudi nyuma kiuchumi kutokana na ubinafsi wa viongozi.

Naye Bosi Mbanga alisema alishindwa kuendelea na masomo ya kidato cha kwanza kutokana na baba yake aliyekuwa anafanyakazi kiwandani humo kusimamishwa.

"Nikiwa kidato cha kwanza kiwanda kilifungwa baba akakosa fedha za kusomesha, nimebaki kuwa mkulima wa chai na nauza hapa kiwandani, nawadai kwa miezi 11 sasa," alisema.

"Wakati mmefunga kiwanda nilikuwa kidato cha kwanza najitambua mnauza mota, mashine na friji... tulikuwa tunaona, leo mnaturudisha nyuma na kufanya maisha yetu kuwa magumu," alidai.

Naye Rehema Malekela alisema siku mali zinaondolewa kiwandani humo alilala barabarani kuzuia, lakini aliondolewa, na kwamba mali ziliondolewa na kwenda kuuzwa.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Christopher Ole Sendeka, alisema kwenye ushirika huo kuna ufisadi, na kwamba wapo wazee na viongozi ambao hawaoni makosa.

"Sipati kigugumizi kusema huu ni ufisadi mtupu, bahati mbaya mlifanya ufisadi uchaguzi wa mwaka 2015 mkaanza kuweka siasa kwa sababu ya mwavuli wa watu waliowakamata," alisema Sendeka na kuongeza:

"Mtu amechukua fedha za ushirika kifisadi, unawaghilibu watu unawapa mwelekeo wa kuingia msituni ili waweze kukulinda."

Awali, Kaimu Meneja wa kiwanda, Allen Mbafu, alisema licha ya kufungwa kwa kiwanda hicho kwa takribani miaka minane kutokana na mgogoro, lakini wameendelea kujiimarisha na kutoa ajira kwa wakazi wa Lupembe.

# Mafuriko yaacha watu 1,000 bila makazi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

ZAIDI ya watu 1,000 wamekosa makazi, baada ya nyumba 237 kubomolewa na mvua zinazoendelea kunyesha mkoani Dodoma.

Wakazi walioathirika kutokana na mvua hizo ni wa Wilaya ya Bahi, huku miundombinu ya barabara ikiharibiwa.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Mwanahamisi Munkunda, alipokuwa akizungumza jana, baada ya ziara ya kukagua maeneo yaliyoathiriwa na mvua hizo.

Katika ziara hiyo, Munkunda aliambatana na wataalamu wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi na madiwani ili kujionea uharibifu uliojitokeza na namna ya kuwasaidia watu walioathirika.

Munkunda aliyataja maeneo yaliyoathiriwa na mvua hizo ni Bahi Sokoni, Bahi Misheni, Mji Mpya na Nkogwa pamoja na vijiji vya Mbuyuni, Uhelela,

Laloi, Mugu na Nagulo. Nyumba zilizoathirika Mahi Sokoni ni 80, Mzongole 92, Uhelele nyumba 3 na Nagulo Bahi (30).

Aidha, aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari, huku akiwataka wazazi kuhakikisha watoto wanacheza kwenye maeneo salama badala ya kuogelea kwenye mito na madimbwi yaliyojaa maji.

Alisema kuna mito mingi ya maji kutoka mikoa jirani na wilaya inayoishia katika Wilaya ya Bahi, hivyo wananchi wachukue tahadhari kutokana na maji kuingia kwenye makazi ya watu.

"Ukiwaacha watoto au mtu mzima akitegemea kuwa maji yaliyopo ni yale ya siku zote, kumbe yameongezeka...tuwe makini ukiona mto umefurika usipite mpaka ujiridhishe maji yamepungua," alisema.

Hata hivyo, alisema wameomba kiasi cha Sh. milioni 400 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu yakiwamo madaraja yaliyoharibiki, na kwamba fedha hizo zimeshapelekwa na zitaanza kutengeneza miundombinu

INAENDELEA UK. 8


Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU**
*(Barua zote za kiofisi zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)*

**Mkoa wa Arusha**
Telegram: Meru
Simu: (+ 255) 027 254-1112
Faksi: (+ 255) 027 254-1112
Barua pepe:ded@merudc.go.tz
website:www.merudc.go.tz

HALMASHAURI YA WILAYA MERU DISTRICT COUNCIL

Ofisi ya mkurugenzi mtendaji,
S. L. P 462,
USA RIVER
ARUSHA
26/11/2018

**TANGAZO KWA UMMA**

**UUZAJI WA VIWANJA KATIKA MRADI WA NGURUDOTO ESTATE**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru kwa kushirikiana na Kampuni ya **ZULFIROZ ESTATE LTD** wanawatangazia wananchi wote kuwa zoezi la upimaji wa viwanja katika eneo la Ngurdoto limekamilika.

Eneo lipo karibu na Hoteli ya Ngurudoto na Shule ya St. Jude takribani Km 1.25 kutoka Barabara ya Rami iendayo Arusha National Park na Km 3.5 kutoka barabara kuu ya Moshi- Arusha. Kuna viwanja kwa ajili ya **makazi, makazi na biashara, biashara pamoja na viwanja vya matumizi ya Ibada.**

Bei ya kiwanja ni Tsh. 19,000/= kwa mita moja ya mraba. Kiwanja kinalipiwa ndani ya muda wa mwezi mmoja. Utaandaliwa hati baada ya kukamilisha malipo ya kiwanja.

Kwa yeyote anayehitaji kiwanja afike ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru kuchukua fomu na kuchagua kiwanja kuanzia tarehe ya tangazo hili.

Wananchi wote mnakaribishwa

IMETOLEWA NA:

Grace A. Mbilinyi
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU**

MKURUGEZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU
S.L.P. 462 USA RIVER
MERU - ARUSHA

215583902

# Vigogo uchaguzi Tanzania na Malawi wajadiliana

**Na Mwandishi Wetu**

UJUMBE wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Malawi (MEC)) umefanya ziara ya kikazi kwenye ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kwa lengo la kubadilishana uzoefu juu ya mambo mbalimbali yanayohusu uendeshaji wa uchaguzi.

Kwa mujibu wa taarifa ya NEC, ziara hiyo ilifanyika juzi jijini Dar es Salaam.

Ilieleza kuwa ujumbe huo wa watu 11 ambao uliongozwa na Mwenyekiti wa MEC, Jaji Dk. Jane Ansah, ulikutana na kufanya mazungumzo na Wajumbe wa NEC kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu usimamizi wa uchaguzi katika nchi hizi mbili.

Akizungumza katika kikao cha pamoja kati ya tume hizo mbili, Mwenyekiti wa NEC, Jaji Rufani (Mstaafu), Semistocles Kaijage, alionyesha kufurahishwa kwake kwa Tume ya Uchaguzi ya Malawi kuitembelea NEC ili kubadilishana uzoefu.

Alisema: "Tanzania na Malawi ni Wanachama wa Umoja wa Tume za Uchaguzi wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (Sadc), ambao mojawapo ya malengo yake ni kujengeana uwezo katika kusimamia uchaguzi.

Nafurahi kuona mmechagua kuja Tanzania ili kujifunza na kubadilishana uzoefu."

Naye Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Malawi, Jaji Dk. Ansah, aliishukuru NEC kwa kufanikisha kikao hicho cha pamoja kwani masuala mengi ya msingi yaliweza kujadiliwa.

Alisema: "Mazungumzo haya yameibua masuala mengi ya msingi kwa pande zote mbili. Sisi tunaondoka hapa tukiwa na uelewa mpana zaidi wa masuala haya yahusuyo usimamizi wa chaguzi hasa taratibu za ugawaji wa majimbo ya uchaguzi."

Ujumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Malawi ulijumuisha mwenyekiti wa tume, makamishna watano, mkurugenzi wa uchaguzi na maofisa wengine wanne.



Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum, akizungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu warsha ya siku moja iliyoandaliwa na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) mkoa huo, yenye lengo la kuwaelewesha wanawake hasa wa kiislamu juu Tanzania ya viwanda, itakayofanyika Januari 25, mwaka huu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kortini tuhuma kunaswa na 'unga'

**Na Hellen Mwango**

ABUU Kimboko (43), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, akikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi kwa kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya aina ya Heroine na kutakatisha fedha. Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salum Ally.

Upande wa Jamhuri ulionGozwa na Mawakili wa Serikali, Elia Atanas na Tully Helela.

Atanas alidai kuwa, kati ya Desemba Mosi na 29 mwaka jana, akiwa Mbagala Zakhem wilayani Temeke jijini, Kimboko alijihusisha na biashara ya dawa za kulevya aina ya Heroine zenye uzito wa gramu 273.45. Upande wa Jamhuri pia ulidai kuwa, kati ya Desemba Mosi na 29 mwaka jana, katika Jiji la Dar es Salaam, mshtakiwa alijipatia na kutakatisha Sh. 990,000 huku akijua kuwa fedha hizo ni zao la biashara ya dawa za kulevya. Hata hivyo, mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi mpaka itakapopata kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP).

Upande wa Mashtaka, ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo uko hatua za mwisho kukamilika na uliomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa Januari 28 mwaka huu na mshtakiwa apelekwe rumande.

# Uchinjaji minadani wapigwa marufuku

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BODI ya Nyama Tanzania, imepiga marufuku uchinjaji wa mifugo kwenye machinjio yasiyo rasmi ikiwamo minada kwa kuwa una hatarisha afya za walaji.

Marufuku hiyo ilitangazwa jana na Kaimu Msajili wa Bodi hiyo, Imani Sichalise, baada ya kukagua machinjio ya kisasa ya Dodoma (TMC).

Alisema ni lazima kuchinja mifugo kwenye machinjio rasmi ya serikali, kwamba na mtu yeyote atakayekamatwa akichinja nje ya machinjio hayo atakamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

"Napiga marufuku uchinjaji wa mifugo holela hapa jijini, sehemu za minada sio sehemu za kuchinjia, tumebaini kuna watu wanachinja nyama katika maeneo yasiyo rasmi, hivyo kuhatarisha afya za walaji," alisema.

Naye daktari msimamizi wa machinjio hayo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Mariki Meljory, alisema taratibu za ukaguzi zinafuatwa vizuri katika kuhakikisha nyama inayotoka katika machinjio hayo inakuwa safi na salama, na kwamba haiwezi kuwa na madhara yoyote kwa binadamu.

Nipashe ilitembelea maduka mbalimbali ya nyama na kuzungumza na wafanyabiashara wa kitoweo hicho, ambao walikiri kuwapo na uchinjaji holela, huku baadhi ya wananchi wakitaka kuwapo kwa uchunguzi wa kina wa nyama inayouzwa.

Mkazi wa Dodoma, Naomi Cheseo, alisema kama machinjio ya TMC hayatumiki ipasavyo, kuna haja ya kufanya uchunguzi kwa kuwa kuna uwezekano nyama zinauzwa bila kupimwa na kuhatarisha afya za walaji.

Mkazi mwingine, John Mahikwi, aliziomba mamlaka zinazosimamia nyama inayoingia sokoni kufanya ukaguzi wa hali ya juu ili kuwabaini wale wanaokiuka taratibu.

Kwa mujibu wa TMC, ina uwezo wa kuchinja ng'ombe 150 hadi 200 kwa siku, hivyo kukidhi mahitaji ya nyama kwa Mkoa wa Dodoma.

Desemba 28, mwaka jana, serikali ilivunja mkataba wa mauzo ya mali za machinjio ya Dodoma kati yake na kampuni ya NICOL uliosainiwa mwaka 2008, huku ikiitaka kampuni hiyo kulipa zaidi ya Sh. bilioni 14.96 za madeni ya TMCL na mapunjo katika biashara ya machinjio kwa serikali.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, katika kikao cha wadau kujadili namna ya kunusuru machinjio hayo, alisema huduma za uchinjaji zitaendelea kutolewa kama kawaida katika kipindi cha mpito chini ya usimamizi wa serikali wakati mchakato wa kumpata mwekezaji mahiri wa mpito na wa kudumu ukiendelea.

"Katika kipindi cha muda mfupi machinjio ya Dodoma itafufuliwa na kupanuliwa na kuwa ya kisasa zaidi," alisema.

HABARI KITAIFA

# Mmiliki wa Oryx kizimbani tena

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MFANYABIASHARA maarufu jijini Arusha, Shabiby Virjee, anayemiliki kituo cha mafuta cha Oryx na wenzake wawili, wanaokabiliwa na kesi ya kutoa na kupokea rushwa ya Sh. milioni 10, wamefikishwa kwa mara ya pili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha.

Wengine waliopanda kizimbani ni aliyekuwa askari polisi jijini hapa, Paulo Erasmo na mfanyakazi wa kampuni hiyo, Nkenzi Pazi.

Wakili wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Arusha, Hamidu Singano na Richard Jacopiyo walidai mbele ya Hakimu Mfawidhi Martha Mahumbuga kuwa upelelezi wa shauri hilo umekamikika lakini wanaomba tarehe nyingine kwa ajili ya watuhumiwa kusomewa maelezo ya awali.

Hakimu Mahumbuga, baada ya maelezo hayo, aliridhia na kuahirisha kesi hiyo hadi Februari 13, mwaka huu, na kuwataka washtakiwa ambao wako nje kwa dhamana, kuhakikisha wanafika mahakamani siku hiyo bila kukosa.

Washtakiwa hao wanatetewa na Wakili Godluck Michael na Sambo Gwakisa katika mashtaka yao mawili.

Mapema Januari, mwaka huu, washtakiwa hao walisomewa mashtaka ikidaiwa kuwa Virjee anashtakiwa kutoa rushwa ya Sh. milioni 10 ili kumpatia askari polisi Meshack Laizer aliyekuwa amewakamata wafanyakazi wawili wa kampuni ya Oryx wakiuza mafuta kinyume cha sheria ili awaachie.

Wakati huo huo, Takukuru mkoani Arusha, inatarajia kumfikisha mahakamani askari polisi mkongwe Sajenti Michael Njau ambaye ni mpelelezi wa makosa ya jinai katika Kituo Kikuu cha Polisi Arusha.

Njau anatuhumiwa kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 650,000 kati ya Sh. milioni 1.5 alizokuwa ameomba kutoka kwa ndugu wa mtuhumiwa.

Mkuu wa Takukuru mkoani wa Arusha, Frida Wikesi, alieleza Nipashe kuwa mtuhumiwa katika utekelezaji wa majukumu yake ya upelelezi wa kesi ya jinai alishawishi na kupokea rushwa, kutoka kwa mmoja wa ndugu wa mtuhumiwa ambaye alikuwa anachunguza kesi yake, ambaye alimshikilia mahabusu kwa zaidi ya siku 20.

Alisema mtuhumiwa huyo akiwa na mwenzake, Mohamed, walikamatwa wakiwa wamepokea Sh. 650,000 sehemu ya fedha hizo na wanatarajiwa kufikishwa mahakamani muda wowote.

# Eneo mauzo mazao ya mifugo lafungwa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

BODI ya Nyama Tanzania imefungia eneo linalotumika kwa mauzo ya mazao ya mifugo katika Manispaa ya Morogoro na kutoa onyo kali kwa watakaoendelea kufanya shughuli hiyo.

Kaimu Msajili wa Bodi ya Nyama, Imani Sichwale, akiongozana na askari polisi, walifika jana kwa kushtukiza katika eneo maarufu kwa kuuza mazao ya mifugo kama miguu ya ng'ombe (kongoro), mikia na vichwa lililoko karibu na machinjio ya nyama na kubainisha kuwa eneo hilo si rasmi kwa ajili ya biashara hiyo.

Baada ya kubainisha hilo, Sichwale alifunga eneo hilo na kuonya watakaoendelea na kazi hiyo watachukuliwa hatua.

Alisema sababu za kufunga eneo hilo ni kutokana na serikali ilishapiga marufuku uuzaji wa nyama maeneo ya wazi kwa kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kutokea magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu kwa sababu wadudu kama nzi huruka ovyo, hivyo si vyema biashara ya chakula kufanyika holela.

"Kuna kanuni na Sheria ya Nyama Namba 10 ya mwaka 2006 inayoeleza wazi na kupinga uuzaji wa nyama katika maeneo ya wazi," alisema.

Sichalwe alisema walishamwandikia Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro juu ya kufunga eneo hilo, lakini kwa muda mrefu biashara hiyo iliendelea na kusababisha wananchi kulishwa vibudu kutokana na kutokuwapo usimamizi wa kutosha na kukagua nyama inayouzwa.

"Mkoa wa Morogoro umekuwa na wizi mkubwa wa mifugo na wezi wengi wamekuwa wakijificha katika eneo hili kwa kuchinja nyama holela porini na kuja kuuzia katika maeneo kama haya, hivyo kufungwa kwake kutapunguza wizi wa mifugo mkoani hapa," alisema.

Daktari wa Mifugo Manispaa ya Morogoro, Peter Lema, alibainisha kuwa soko hilo limekuwa kero kwa muda mrefu na tayari walishamwandikia barua mmiliki wake bila mafanikio, aliipongeza bodi kwa kuweka nguvu katika suala hilo.

Nao wafanyabiashara wa nyama katika eneo hilo wakiongozwa na mwenyekiti wao, Abeid Matonya, walisema wamekuwa wakifanya biashara katika eneo hilo kwa muda bila matatizo na kwamba wanachouza si nyama bali ni mazao ya nyama ambayo si rahisi kuuziwa buchani.

"Ukienda buchani kununua nyama ukitaka mkia au kongoro huwezi kupata kwa vile huwezi kuwasha moto ukaanza kukwangua miguu au mkia ndiyo maana huwa tunakuja kuchomea huku. Serikali inapofanya uamuzi wake, iangalie na watu kama sisi," alisema John Stambuli, mmoja wa wafanyabiashara hao.

Naye mfanyabiashara wa vyakula, Latifa Ramadhani, alisema wamekuwa wakiendesha maisha yao kwa kutumia eneo hilo kwa kununua baadhi ya mazao ya mifugo kama utumbo, miguu na mkia, hivyo akaiomba serikali kuandaa eneo lingine kwa ajili ya kufanyia shughuli hizo.

**"Mkoa wa Morogoro umekuwa na wizi mkubwa wa mifugo na wezi wengi wamekuwa wakijificha katika eneo hili kwa kuchinja nyama holela porini na kuja kuuzia katika maeneo kama haya, hivyo kufungwa kwake kutapunguza wizi wa mifugo mkoani hapa."**




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mpango mabasi yote tiketi kielektroniki uharakishwe

**CHAMA** cha Wamiliki wa Mabasi (Taboa), kimesema kinatarajia kuanza kukatisha tiketi kwa njia ya kielektroniki mwezi ujao kwa kampuni zote za mabasi ili kupunguza msongamano unaojitokeza.

Katibu wa chama hicho, Enea Mrutu, ndiye aliyebainisha kuanza kutekelezwa kwa mpango huo, na kwamba baada ya kikao chao na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), wamekubaliana ukatishaji tiketi ufanyike kwa njia ya elektroniki kuanzia mwezi ujao kwa mabasi yote.

Alieleza kuwa kama TRA haitawaangusha kuhusiana na mambo waliyokubaliana, basi mpango huo utaanza rasmi Februari.

Kwa mujibu wa Mrutu, wamiliki wa mabasi hayo wanahitaji kufanya kazi kwa kwenda na teknolojia mpya, na kwamba utaratibu huo ambao ulioanza katika baadhi ya kampuni za mabasi, utatumika kwa kampuni zote za mabasi baada ya kukamilika kwa baadhi ya mambo waliyokubaliana kisha utazinduliwa rasmi na kuwekwa agizo kwa mabasi yote.

Alisema mfumo huo utasaidia kuwarahisishia wateja kupata tiketi au kuweka maombi ya kukata tiketi kwa njia ya mtandao.

Kwa wale ambao wamekuwa wakitumia usafiri wa mabasi ya kampuni zinazotumua mfumo wa tiketi za kielektrokini bila shaka ni mashahidi kwamba ni mzuri na wa kistaarabu.

Kwamba anayetarajia kusafiri anapata toketi bila usumbufu na kwa uhakika, kwa kuwa unampunguzia muda na gharama nyingine za kwenda kukata tiketi kwenye stendi na ofisi za mawakala wa kampuni za mabasi.

Pia, mfumo huo unamwondolea uwezekano wa kutapeliwa na matapeli waliotapakaa maeneo mbalimbali wakijiita ni mawakala wa mabasi. Utapeli huo ni wa kuuziwa tiketi, lakini msafiri baada ya kupanda basi anakosa namba ya kiti.

Vile vile, kuna vibaka katika maeneo yanayozunguka stendi za mabasi kama ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, ambao wakati mwingine huwaibia abiria fedha na mizigo pamoja na kuwabughudhi.

Kwa hiyo ni jambo la kupongeza kuona kwamba wamiliki wote wa mabasi wakiona umuhimu na faida za kutumia mfumo huo ili huduma za usafiri na usafirishaji kuwa za kisasa na uhakika.

Tunafahamu kuwa mbali na mfumo huu kuwa wa kisasa na rafiki, baadhi ya watu watakosa kazi hususan wanaojipachika majina ya uwakala.Hata hivyo, faida zitakuwa nyingi kuliko athari.

Mojawapo ya faida, ni kwamba serikali itapata kodi yake stahiki. Tunasema hivyo kwa sababu mfumo wa sasa una mianya ambayo inasababisha serikali isipate kodi halisi wanazopaswa kulipa wasafirishaji wa mabasi.


Sisi tunaunga mkono kuanzishwa kwa mfumo huu wa kisasa, tukiamini kuwa utasaidia kuboresha usafiri wa mabasi, kuwa wa kistaarabu na wa uhakika kwa kuwa utawaondoa wajanja, matapeli na wababaishaji waliokuwa wakisababisha usumbufu.

Tunaamini kuwa wamiliki wote wa mabasi watakubali kuzingatia bila kuzua visingizio visivyo vya msingi. Tunapata uhakika huo kutokana na kampuni zinazoutekeleza kutolalamika hadi sasa.

Tunazishauri mamlaka husika za serikali hususan TRA kutekeleza makubaliano yake na Taboa yaliyobakia haraka iwezekanavyo ili mfumo huo uanze kazi kama ilivyopangwa mwezi ujao.

Kama kuna mambo hayajawekwa sawa, ni vizuri kuutumia muda uliobaki kuyasawazisha ili kuondoa uwezekano wa utekelezaji wake kuanza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mtanzania, kadi yako, kura yako nenda leo kajiandikishe

Na Sabato Kasika

**TANZANIA** inatarajia kufanya uchaguzi mkuu wa madiwani, wabunge na rais mwishoni mwa mwaka huu. Watakaofanikiwa, watashika nyadhifa katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Katika kufanikisha uchaguzi huo, kuna mambo mbalimbali yanaendelea kufanyika nchini, hasa uboreshaji wa Daftari za Kudumu la Wapigakura, pia utoaji elimu ya mpigakura.

Mambo hayo mawili yanaendelea kufanyika kwenye mikoa mbalimbali nchini na wananchi wamekuwa wakihimizwa kujitokeza kujiandikisha na pia kupokea elimu hiyo kwa manufaa yao.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec), inaboresha daftari hilo, ikieneza kaulimbiu isemayo: “Kadi yako, kura yako nenda kajiandikishe” ambayo ni rasmi kwa kuhamasisha umma kutambua umuhimu wa kujiandikisha. Ni kwa azma hiyo, asasi za kiraia nchini zimepewa jukumu kubwa la kutoa elimu ya mpigakura kwa ajili ya kutekeleza kikamilifu mambo hayo muhimu ya kikatiba na kidemokrasia.

Kutokana na umuhimu huo, mwaka jana Nec iliteua asasi za kiraia zaidi ya ishirini, kwa ajili ya kazi hiyo, ili kusaidia Watanzania wakiwamo vijana kutambua umuhimu wa kupiga kura.

Hadi sasa, NEC inaendelea na kazi ya kuboresha Daftari za Kudumu la Wapigakura katika mikoa mbalimbali, ili kuwawezesha Watanzania kupiga kura siku ya uchaguzi mkuu.

Mwenye sifa ya kupiga kura ni yule aliye na kadi ya mpigakura, vinginevyo hawezi kuruhusiwa, ndiyo maana Nec inafanya jitihada kuhakikisha kila Mtanzania aliyefikisha umri wa kupigakura aandikishwe. Ikumbukwe, uboreshaji wa daftari hilo unaenda sambamba na uandikishaji wapigakura wapya waliotimiza umri wa miaka 18 na zaidi na wale watakaotimiza umri huo ifikapo siku ya uchaguzi huo mwaka huu.

Wahusika wengine ni wote ambao wana sifa, lakini hawakujiandikisha mwaka 2015, kutoa kadi mpya kwa wapigakura waliopoteza kadi zao, kadi mpya kwa wapigakura, ambao kadi zao zimeharibika.

Aidha, uboreshaji huo unahamisha taarifa za wapigakura waliohama kata au majimbo na kwenda katika maeneo mengine ya uchaguzi na kurekebisha taarifa za wapigakura, ambazo zilikosewa.

Taarifa za wapigakura zilizokosewa, ni pamoja na majina na kuna kuondoa wapigakura waliopoteza sifa kama vile waliofariki dunia.

Hayo yote na mengine ni muhimu Watanzania wapewe elimu ya mpigakura, ili waelewe kuwa wao ni wadau muhimu katika zoezi linaloendelea sasa la uboreshaji wa daftari hilo, wasiachwe nyuma katika uchaguzi mkuu ujao.

Kinachotakiwa ni Watanzania kutambua kuwa wakijiandikisha, watapata kadi na ndiyo itakayowawezesha kushiriki, katika uchaguzi mkuu kwa ajili ya kuwapata viongozi wanaowataka.

Wale ambao, hawajapata elimu ya mpigakura, wafikiwe mapema ili nao wajue kuwa sifa muhimu ya kuwawezesha kupiga kura siku ya uchaguzi mkuu ni kuwa na kadi ya mpigakura tu.

Uboreshaji daftari ulianza rasmi Julai mwaka jana mkoani Kilimanjaro, baada ya uzinduzi uliofanywa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa.

Katika uzinduzi huo, Waziri Mkuu alihimiza vijana waliotimiza umri wa miaka 18 kujitokeza kwa wingi kujiandikisha, ili wawe na sifa ya kushiriki katika uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika mwishoni mwa mwaka huu.

Waziri Mkuu akakumbusha kuwa, bila kujiandikisha hawawezi kutumia haki yao ya msingi ya kuchagua viongozi wanaowataka. Hivyo, kujiandikisha kwao kutawahakikishia ushiriki, katika uchaguzi wa viongozi.

Pamoja na hayo, anaziasa asasi za kiraia zilizopewa vibali vya kutoa elimu ya mpigakura, kujiepusha na ushabiki wa kisiasa, badala yake zizingatie mwongozo wa elimu ya mpigakura uliotolewa na Nec.

Uchaguzi hasa wa viongozi katika nchi, ni mchakato rasmi unaoendeshwa kwa mujibu wa sheria kuwezesha wananchi kuwapigia kura watu, ambao wanawataka waongozwe nao kwa kipindi fulani.

Njia pekee ya kufikia hatua hiyo ni kufuata kile ambacho kinaelekezwa na Nec kwamba ni lazima mtu mwenye sifa za kupiga kura aandikishwe kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura na kupata kadi.

HABARI KITAIFA



Rais John Magufuli akiongoza kikao cha Baraza la Mawaziri, Ikulu, jijini Dares Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# RC aagiza mkataba ujenzi kuvunjwa

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, ametoa siku saba kwa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) kuvunja mkataba na mkandarasi wa kampuni ya Juniour Construction anayekarabati barabara ya Naiyobi mpaka eneo la View Point kwa kiwango cha changarawe.

Gambo amefikia hatua hiyo baada ya kutoridhishwa na kasi ya ujenzi licha ya mkandarasi kuongezewa miezi mitano badobarabara haipitiki.

Akizungumza katika ziara yake ya kukagua miradi ya ujenzi wa barabara juzi, wakati akikagua barabara hiyo iliyotengewa Sh. bilioni 1.39, Gambo alieleza kusikitishwa na mkandarasi huyo licha ya umuhimu wa barabara hiyo kwa watalii wanaotembelea Ngorongoro huku akisema hiyo ni sawa na hujuma kwa taifa.

Gambo alisema Bodi ya NCAA ikae na kufanya uamuzi wa kuvunja mkataba kwa kufuata taratibu zote kwa kuwa barabara hiyo ya kilomita 78 imekarabatiwa kilomita 14 pekee na hizo pia haziko katika hali ya kuridhisha, hivyo hatua zichukuliwe dhidi yake.

"Natoa siku saba kwa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kuvunja mkataba wa huyu mkandarasi anayekarabati hii barabara ya Naiyobi mpaka View Pointi maana kazi yake hairidhishi kabisa japo ameongezewa siku tano," alisema Gambo.

Pia aliitaka mamlaka hiyo kuangalia namna mkandarasi huyo alivyopatikana kwa kuwa ameonekana kutokuwa na sifa kutokana na utendaji wake mbovu unaokwamisha miradi ya barabara.

Naye Kaimu Kamishna wa NCAA, Asangye Bangu, alisema wamepokea agizo hilo hilo na watalitekeleza kwa haraka ili kutatua changamoto ya miundombinu mibovu na kuhakikisha barabara zinapitika.

# Daraja lakwamisha shule kufunguliwa

**Na Dege Masoli,** KOROGWE

ZAIDI ya wanafunzi 600 katika Shule ya Sekondari ya Magoma wilayani Korogwe, wameshindwa kwenda shule baada ya daraja lililosombwa na maji kutopatiwa ufumbuzi mpaka sasa.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Korogwe, Nassoro Hemed, alisema juzi kuwa licha ya suala hilo kulalamikiwa ngazi mbalimbali ikiwamo kwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Elias Kuandikwa, alipofanya ziara wilayani hapa kukagua hali halisi ya uharibifu uliyofanywa na mvua hizo, bado halijatengenezwa.

Hemed aliliambia gazeti hili kuwa mpaka sasa wanafunzi wapatao 600 wamekwama kwenda shuleni licha ya wenzao kuanza masomo kutokana na daraja hilo muhimu linalounganisha vijiji sita kusombwa na maji tangu Novemba, mwaka jana.

Alisema watoto hao ni wale wanaotoka vijiji vya jirani na Magoma yaliko makao makuu ya Kata ambao mpaka wafike shuleni hapo, lazima wavuke daraja.

Alisema kutokana na mvua kusomba daraja hilo, sambamba na wanafunzi hao, wakazi wa vijiji sita wamekosa mawasiliano ya barabara, hivyo kuongeza gharama ya mahitaji ya kibinadamu ya kila siku ambayo walikuwa wakiyapata Magoma.

Kwa mujibu wa Hemed, wakazi wa vijiji hivyo wana hali mbaya licha ya kuwa na mazao kwa kuwa hakuna soko na wanunuzi hawafiki katika maeneo yao na wanapolazimika kuyavusha kunakuwa na ongezeko la gharama.

Alivitaja vijiji vilivyoathirika kuwa ni Mkwajuni, Folofolo, Mavumba, Kitivo, Kwenkeyu na Magoma ambavyo hadi sasa wakazi wake hawajui hatima ya maisha yao kutokana na maeneo ya vijiji hivyo kuwa kama kisiwa.

Mwenyekiti huyo aliiomba serikali kuingilia kati changamoto hiyo ili kujengwa daraja hilo na kueleza kutambua jitihada zinazofanywa katika kutatua kero za wananchi.

# Mkandarasi stendi aiangukia serikali

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KAMPUNI ya ujenzi ya CRJE (East Africa) Ltd, imeiangukia serikali ikiomba kulipwa Sh. bilioni 10 za kumalizia ujenzi wa kituo cha mabasi cha kimataifa cha Ngangamfumuni, Manispaa ya Moshi.

Mradi huo mkubwa wa kimkakati unaotekelezwa kwa fedha za ndani, licha ya kutakiwa kukamilika katika muda wa miezi 24, umefikia asilimia 30.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, aliyetembelea na kukagua maendeleo ya mradi huo jana, alithibitisha kupokea ombi hilo la mkandarasi.

Akiwa katika eneo la utekelezaji wa mradi huo, Mghwira alisema mkandarasi huyo ameiomba serikali kumwongezea fedha licha ya kutaka kujenga mradi huo kwa fedha zake na kisha kuukabidhi serikalini.

Kituo kikuu cha mabasi cha Ngangamfumuni, ujenzi wake umepangwa kutekelezwa kwa zaidi ya Sh. bilioni 27 na utatekelezwa kwa awamu tatu.

Mghwira alisema: "Nimeongea naye (mkandarasi) ameomba serikali kuridhia kwenye ule mkataba apewe Sh. bilioni 10, anasema yeye atamaliza mradi na angetukabidhi. Kuna kazi nyingine asingeweza kuchukua sehemu nyingine mpaka amalize kazi.

"Kwa kweli ni kwamba hiyo stendi ujenzi wake hausuisui kwa sababu fedha zimekuwa zikitoka kwa awamu tofauti tofauti. Hii wanayosema Manispaa kwamba amekwishalipwa fedha na hadai ni ya sasa. Kabla ya hapo amekuwa akidai na yeye ndiye ana kasi kubwa sana na wala si mkandarasi mbabaishaji kama makandarasi wengine, kwa kweli anajitahidi na anafanya kazi zake kwa wakati," alisema.

Alisema kinachotakiwa kwa sasa ni halmashauri kukaa naye na kukubaliana wapeleke mahitaji ya kuendelea na kazi ikiwamo hati ya uthibitisho wa kazi baada ya ukaguzi na kujiridhisha.

"Kwa sababu mkandarasi ametaka sana mara nyingi akisema hata angeongezewa fedha kiasi tu, asilimia 35 ya mradi mzima angejenga amalize na abaki kudaiana na sisi kwa sababu ana kazi nyingine ambazo anashindwa kuzichukua kwa sababu hajamaliza kazi hii," alisema Mghwira.

Kituo hicho ni mradi mkakati uliopitishwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) na awali ulitengewa Sh. bilioni 9.5.

## Kiti cha Lissu kaa la moto Chadema

INATOKA UK. 2

Maendeleo (Chadema) kwa imani aliyoionyesha kwake hadi kumteua kukaimu nafasi hiyo baada ya Lissu kupigwa risasi.

"Licha ya kuwasimamia na kuwaongoza bungeni wabunge wenzangu, uteuzi na nafasi hiyo ilinipa fursa ya kuhudhuria na kukuwakilisha katika kamati mbili muhimu za Bunge, yaani Kamati ya Uongozi na Kamati ya Kanuni na hivyo kunipa uzoefu mkubwa wa uendeshaji wa shughuli za Bunge," inasomeka sehemu ya barua hiyo.

Kwa mujibu wa Selasini, baada ya kutafakari kwa kipindi chote alichotumikia nafasi hiyo, amebaini kuwa kwa miaka yote miwili hajapewa barua rasmi ya kukaimu rasmi wala kuthibitishwa katika utumishi huo."Vilevile, hujawahi kunipa onyo lolote la mdomo au maandishi kuonyesha kuwa huridhishwi na utendaji wangu.

"Na kwa kuwa Ofisi ya Bunge haina uthibitisho wowote wa mdomo au maandishi wa mimi kukaimu nafasi hiyo, hivyo basi, nakutaarifu kwamba nimejiuzulu nafasi hii kuanzia tarehe ya barua hii ili nikupe nafasi ya kufanya uamuzi wa kumteua mbunge mwingine atakayetuongoza katika kipindi kilichobakia cha uhai wa Bunge hili," Selasini anaeleza katika barua yake hiyo.

**MAJIBU YA MBOWE**

Alipofutwa na Nipashe kuzungumzia suala hilo, Mbowe alimtupia lawama Selasini kwa uamuzi wake huo aliodai hauna mashiko.

"Kama hakupewa barua ya kuteuliwa, amewezaje kuandika barua ya kujiuzulu? Kama amefanya kazi zake vizuri, wabunge wote wanamheshimu, wanamsikiliza, uongozi wa Bunge unampa ushirikiano kwa miaka miwili sasa, anashindwaje kumalizia miezi minne iliyobaki?

"Anakwenda kwenye vikao, anapokea posho za vikao bila kikwazo chochote, hakuna anayemzuia, shida iko wapi? Yeye aseme tu, kama ana mambo yake ya siri," alisema na kuonyesha kutofurahishwa na uamuzi huo wa mbunge wa chama chake.

Lissu alishambuliwa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana Septemba 7, 2017 wakati anajiandaa kushuka kwenye gari nyumbani kwake Area D mjini Dodoma, muda mfupi baada ya kumalizika kwa kikao cha mchana cha Bunge ambacho alichangia hoja.

## Mafuriko yaacha watu 1,000 bila makazi

INATOKA UK. 3

hiyo.

"Serikali iko makini kuhakikisha shughuli za kiuchumi hazisimami kwa sababu ya mvua zinazoendelea kunyesha," alisema.

Alibainisha kuwa mito mingi imeacha njia zake za asili, hali inayosababisha hata maji kupita juu ya madaraja na wananchi kushindwa kuvuka kwa kuhofia usalama wao.

Mkuu huyo wa wilaya aliagiza kukarabatiwa kwa daraja la Mto Nkigwa ambalo limeanza kukatika kutokana na mvua hizo.

Naye Diwani wa Kata ya Bahi, Augustino Ndonu, alisema juzi mvua ilinyesha kuanzia saa nne usiku hadi jana alfajiri na kusababisha mito kufurika na maji kujaa kwenye makazi ya watu.

Ndonu alisema kwenye baadhi ya maeneo wananchi walijitolea kujaza mchanga kwenye mifuko na kuziba kwenye kingo za mito ili kupunguza kasi ya maji kuzunguka makazi ya watu.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Bahi Sokoni, Fredrick Kachiwile, alisema katika Kijiji cha Nagulo, barabara ilikatika na kusababisha kukatika kwa mawasiliano na maeneo mengine jirani.

# Upandikizaji uloto kuanza Mloganzila

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili Tawi la Mloganzila, inatarajia kuanzisha huduma ya upandikizaji uloto mwezi ujao. Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Muhimbili Tawi la Mloganzila, Dk. Julieth Magandi, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na maofisa mawasiliano wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, waliotembelea hospitali hiyo jijini Dar es Salaam.

Maofisa habari hao wako katika ziara ya kampeni ya kukagua mafanikio ya serikali katila sekta ya afya ijulikanayo kama 'Tumeboresha Sekta ya Afya'.

Dk. Magindi alisema kwa kushirikiana na Muhimbili, huduma hiyo kwa mara ya kwanza itaanza kutolewa katika tawi hilo na maandalizi yamekamilika.

"Ifikapo Februari mwaka huu tunatarajia kuanza kutoa huduma ya upandikizaji wa uloto, huduma hii kwa sasa nchini haipo," alisema.

Aliongeza kuwa wana mpango wa kuanzisha huduma ya kuondoa mawe kwenye figo kwa njia ya kitaalamu, wakitumia mionzi.

Alisema huduma hiyo inatarajiwa kuanza kutolewa siku za karibuni baada ya kukamilika kwa taratibu za kitaalamu zinazofanyika.

Pia, alisema wamejipanga kuimarisha huduma za wagonjwa mahututi (ICU) na wanategemea kupokea wataalamu sita kutoka Cuba ambao wamebobea katika huduma hizo.

Alisema wataalamu hao wanatarajia kuwasili nchini hivi karibuni kwa ajili ya kuanza kazi hiyo.

Dk. Magindi alisema wanaendelea kudhamini mafunzo ya kibingwa kwa watumishi wao na tayari wameshadhamini watumishi 45 ambao wanasoma fani mbalimbali za kibingwa.

Kuhusu utoaji huduma wa hospitali hiyo, tangu ilipowekwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Afya Oktoba 3 mwaka juzi, alisema kumekuwa na ongezeko la wagonjwa wa nje kutoka 17,116 katika robo ya mwaka 2018 (Julai hadi Septemba mwaka 2018) hadi kufikia wagonjwa 24,945 katika robo mwaka uliofuata (Oktoba hadi Desemba 2019), sawa na ongezeko la asilimia 46.



Dereva wa bajaj, akibadilisha tairi baada ya kupata pancha eneo la Kitunda, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Walalamikia tozo duara la madini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo wa mgodi wa Kalemaela Gold Rush ulipo kijiji cha Buswangili Kata ya Bulyanuhuru, Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wameulalamikia uongozi wa mgodi huo kwa kuwatoza shilingi 150,000 kwa kila duara moja.

Malalamiko hayo yalitolewa na wachimbaji wadogo kwa Ofisa Madini mkazi Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Joseph Kumburu, akipokwenda kutatua mgogoro unaoendelea kati ya wachimbaji na uongozi wa mgodi.

Mmoja wa wachimbaji, Nyang'anyi Mwita, alisema awali walikuwa wakichimba madini katika mgodi huo, na yalipopungua walielekea mgodi wa namba tisa Kata ya Bulyanhuru, lakini waliporejea katika eneo lao, uongozi wa mgodi unawatoza kiasi hicho cha fedha. Aliongeza: "Tuliporejea katika maduara yetu katika mgodi huu tunashangaa kuona uongozi ukitutoza faini ya shilingi 150,000 kwa madai kwamba tuliwaambia na kuelekea kwenye mgodi mwingine."

Mwita aliendelea kumweleza Mhandisi Kumburu kuwa wachimbaji wote walikubaliana kuwalipa kiasi hicho cha fedha na baadaye waliondoka kutafuta wafanyakazi wa machimbo hayo, lakini cha kushangaza waliporudi na wafanyakzi wao walikuta maduara yao yameuzwa tena.

Naye Mwenyekiti wa chama cha wachimbaji wadogo wilayani Kahama (SHIREMA), Nochodemas Majabe, alisema serikali inafahamu kila kitu kinachoendelea katika mgodi huo, na kuwataka kuacha mchezo wa kucheza na dhabau badala yake kila mchimbaji apate haki yake.

Mhandisi Kumburu alisema alikiri kupata malalamiko ya wachimbaji wadogo kunyang'anywa maduara na kutozwa shilingi 5,000 kila wiki na shilingi 1,000 getini kila siku na watu wawili tofauti.

Kumburu aliomba Taasisi ya Kupamba na Kuzuia Rushwa (Takukuru) kupeleleza na kutambua shilingi 5,000 na shilingi 1,000 zilizokuwa zikitozwa na uongozi wa mgodi huo zilikuwa zinakwenda wapi, licha ya uongozi huo kutojenga hata choo.

HABARI KITAIFA

# Wasiojulikana wabaka mtoto, wamuua kikatili

**Na Neem Hussein,** KATAVI

MTOTO wa miaka 10 Levana Oscar, mwanafunzi wa darasa la nne Shule ya Msingi Katisunga, amefariki dunia, baada ya kubakwa kisha kupigwa kwa jiwe kichwani na mwili wake kutupwa porini na watu wasiojulikana.

Tukio hilo lilitokea siku chache zilizopita katika Kijiji cha Society Halmashauri ya Nsimbo mkoani Katavi baada ya mtoto huyo kwenda kuchota maji kwenye dibwi lililopo pembezoni mwa makazi ya watu akiwa na mwenzake. Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Magamba, Shamu Adamu Isike, alisema baada ya kufika eneo la tukio na kufanya vipimo ilionekana ni kweli mtoto huyo kafanyiwa vitendo hivyo vya kikatili.

Hata hivyo, alisema inawezekana mtoto huyo aliwafahamu wahusika wa tukio hilo baada ya kumbaka wakati akiondoka kurudi nyumbani ndipo walimfuata nyuma na kuamua kumpiga jiwe hilo kichwani.

"Ni kweli siku kadhaa zimepita niliijiwa hapa kwenda eneo la tukio...kufika kule kabla ya uchunguzi wa ndani mtoto alionekana amepigwa jiwe kwa nyuma maeneo ya kichwani hadi kupoteza maisha, ila baada ya kufanya vipimo niligundua kweli alibakwa," alisema Dk. Isike.

Baba wa mtoto huyo, Oscar Charles Nyansio, alisema kutokana na maumivu alionayo kuhusu kifo cha mwanawe anaiomba serikali imsaidie kupatikana kwa wahusika wa tukio hilo.

"Yaani sijui ata niseme nini, naumia sana moyoni mwangu... maumivu ninayopata ni makali sana niombe tu serikali inisaidie waliofanya hivyo wapatikane," alisema Nyansio.

Baadhi ya majirani waliohudhuria mazishi ya mtoto huyo, walisema walipokea taarifa kutoka kwa mtoto mwenzie ndipo walichukua jukumu la kwenda katika pori hilo kumtafuta na kufanikisha kupata mwili wake.

Tukio hili linafananishwa na tukio jingine ambalo lilitokea mwaka jana katika eneo la Makanyagio mkoani hapa ambapo mwanamke mmoja alibakwa hadi kufa wakati akitoka dukani kununua mafuta ya taa majira ya usiku.



Rundo la takataka likiwa limetelekezwa kando ya barabara katika eneo la Kigogo CCM, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana, na kusababisha usumbufu kwa wananchi na hasa wakazi wa eneo hilo. **PICHA: JOHN BADI**

# Wavuvi Mafia wataka mafunzo sheria, kanuni

**Na Beatrice Philemon**

WAVUVI katika Halmashauri ya Wilaya ya Mafia Mkoa wa Pwani wameiomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuwapa mafunzo juu ya sheria na kanuni za uvuvi ili kufahamu kitu gani kinatakiwa katika sekta ya uvuvi na kunufaika na shughuli za uvuvi.

Akizungumza kwa niaba ya wavuvi, Katibu wa Chama cha Ushirika Twendekazi Mibulani, Twaha Ismail, alisema kuwa wanaiomba serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mafia kuwapa mafunzo kwa sababu hivi sasa vijana wengi wanaomaliza darasa la saba wanajikita katika shughuli za uvuvi na wengi wao hawajui sheria za uvuvi.

Alisema ingawa vijana hao wana leseni za uvuvi kutoka halmashauri, lakini wengi wao hawajui sheria za uvuvi...wanajivulia tu na mwisho wake wanakuja kukamatwa na maofisa uvuvi.

"Tunaomba watu wa idara ya uvuvi waje kutoa mafunzo kwa wavuvi kuhusu sheria za uvuvi na siyo kuja kukamata watu tu, na mvuvi akivunja sheria hizo ndiyo akamatwe," alisema.

Alisema hivi sasa katika Wilaya ya Mafia kuna watoto wengi wa darasa la saba wanataka kuingia kwenye sekta ya uvuvi, lakini hawajui sheria za uvuvi.

Pia waliiomba wizara kuwawezesha wavuvi kuwa na vyombo vya kisasa ili waweze kwenda kwenye kina kirefu kuvua samaki.

Alisema wakazi wa Mafia hawawezi kuondokana na umaskini bila kuwa na vyombo vya kisasa.

"Asilimia kubwa ya wananchi wa Mafia, wanatumia mitumbwi midogo ambayo haiwezi kwenda mbali kuvua samaki wala kupata samaki wengi, alisema.

Wavuvi hao walisema kuwa ingawa ActionAid Tanzania wamewawezesha kupata elimu ya masuala mbalimbali ikiwamo kupewa boti ya kisasa, wanaiomba pia Halmashauri ya Wilaya ya Mafia iwawezeshe kupata elimu ya uvuvi kutoka kwa wataalamu wa Chuo cha Uvuvi Mbegani ili kufanya shughuli za uvuvi kisasa.

"Tunaomba halmashauri yetu itusaidie katika suala hili kwa sababu uvuvi tunaovua ni wa asili ambao umepitwa na wakati, tunatumia mitumbwi midogo midogo ambayo haiwezi kwenda mbali na kuwasaidia kuvua samaki wengi," alibainisha.

Vilevile wanaiomba halmashauri iwawezeshe nyenzo za uvuvi za kisasa, na kuwa wako tayari kukopeshwa kwa sababu wanafanya kazi katika mazingira magumu, ambayo ni hatarishi kwa maisha yao na kipato chao hakiongezeki.

Naye Ofisa Uvuvi wa Wilaya, Ayoub Sabu, alisema kazi ya halmashauri ni shughuli zote zinazohusiana na uvuvi endelevu, kutoa vibali maalumu vya shughuli za uvuvi, kufuga na kuvua, kutoa elimu kwa wavuvi juu ya uvuvi endelevu na kutunza viumbe maji (mwani).

Pia shughuli nyingine kubwa wanazozifanya ni kuunganisha wavuvi, wafanyabiashara kujiunga katika vikundi ili waweze kukopesheka.

Kwa sasa wizara ina mkakati wa kusaidia wavuvi kukopesheka hasa vikundi vidogo vidogo na vyama vya ushirika na pia mpaka sasa halmashauri imeunda vikundi viwili vya wavuvi katika eneo la Kilindoni.

"Mara nyingi tumeshindwa kutoa mafunzo kwa wavuvi kutokana na uhaba wa watumishi wa sekta ya uvuvi na uhaba wa bajeti ili kufikia watu hao," alisema

Wilaya ya Mafia ina wavuvi 5,133 na vyombo vya uvuvi 1,011 ikiwamo mitumbwi, boti na ngao.

# Waja juu kusuasua ujenzi kituo cha afya

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

WAKAZI wa Kijiji cha Samazi wilayani Kalambo mkoani Rukwa, wamelalamikia kitendo cha halmashauri hiyo kusuasua katika ujenzi wa kituo cha afya katika kata yao.

Wamedai kuwa hiyo inawalazimu kutembea zaidi ya kilomita 20 kutafuta huduma za afya.

Malalamiko hayo waliyatoa kwa Naibu Katibu Mkuu Tamisemi, Dorothy Gwajima, alipofanya ziara ya kikazi wilayani humo na kutembelea eneo linalojengwa kituo hicho cha afya.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Saimon Kapesa, alisema kutokana na kukosekana kwa kituo cha afya katika kata yao, wanalazimika kutembea kilometa 20 kutafuta huduma za afya katika kata nyingine, hivyo aliiomba serikali iwajengee kituo hicho cha afya haraka ili kuwaondolea usumbufu.

"Katika kijiji chetu, tunalazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilometa 20 kutafuta huduma za afya, na hii ni tabu zaidi kwa wajawazito na watoto ambapo wakati mwingine wanahitaji huduma za dharura, na pengine hata baadhi ya vifo vinavyotokea kijijini vinatokana na kukosekana kwa matibabu kwa wakati," alisema. Naye Monica Nakazwe alisema kuwa haoni sababu kwa nini kuna kusuasua katika ujenzi wa kituo hicho, ilhali serikali imeshatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho kwani kwa kufanya hivyo kunawasababishi usumbufu na gharama zisizokuwa za lazima katika kufuata huduma za afya katika vituo vya afya vya Ngorotwa na Matai, ambavyo vipo mbali na kijiji chao.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kalambo, Nicholaus Mlango, alisema serikali imetoa Sh. milioni 400 na tayari halmashauri hiyo imeshaanza ujenzi wa kituo hicho cha afya.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kalambo, Frank Sichalwe, aliishukuru serikali kwa kutoa fedha hizo na kuwa ujenzi wa kituo cha afya umeshaanza na utakapo kamilika utaondoa kero zinazowakabili wakazi wa kijiji hicho.

Gwajima alitishia kuzichukua fedha hizo Sh. milioni 400 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya, huku akimpa siku saba Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kalambo kuanza ujenzi.

# Mbunge CCM 'atesti' mitambo kwa UWT

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

VIONGOZI wa Jumuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (CWT), wametakiwa kuwafikia wananchi kwa wakati, kusikiliza changamaoto zinazowakabili na kuzipatia ufumbuzi.

Pia wametakiwa kuwaeleza mazuri yanayofanywa na serikali inayoongozwa na CCM.

Hayo yalibainishwa na Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mwanza, Kemirembe Lwota, wakati akikabidhi baiskeli 74 kwa wenyeviti na makatibu wa jumuiya hiyo ngazi ya kata kwa kata zote za wilaya za Ilemela na Nyamagana ili kuwarahisishia kazi ya kuwafikia wananchi na kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

"Viongozi wote wa jumuiya kutoka matawi, kata, wilaya na mkoa mnatakiwa kuwafikia wananchi kwenye maeneo yao kutatua kero zao na kuwaeleza miradi mikubwa inayotekelezwa na serikali ikiwamo ya upanuzi wa uwanja wa ndege, ujenzi wa reli ya kisasa, mradi wa ufuaji wa umeme, ununuzi wa ndege mpya, uboreshaji wa sekta ya afya na namna inavyotatua kero na changamoto za muda mrefu zilizokuwa zikiwakabili," alisema Lwota.

Pia aliwataka waungane na kujenga umoja na wabunge wa majimbo yao ili kuongeza kasi na urahisi wa utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi iliyonadiwa na Rais John Magufuli kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo.

Kwa upande wao Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Ilemela, Nelson Meshack na Mwenyekiti wa (UWT) Wilaya ya Nyamagana, Witness Makale, walimshukuru mbunge huyo kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatumikia wananchi waliomchagua, hivyo walimhakikishia ushirikiano katika kuwatumikia wananchi.

"Tulikuwa na changamoto ya usafiri ambayo iligeuka kuwa kero iliyochangia wakati mwingine tushindwe kutekeleza majukumu yetu ya kuwafikia wananchi kwa wakati... sasa tumepata mkombozi, hivyo tutashirikiana vyema na kuleza maendeleo na kuondoa adha zinazowakabili wananchi," alisema Makale.

# Waziri asisitiza ziara za kushtukiza viwandani

**Na Mwandishi Wetu,**
MKURANGA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, amesema ziara za kushtukiza maeneo ya viwanda ni endelevu ili kuhakikisha sheria na taratibu za kuhifadhi mazingira zinafuatwa sambamba na kuhamasisha uwekezaji wa viwanda nchini.

Akizungumza katika ziara yake wilayani Mkuranga katika Mkoa wa Pwani, Simbachawene alisema serikali inahamasisha na kuvutia uwekezaji katika viwanda kwa kuzingatia sheria na kanuni za utunzaji wa mazingira.

"Kama waziri mwenye dhamana ya mazingira nitaendelea kufanya ziara za kushtukiza sehemu mbalimbali nchini kuhakikisha kuwa uwekezaji katika viwanda hauathiri mazingira au kuleta adha kwa wananchi sehemu husika," alisema. Simbachawene alisema uwekezaji mzuri na endelevu ni ule unaojali na kulinda mazingira yanayozunguka hivyo azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025 itatekelezwa sambamba na utunzaji wa mazingira. Kauli ya waziri ilikuja kufuatia ziara ya kushtukiza kwenye kiwanda cha kuzalisha nondo cha Fujian Hexingwang kilichopo eneo la Kisemvule katika Wilaya ya Mkuranga ambapo wananchi walikuwa wakilalamikia kiwanda hicho kwa kutozingatia taratibu za utunzaji wa mazingira.

Simbachawene amewaonya wawekezaji kuacha kutumia mwanya wa ujenzi wa viwanda kwa kukiuka sheria na kanuni za mazingira na kamwe wizara yake haitamvumilia mwekezaji wa aina hiyo. "Sheria na kanuni zetu za mazingira zinawataka wawekezaji wa viwanda kupitia michakato kadhaa kabla ya kuanza uzalishaji, lakini wapo wawekezaji wanaopita njia za mkato na kuanza uzalishaji, huku miundombinu ya msingi katika viwanda hivyo vikiwa bado havijakamilika hali inayosababisha malalamiko kutoka kwa wananchi," alisisitiza Simbachawene.

Aidha, alitoa angalizo kwa viwanda ambavyo vinaendelea na uzalishaji, huku vikiwa vimekamilisha taratibu na sheria za mazingira, lakini wakati uzalishaji ukiendelea viwanda hukiuka taratibu zinazowaongoza.

"Kuna viwanda vimefuata taratibu zote kupitia NEMC, lakini wanapoanza uzalishaji hujikuta wanakiuka taratibu hizo, ofisi yangu kwa kushirikiana na NEMC tutahakikisha tunapitia viwanda hivyo na kama vitabainika kuwa na makosa basi vitapigwa faini kwa mujibu wa sheria," alisema.

Simbachawene ameyataja makosa ambayo yamekuwa yakijirudia kwa viwanda vingi ni pamoja na kutiririsha majitaka bila kuyatibu, mfumom mbovu wa utupaji taka za viwandani, hewa chafu na milipuko hali inayochangia uchafuzi wa mazingira na kuleta athari za kiafya kwa wananchi.

"Tunajenga uchumi wa viwanda ambao utaleta uwiano mzuri na ustawi wa jamii, tunawapongeza wale wote ambao wamekuwa wakitekeleza majukumu yao kwa mujibu wa kanuni na sheria za mazingira, lakini kwa wale ambao wamekuwa wakikiuka utaratibu basi watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria," alisema Simbachawene. Katika ziara hiyo, Simbachawene alikifungia pia Kiwanda cha Fujian Hexingwang kwa kipindi cha mwezi mmoja kwa ukiukwaji wa kanuni za mazingira ambapo mmiliki wa kiwanda hicho alipewa wa kukamilisha ujenzi wa miundombinu.



Mkurugenzi wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa wa Bunge, Daniel Eliufoo (kulia), akiwapatia maelezo Maofisa Waandamizi wa Jeshi kutoka Chuo cha Ulinzi cha Taifa (NDC), walipotembelea ukumbi wa Bunge, jijini Dodoma jana, kwa ajili ya kujifunza jinsi Bunge linavyofanya kazi zake. **PICHA: BUNGE**

# Sababu halmashauri kuwarejeshea wamiliki maeneo

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa, imeamua kuyarejesha kwa wamiliki maeneo iliyokuwa imeyachukua kwa lengo la kupima viwanja kisha kuviuza kutokana na kushindwa kulipa fidia ya Sh. milioni 600 kwa wamiliki wa maeneo hayo.

Akizungumza na wananchi ambao maeneo yao yalichukuliwa, Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Jacob Mtalitinya, alisema kuwa kwa sasa halmashauri haina uwezo kuwalipa fidia na wala haijui ni lini fedha hizo zitapatikana.

Alisema ili kuepuka migogoro, halmashauri imeona ni vema iwarudishie wananchi maeneo yao, isipokuwa wale ambao maeneo yao yamechukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa taasisi za serikali na ambao maeneo yao yalipimwa na kuuzwa viwanja vya makazi hao ndio watalipwa fidia.

Mtalitinya aliwaagiza watendaji wa halmashauri kuyatambua maeneo ambayo yameshatumika ili ufanyike utaratibu wa kuwalipa fidia na ambayo hayajauzwa yatarejeshwa kwa wamiliki wake ili wayalipie, na wakiamua kuyatumia ama kuyauza wao wenyewe wahakikishe wanafuata taratibu za ujenzi pamoja na taratibu za mipango miji. "Binafsi nimeona si busara kuendelea kuyashikilia maeneo hayo kwani mpaka sasa tumeyashikilia kwa miaka kumi, wananchi wanasubiri fidia, na hakuna uwezekano wa kuwalipa, ndiyo maana nimeona ni bora niyarudishie maeneo yenu mwendelee na matumizi mnayo yataka ninyi," aliwaeleza wananchi hao.

Mkurugenzi huyo alisema kwa kuwa halmashauri ina viwanja zaidi ya 600 ambavyo vimepimwa katika eneo la Nambogo, na havijapata wanunuzi, viwanja hivyo ndiyo vitakuwa vikiuzwa kwa wananchi wanaotaka kujenga makazi.

Aliongeza kuwa haoni sababu ya kuendelea kuyashikilia maeneo mengine ya wananchi, ndio maana ameamua kuyarudisha.

Mmoja wa wananchi hao, Monica Makandi, alimshukuru mkurugenzi huyo kwa uamuzi huo kwa kuwa wamechoka kusubiri fidia ambapo ni zaidi ya miaka 10 sasa, na hakuna matumaini ya kupata fedha hizo, hivyo bora wenyewe wayauze maeneo yao au wayatumie watakavyo ona inafaa.

# Wafanyakazi hawajalipwa mishahara mwaka mzima

**Na Cynthia Mwilolezi,** MIRERANI

HATIMAYE uongozi wa Kampuni ya Tanzanite One, umewalipa mshahara wa mwezi mmoja wafanyakazi wake, ili kukabiliana na ukata uliotokana na kusimamishwa uchimbaji wa madini ya tanzanite kwa miaka miwili sasa.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, baadhi ya wafanyakazi wa kampuni hiyo walidai licha ya kulipwa mshahara huo, bado wana hali ngumu ya kimaisha kutokana na malimbikizo ya muda mrefu ya mishahara. Elisamehe Msuya, mfanyakazi wa kampuni hiyo, alishukuru kwa kulipwa mshahara wa mwezi mmoja, lakini akabainisha: "Tuna miezi 13 hatujalipwa mishahara kwa kuwa uchimbaji umesitishwa katika migodi yetu, hali hii inatupa wakati mgumu."

Mkuu wa Idara ya Ulinzi wa Tanzanite One, Abubakar Lomba, alidai kulipwa mshahara wa mwezi mmoja, kumeanza kurejesha ari kwa wafanyakazi, ambao wengi walikuwa wameanza kukata tamaa.

Katibu wa Tanzanite One, Kisaka Mzava, alikiri kampuni hiyo, kulipa walau mshahara wa mwezi mmoja kwa wafanyakazi ambao wako kazini, akidai wamelipa zaidi ya Sh. milioni 40.

Alisema kampuni hiyo, imeamua kulipa mishahara japo wa mwezi mmoja, ili kuwasaidia wafanyakazi kukabiliana na hali ngumu ya kimaisha, ingawa hakuna uzalishaji ambao unaendelea katika migodi yake.

"Tutaendelea kulipa kila tunapopata uwezo kutoka katika vyanzo vingine na tunajua wafanyakazi wetu wanadai," alikiri.



Mjasiriamali Pamela Mollel akiuza uji unaojulikana kwa jina la 'Pam porridge' katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha juzi.
**PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Madiwani waililia Tarura ubovu wa barabara zao

**Na Jaliwason Jasson,** HANANG

MADIWANI wa Halmashauri ya Hanang' mkoani Manyara, wameutaka Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (Tarura), kuwajengea madaraja na barabara, ili kuimarisha mawasiliano katika maeneo mengi ambayo yamekosa huduma hiyo.

Wawakilishi hao wa wananchi walieleza kilio chao hicho wakati wa kikao maalum cha Baraza la Madiwani katika halmashauri hiyo, kilichojadili mapendekezo ya mapato na matumizi ya mwaka ujao wa fedha.

Katika kikao hicho, madiwani wengi waliomba kujengwa kwa barabara zao na madaraja, baada ya Meneja wa Tarura wa Wilaya hiyo kusoma taarifa yake juu ya mapendekezo ya matumizi ya mwaka ujao wa fedha.

Diwani wa Gisambala, Yohana Hange, aliomba Tarura ijenge daraja la Changanyikeni, akieleza kuwa lililokuwapo, limekatika.

"Tunaomba mtujengee daraja pale Changanyikeni, maana tunaendelea kuwazika ndugu zetu na jana tumetoka kumzika mwenzetu kutokana na eneo hilo kukosa daraja na maji yanasomba watu kila mara," alilalamika.

Alisema kati ya madaraja 150 ambayo Tarura wamepanga kujenga mwaka ujao wa fedha, wanaomba mojawapo liwe la Changanyikeni, ili kuokoa maisha ya wananchi wake.

Diwani wa Endasaki, Hashimu Gamnga, aliwashauri Tarura kwa kuwa na mpango huo, lakini akawataka waangalie maeneo muhimu ya kutoa huduma ndiyo yapewe kipaumbele na siyo kupendelea baadhi ya madiwani.

Akijibu hoja za madiwani hao, Kaimu Meneja wa Tarura Wilaya ya Hanang', Nicolaus Ludigery, alisema katika mapendekezo ya mwaka ujao wa fedha, wilaya hiyo imetenga Sh. milioni 875.03 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida na maeneo korofi.

Alisema barabara zilizotajwa ni nyingi lakini fedha zilizotengwa ni kidogo, hivyo akaahidi kadri watakavyoendelea kutengewa fedha, watengeneza barabara hizo.

Meneja huyo pia alisema kuna barabara zinazochongwa na wananchi na hazina sifa kwa kuwa ni nyembamba na baadhi ni uchochoro, hivyo Tarura haitazitengeneza.

## Wafugaji ng'ombe wapewa neno

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

DAKTARI Bingwa wa Mifugo Wilaya ya Longido mkoani Arusha, Safan Kagome, amewataka wafugaji wa ng'ombe kuchanja mifugo yao, ili kuwakinga dhidi ya ugonjwa wa vipele unaosumbua kwa sasa baada ya kutoweka mwaka 2015.

"Kila ng'ombe chanjo itatolewa kwa Sh. 400 tu, hivyo kila mmoja ni vyema akapeleka ng'ombe wake ili aepukane na ugonjwa huo," alishauri.

Dk. Kagome alikuwa anazungumza na wenyeviti na watendaji wa vijiji vya wilaya hiyo kwenye Ukumbi wa Halmashauri, akibainisha kuwa chanjo hiyo inaanza kutolewa Januari leo.

Alisema awali walikubaliana tarehe hiyo, ila baadhi ya maeneo wilayani hapo yaliomba kutolewa kabla ya tarehe tajwa, hivyo Kijiji cha Tingatinga kilichoko Tarafa ya Enduiment, chanjo hiyo ilitolewa Januari 9 mwaka huu.

Dk. Kagome alisema wilaya hiyo inakadiriwa kuwa na ng'ombe zaidi ya 200,000 na kuwaagiza wafugaji hao, kuhakikisha mifugo hiyo inapata chanjo.

"Sheria ya Mifugo inasema kila mfugaji lazima achanje mifugo yake na asiyechanja, lazima ashtakiwe mahakamani, adhabu yake ni faini kuanzia Sh. 300,000 au 500,000 au kifungo cha mwaka mmoja jela. Hata ikiwezekana adhabu zote kwa pamoja," alionya.

Pia aliwataka viongozi hao kufufua majosho yaliyoko katika maeneo yao, kwa kuwa serikali imetoa dawa aina ya Parinet lita 136 kwa ajili ya kuogesha mifugo ili kudhibiti kupe.

Alifafanua kuwa pamoja na serikali kutoa dawa hiyo, masharti ya kupewa dawa ni kuhakikisha majosho yanafanya kazi na kuna upatikanaji wa maji ya kutosha kwenye majosho na kuanzisha kamati za kuyasimamia.

"Mkikamilisha hayo, tukaja kukagua tukahakiki kuwa mmetimiza vigezo, tunawapatia dawa. Hadi sasa, maosho la Matiani na Eworendeke ndiyo yanafanya kazi, mengine bado," alibainisha.

Alisema kuwapo kwa wadau wa maendeleo wilayani hapa, kumewezesha kukarabatiwa kwa majosho saba kupitia mradi wa Maisha Bora, lakini hadi sasa ni majosho mawili tu ndiyo yanafanya kazi licha ya kukarabatiwa na haelewi tatizo linalokwamisha maeneo mengine.

Aliwataka wafugaji kusimamia mifugo yao kwa umakini na kutoachia mifugo kuzurura kwenye mazingira ya barabara, ili kuepuka kugongwa na hata wakati mwingine kuonekana kero kwenye maeneo ya makazi ya watu ambao hawafugi.

"Punda wameonekana kuzagaa sana Barabara ya Engikaret hadi Namanga, unakutana na kundi lenye punda zaidi ya 200, hawana msimamizi, niombe walindeni na kuwatunza wasionekane kero kwa jamii," aliagiza.

Mfugaji kutoka Kijiji cha Irikaswa Saruni Lukumay alisema, ugonjwa wa vipele umeonekana pia kwa mifugo mingine, hasa mbuzi na kondoo, hivyo akaiomba serikali kutoa chanjo kwa mifugo hiyo pia.





# Sheikh aona tatizo viongozi wenzake

**Na Mary Mosha,** SIHA

KAIMU Shekh wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mlewa Shabani, amewataka viongozi wa kiislamu kuacha migogoro ya kuwatenganisha waumini wa dini hiyo. Badala yake kiongozi huyo wa kiroho amewashauri kujitathmini namna walivyoweza kujikita katika kuitetea amani ya Watanzani, na namna walivyoweza kuleta mabadiliko ya kimaendeleo.

Hayo yalisemwa jana wakati wa mashindano ya Qur'an sambamba na kuliombea dua taifa iliyofanyika katika Msikiti wa Ngarenairobi wilayani humo huku akiwataka viongozi hao kutambua wajibu wao na kuacha migogoro ya mara kwa mara. "Viongozi mjitathmini kama kweli mnatimiza wajibu wenu, kwani kwa sasa kuna migogoro mikubwa inayoibuka katika taasisi za kiislamu na misikiti, lakini mingi inachangiwa na viongozi wake kwa ajili ya maslahi yao binafsi," alisema na kuongeza:

"Tunapaswa kuliombea Taifa, katika kuwaasa watoto wetu na vijana kujikita katika kufanya kazi na kumtumikia Mungu, hii inaweza kusaidia kumaliza kabisa matatizo mbalimbali ikiwemo rushwa."

Naye Katibu wa baraza hilo, Awadhi Lema, aliwataka waumini hao na Watanzania kwa ujumla kuendelea kuliombea Taifa amani na kupendana huku wakifanya kazi kwa bidii ili kujikwamua kiuchumi.

Lema alisema taifa likiwa na amani na utulivu bila ya kuwa na chembe chembe ya mifarakano litasonga kwa misingi ya haki na kukuza uchumi. "Taifa lenye amani, wafanyabiashara wanaweza kufanya biashara, wawekezaji kuwekeza, wafugaji kufuga, viongozi wa kiisilamu tunaongoza kila kona katika kuwa na migogoro yetu binafsi na kuwafanya waamini kukusa imani na sisi, tuache na badala yake tuwaongoze katika misingi ya kuliombea taifa na kujinyanyua kiuchumi," alisema.

Mmoja wa waumini, Athumani Ngulum kutoka Tarili, aliwataka viongozi hao kuacha mara moja migogoro huku wakiwaomba viongozi wa mkoa kuwachukulia hatua wote watakaobainika kuendeleza migogoro.

# Wafanyabiashara walalama kutimuliwa eneo walilolipia

**Na Mary Mosha,** MOSHI

BAADHI ya wafanyabiashara pembezoni mwa kituo cha treni cha Moshi, wameulalamikia uongozi wa kituo hicho kuwaondoa wasiendelee na biashara zao licha ya kuwa wanalilipia kihalali.

Baadhi ya wafanyabiashara hao walisema kuwa uongozi wa kituo hicho umewataka kuondoka eneo hilo bila maelezo yoyote, jambo linalohatarisha ustawi wa biashara zao.

"Tunasikitishwa na uongozi huo sisi tumepewa maeneo haya kihalali na tunafanya kazi hapa kwa muda mrefu, ila cha kushangaza barua Desemba 27, mwaka jana tumepewa barua ya kuondoka ifikapo Agosti Mosi, mwaka huu," alisema Geraid Gabriel.

"Huu ni uonevu kwa kuwa tumewekeza mikopo na muda wanaotutaka kuhama ni mdogo, lakini pia wangetushirikisha kama wanataka kufanya maboresho au nini ili na sisi tuombe muda wa kutafuta maeneo mengine," alisema Mwita Said.

Alisema ikiwa shirika limeazimia kufanya marekebisho ni vyema wafanyabiashara hao wakaongezewa muda, ili waweze kuondoa vibanda vyao.

Mwanahawa Mzava, aliliomba shirika hilo kufuta agizo la Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa, katika uzinduzi wa gari Moshi hilo lililowataka wafanyabiashara kutumia fursa hizo.

"Waziri Mkuu Majaliwa alitutaka kutumia fursa za uwapo wa gari Moshi hili katika kufungua biashara na kuwekeza ... inasikitisha kuona leo mnakiuka agizo hilo na kutaka kubomoa vibanda vyetu bila hata kutushirikisha," alisema Mwanahawa.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, ambaye alisema wamelazimika kuwaondoa wafanyabiashara hao ili kufanya ukarabati wa kituo ambacho ni chakavu kwa sasa.

"Sisi hatujawafukuza bali tunataka kufanya marekebisho na kisha kuwarudisha kwa utaratibu... tusieleweke kuwa tumewafukuza, tunatengeneza mazingira rafiki kwa wateja na wao wenyewe.



Diwani wa Nasai (CCM), Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, Solomon Mmari, akizungumzia na wakazi wa kata hiyo, jana, kuhusu kukithiri kwa matukio ya ukatili wa watoto na hatua zinazochukuliwa na wadau wa maendeleo. **PICHA: GODFREY MUSH**

# RC apata dawa migogoro ya wakulima na wafugaji

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amewataka wananchi wa vijiji vya Mtakuja na Mserikia katika Wilaya ya Moshi kupunguza idadi ya mifugo kwa kuuza ikiwa ni njia mojawapo ya kukabiliana na migogoro ya kugombea maeneo ya malisho kati ya wafugaji na wakulima hasa nyakati za ukame.

Dk. Mghwira alitoa agizo hilo juzi, wakati akizungumza na wananchi wa vijiji juu ya njia bora za kumaliza migogoro kati ya makundi hayo mawili.

Alisema kuna haja ya jamii hiyo kuanza kufuga kisasa na kupunguza idadi ya makundi makubwa ya mifugo ambayo yamekuwa yakiharibu mashamba ya wakulima na kusababisha migogoro ya mara kwa mara.

"Viongozi wa vijiji hivi viwili, nataka muandae mpango mkakati wa kuisaidia jamii ya wafugaji kuwa na shughuli mbadala za kuwaingiza kipato, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanawaelimisha wafugaji namna bora ya kupunguza mifugo yao katika kuhakikisha wanauza na kujipatia kipato," alisema na kuongeza;

"Naagiza na ninyi wafugaji fikirieni kupunguza sehemu ya mifugo yenu na kubakisha idadi ndogo ya mifugo kwa sababu ongezeko la watu limesababisha ardhi kuwa finyu na haitoshi kwa malisho na kilimo."

Baadhi ya jamii ya wafugaji katika eneo la Mserikia, Lomayani Alaisi, alisema hawana tatizo na agizo hilo kwa kuwa wanafahamu linalenga kuwahimiza kufugaji kisasa na kuepukana na migogoro isiyo ya lazima.

"Mimi binafsi sina tatizo na nitatii agizo la serikali nitaanza kufuga mifugo ya kisasa, naijua adha kubwa ninayoipata kipindi cha kiangazi tunapohama na makundi ya mifugo kwa ajili ya kuitafuta malisho katika mikoa ya jirani. Kazi kubwa iko kwa wenzangu kukubaliana na jambo hili ambalo kwao ni gumu," alisema Lomayani.

Awali, Diwani wa Kata ya Mabogini (Chadema), Emmanuel Mzava, akizungumza mbele ya mkuu huyo wa mkoa alisema kwa sasa wameanza utaratibu wa kutenga maeneo ambayo hayajaendelezwa kwa ajili ya malisho.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Baraza la Maendeleo ya Kata (Wadc) lilikaa na kupitisha azimio la kuunda kamati za kudhibiti makundi ya mifugo yanayotoka mbali na kuingizwa kwenye mashamba ya wakulima, kamati hiyo ipo na imeshaanza kazi.

Pia tumetenga maeneo kwa ajili ya malisho hivyo tunaamini migogoro hii itafikia mwisho," alisema Mzava.

Ukurasa 17



**Uturuki, Russia zaua vita za Libya na Syria**

**MZIZI WA SERIKALI...**
Unakijua kijiji? Hivi ndivyo kinavyojipanga, kufanya kazi



Ukurasa 15

**Kimataifa**



**Fumbo linalowatesa Waingereza mwanamfalme kuhamia uraiani**

Ukurasa 18

siasa
JUMATANO JANUARI 15, 2020
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe



**Visasi vinavyotawala tangu siku kuangushwa Boeing ya Ukraine**

Ukurasa 16

## OLE WENU NDUGU!

# Mangula na marufuku yenye mwangwi kitaifa

• Rushwa, kujipitisha CCM?

**Na Sabato Kasika**

WAKATI nchi ikielekea kwenye uchaguzi mkuu, ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), kuna madai ya makada wa chama hicho wanaojipitisha kwa wapigakura, kinyume na utaratibu wa chama na sheria za nchi.

Aidha, kuna wanaodaiwa 'kufanya rafu.' Sasa wameonywa kwamba, watachukuliwa hatua za kinidhamu na kutakiwa kuacha mara moja mchezo huo, kwa vile ni kinyume na kalenda ya chama.

Kwa wale wanaofuatilia siasa kitaifa, watakuwa wameshamsikia Makamu Mwenyekiti wa CCM -Tanzania Bara, Philip Mangula, ambaye kila mara anarudia onyo hilo kwa makada wanaoonekana kujipenyeza.

Mtu anapofuatilia kwa karibu kauli zake, zinabeba ujumbe mwangwi wa kile alichotamka wakati anakabidhiwa wadhifa wa sasa na anachoendelea kutamka 'huku na kule.'

Inajulikana kuwa ni kawaida kwa mwanasiasa anayewania nafasi fulani katika mchakato wa kura za maoni ndani ya chama chake na hatimaye kupewa nafasi ya kukiwakilisha chama, dhidi ya wagombea wa vyama vingine, kama watakuwapo.

Mangula, aliyewahi kuwa mtendaji mkuu wa CCM hivyo anaijua vyema, ametoa onyo na kuahidi kuwachukulia hatua kali za kimaadili kupitia kamati za ngazi tofauti za siasa ndani ya chama, wanasiasa wote wanaoanza kujipitisha katika dodosa za kisiasa.

Hapo wanajisogeza kwa wananchi na kutangaza nia ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kinyemela, jambo ambalo ni kinyume na kalenda kuu ya CCM.

Endelea 14



Philip Mangula.

**BURIANI QABOOS AL SAID** Ukurasa 19

Inatoka Uk. 13

**ONYO SINGIDA**
Alipokuwa mkoani Singida, Mangula aliwaonya wanaCCM wanaoanza kujipenyeza majimboni, kuwania nafasi za ubunge na udiwani, ilhali nafasi hizo bado zina wawakilishi.

Ni onyo la Julai mwaka jana, alipozungumza na wana CCM wilayani Ikungi, mkoani Singida, katika mkutano wa kuwapongeza wana – CCM, Jimbo la Singida Mashariki, kwa ushindi aliyoupata mgombea ubunge, Miraji Mtaturu, aliyetumia tiketi ya chama kwenye uchaguzi mdogo.

"Natoa maelekezo kuwa mtu yeyote atakayebainika kuanza kujipenyeza katika majimbo kwa nia ya kufanya kampeni ya kuwania nafasi hizo za uongozi, hatutamwonea huruma. Tunamchukulia hatua kali za kinidhamu," anasema.

Mangula anaendelea kuwa majimbo hadi sasa yana wawakilishi, ambao muda wao wa miaka mitano haijaisha, hivyo waachwe watekeleze ilani ya chama hicho inayoelekeza azma ya kuwapelekea wananchi maendeleo.

Anatamka kwamba, mwana - CCM mwenye nia ya kushika nafasi hizo, anatakiwa kuwa na subira muda sahihi ufike. Wanachotakiwa kukifanya sasa, ni kwenda kwa wananchi kutangaza maendeleo yaliyofanywa na viongozi waliopo, daima si kuwania majimbo.

Mkimuona mtu yeyote ameanza kujipenyeza katika majimbo mtoe taarifa, ili achukuliwe hatua kali kupitia kamati ya maadili," anasema Mangula.

**ALIPOTUA SIMIYU**
Mnamo Desemba mwaka jana, Mangula akiwa kwa mara myingine alirejea marufuku mkoani Simiyu kwa viongozi wa chama hicho wanaotoa siri za vikao vya chama, akiwakumbusha kufanya hivyo ni kukiuka maadili.

Hapo alikuwa akizungumza katika Mkutano wa Halmashauri ya CCM ya Wilaya na Mkoa na watendaji wa serikali wa halmashauri sita za wilaya za mkoa wa Simiyu.

Mangula anasema, viongozi wanaotoa siri za vikao hawafai kuongoza chama na wanapobainika ni wa kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

"Kumekuwa na tabia chafu kwa baadhi ya viongozi ndani ya chama chetu ambao wanatoa siri za ndani za vikao... na kama hamjui kufanya hivyo ni kukiuka kanuni za chama na kama kuna viongozi watakaobainika kufanya hivyo, wachukuliwe hatua za nidhamu," anasema.

Mangula anaendeleza onya dhidi ya viongozi wa CCM wanaotumia madaraka yao kubughudhi watendaji wa serikali, ingawa katika sura ya pili ya shilingi anapongeza mkoa wa Simiyu kwa ujenzi shule bora na zahanati.

OLE WENU NDUGU!

# Mangula na marufuku yenye mwangwi kitaifa



Philip Mangula, katika vikao vya chama. **PICHA: MTANDAO.**

**NYUMBANI WANGING'OMBE**
Huku ni kwao kwa asili, mkoani Njombe. Mangula alipokuwa katika kikao cha Halmashauri Kuu ya Chama Wilaya ya Wanging'ombe mwezi huu, kwa mara ya tatu akatoa onyo kwa wale wanaothubutu kujipitisha kwa wananchi kutangaza nia ya kuwania nafasi mbalimbali.

Makamu Mwenyekiti huyo, anaahidi kuwachukulia hatua kali za kimaadili kupitia kamati za ngazi tofauti za siasa ndani ya chama, dhidi ya wanasiasa wanaoana kupita kwa wananchi kutangaza nia ya kugombea nafasi mbalimbali, jambo ambalo ni kinyume na kalenda ya CCM.

Hapo analifafanua kwa kauli kwamba "kunakiuka misingi na maadili ya chama na kuathiri utendaji wa viongozi waliopo madarakani."

Msimamo aliowapa wanaCCM wenzake ni kwamba, ni kupiga marufuku kutoa zawadi au msaada wa aina yeyote bila mawasiliano na mwakilishi wa jimbo au kata.

Kwa maonyo hayo na mengine mengi, ni wazi kwamba amedhamiria kuhakikisha mchakato wa kupata makada wa kuwakilisha chama wanapatikana kwa njia halali.

MSIMAMO WAKE
Kwa wanaomjua, huyo ni kada mkongwe, aliyepikwa tangu zama hizo akiwa katika Umoja wa Vijana wa Tanu (UVT) akiwa na msimamo unaojulikana, hata zama alipokuwa, Katibu Mkuu wa CCM kwamba 'makandokando' yakiwamo ya rushwa na yeye wako mbalimbali.

> "Kumekuwa na tabia chafu kwa baadhi ya viongozi ndani ya chama chetu ambao wanatoa siri za ndani za vikao... na kama hamjui kufanya hivyo ni kukiuka kanuni za chama na kama kuna viongozi watakaobainika kufanya hivyo, wachukuliwe hatua za nidhamu," anasema.

Mara alipochaguliwa kuwa Makamu wa Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara mwaka 2012, aliahidi kupitia tamko "hakuna mla rushwa ndani ya chama atakayepona."

"Namshukuru (Rais Jakaya) Kikwete, kwa imani aliyoonyesha kwangu hadi akaniteua kugombea nafasi hii. Sitamwangusha, nitamwonyesha kuwa hata wakulima wa nyanya wanaweza," anashukuru.

Aliteuliwa kuwania nafasi hiyo, baada ya kukaa nje ya uongozi kwa miaka mingi tangu alipostaafu nafasi ya Katibu Mkuu wa CCM, akisema baada ya hapo alijikita katika uzalishaji nyanya katika kipindi hicho chote.

Akiwa jijini Dar es Salaam, baada ya kuchaguliwa alitoa miezi sita kukisafisha chama hicho kwa kuwafuta wote waliotajwa kuhusika na rushwa katika chaguzi za ndani ya chama hicho.

"Natoa miezi sita walioingia kihalali wataendelea na wale walioingia kwa rushwa nje... hata wale vibaraka waliokuwa wanatumwa vibahasha nao nje. Wote tutasafisha chama chetu, hatutakubali CCM ituhumiwe kwa rushwa popote," anasema.

Katika uchaguzi wa CCM ngazi mbalimbali zilizowahi kulalamikiwa kwa rushwa, ni zinazohusu jumuiya za chama hicho; Umoja wa Wanawake (UWT), Umoja wa Vijana (UVCCM) na Jumuiya ya Wazazi.

> "Natoa miezi sita walioingia kihalali wataendelea na wale walioingia kwa rushwa nje... hata wale vibaraka waliokuwa wanatumwa vibahasha nao nje. Wote tutasafisha chama chetu, hatutakubali CCM ituhumiwe kwa rushwa popote," anasema.

MZIZI WA SERIKALI...

# Unakijua kijiji? Hivi ndivyo kinavyojipanga, kufanya kazi

Na Mwandishi Wetu

UNAPOZUNGUMZIA msamiati kijiji, si mgeni kwa jamii. Mara moja kuna dhana ya kwanza inayojengeka, eneo lenye makazi ya pamoja ya watu, katika eneo lisilo mjini.

Katika zama za utekelezaji wa siasa za kijamaa, katika zama hasa kati ya mwaka 1964 na 1985, ilitumika sana kutekeleza uchumi kupitia itikadi za siasa hizo. Hapo ndipo kulizaliwa vijiji vya ujamaa na vijiji vya kawaida.

Kijiji kwa muundo na utekelezaji ndio unaunda serikali, ikiwa ndiko kwenye msingi mkuu wa serikali ya mtaa.

Mwaka 1975, panakumbukwa nchi kuwepo operesheni vijiji kitaifa, ambavyo katika sehemu nyingi watu walihamishwa makazi kuishi katika maeneo ambako serikali iliona ni bora kuwaletea maendeleo ya pamoja.

Makazi mapya yalianzishwa wakati huo, ikiwemo hata Jiji la Dar es Salaam, maeneo ya pembezoni kama Tegeta (Wilaya Kinondoni), Kubugumo na Mwanadilatu, ambako sasa ni jiji, kulikuwa vijiji vipya

**MUUNDO WAKE**

Kijijini ndiko kwenye maisha ya umma, wananchi wanashiriki katika serikali za mitaa au mikutano mbalimbali kujadili na kutoa mapendekezo kuhusu mipango na matatizo yanayowakabili kurahisisha uboreshaji huduma za kijamii wanakoishi.

Huko ndiko asilimia kubwa ya wananchi wanapatikana, wengi wadau pacha wa uchumi; kilimo, ufugaji uvuvi.

Katika majukumu yao, mkutano wa kijiji ni chombo kikuu cha utawala na kipo kisheria. Wajumbe wake ni wanakijiji waliofikia umri usiopungua miaka 18 na hakuna akidi maalum ya kikao, ingawa kila kijiji hujiwekea, mathalani asilimia 20 ya wajumbe.

Kwa kawaida mkutano hufanyika kila baada ya miezi mitatu na kikao cha dharura kinaweza kuitishwa kukiwapo haja na kufanya hivyo. Taarifa ya kuitishwa Mkutano Mkuu wa Kijiji hutolewa si chini ya siku saba.

Pia, kila baada ya miaka mitano, kunakuwapo na mkutano mkuu maalum wa, uakindaa mchakato kwa wanakijiji kugombea nafasi za uongozi kwenye halmashauri ya kijiji au uenyekiti wa kijiji na nafasi nyingine kijijini.

Katika kuandaa mkutano, Mwenyekiti na Ofisa Mtendaji wa Kijiji (VEO) hupanga ratiba za vikao na kuitisha vikao vya Mkutano Mkuu wa Kijiji.

**MADARAKA MKUTANO**

- Kusimamia na kuwajibisha watendaji.
- Kuweka taratibu za kuitisha vikao vya dharura.
- Kupitia mkutano mkuu maalum wa uchaguzi. Kuchagua mwenyekiti wa kijiji na wajumbe halmashauri ya kijiji.
- Kujaza nafasi wazi za viongozi wa halmashauri ya kijiji.
- Kujadili na kupokea au kukataa taarifa za utekelezaji wa shughuli za kijiji kutoka halmashauri ya kijiji.
- Kupokea, kujadili na kupitisha au kukataa taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za kijiji.



Baadhi ya wana kikundi cha Ujamaa, wakishirikiana kupanda mbegu bora, baada ya uzinduzi rasmi wa shamba darasa, kutokana na kufunzwa na mtaalamu wa mazao ya mizizi kutoka Kituo cha Utafiti wa Kilimo Maruku, Bukoba , Jojianas Kibula (hayupo pichani).

- Kupokea, kujadili na kupitisha au kukataa mapendekezo ya kodi, ushuru na vyanzo vingine vya mapato ya kijiji.
- Kupokea na kujadili taarifa ya makusanyo ya fedha za kodi, ushuru na mapato mengine kijijini.
- Kupokea, kujadili na kufanyia uamuzi mapendekezo ya serikali ya kijiji kutunga sheria ndogo.
- Kupokea, kujadili na kufanyia uamuzi ugawaji wa ardhi na matumizi ya rasilimali za kijiji.
- Kuhoji, kudadisi, kukosoa, kukubali au kukataa taarifa na mapendekezo ya serikali ya kijiji.
- Kuondoa madaraka serikali ya kijiji au mjumbe yeyote kabla ya muda wao.
- Kupitisha azimio la kukaripia rasmi mjumbe yoyote wa halmashauri au halmashauri kwa ujumla kwa utendaji mbovu.

**HALMASHAURI KIJIJI**

Halmashauri ni chombo kikuu cha utendaji katika utawala wa kijiji. Hukutana mara moja kila mwezi na mikutano ya dharura inaweza kuitishwa, akidi yake ni nusu ya wajumbe wote kijijini.

Wakati Mkutano Mkuu ni kama Bunge, Halmshauri ya Kijiji ni kama serikali. Wajumbe wake huchaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji, wakisimamiwa na mkurugenzi wa halmshauri ya wilaya

Ni mkutano mkuu, ambao kwa kushirikiana na mamlaka za kusimamia uchaguzi, hupendekeza idadi ya wajumbe wanaowafaa, kutegemea na wingi na ukubwa wa eneo lao (idadi ya vitongoji).

Humo kuna wajumbe kama mwenyekiti kijij, na wenyeviti kitongoji, viti vya wanawake wateule, halmashauri ikiongozwa na mwenyekiti wa kijiji, wanaochaguliwa na wakazi wa vitongoji husika

Katika majukumu yake, ndio injini ya kutafakari uamuzi, mapendekezo na maazimio ya mkutano mkuu wa kijiji na kubuni mbinu na njia za utekelezaji.

Ikiwa wajumbe wa halmashauri hawaridhiki na utendaji wa mwenyekiti wa kijiji, wana nguvu za kuendesha mchakato wakumuondoa na kuitisha mkutano mkuu wa kijiji, kuchagua mwingine.

Aidha, ndicho kikao kinachopekea taarifa za mikutano ya vitongoji na kamati zake, kufanyia kazi na kupeleka kwenye mkutano mkuu wa kijiji.

Lingine, ni upokea, kutafakari na kufanyia kazi maagizo na mapendekezo kutoka kamati ya maendeleo ya kata (WDC) na halmshari ya wilaya.

Halmashauri inabuni na kuendeleza sera na mwelekeo wa kijiji kwa mkutano mkuu wa kijiji, huku ikiandaa na kupendekeza mipango ya maendeleo ya muda mrefu kwa mkutano mkuu wa kijiji.

Pia inaweza kutunga sheria ndogo kwa kushauriana na mkutano mkuu wa kijiji, ikawaalika wataalamu panapokuwa na haja ya kufanya hivyo (ila hawatakuwa na haki ya kupiga kura).

Halmashauri ya Kijiji, inapokea, kutafakari na kupendekeza kwa mkutano mkuu wa kijiji, maombi ya ugawaji wa ardhi kubwa na ndogo, kumiliki mali na kuingia mikataba kwa niaba ya kijiji.

- **Kwa mujibu wa marejeo ya kitaalamu kuhusu muundo huo**




Ndivyo kijiji kilivyo. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

SIASA

**Na Anil Kija**

# Visasi vinavyotawala tangu siku kuangushwa Boeing ya Ukraine

## • Marekani vs Iran ‘kavu kavu’

UTAWALA wa Iran ukijua kuwa Rais Donald Trump wa Marekani ana matatizo makubwa kumezesha sera ya kuingia vitani na Iran, endapo ushindani Mashariki ya Kati na mashambulizi yataendelea, imepiga hatua nyingine katika shari inayojengeka eneo hilo.

Baada ya kutupa makombora ambayo hayakuwa na madhara kwa askari wa Marekani katika kambi mbili nchini Iraq, imeangusha ndege ya abiria mali ya nchi ya Ukraine, rafiki wa Marekani, iliyotengenezwa na kampuni ya Boeing ya Marekani.

Kwanza Iran ilisema kulikuwa na hitilafu ya kiufundi katika ndege, taarifa na video zikaonyesha shambulio, ikanywea.

Baada ya muda ikabadili mkondo wa maelezo, kudai kupitia Rais Hassan Rouhani kuwa: “Jeshi la Iran limefanya uchunguzi na kugundua kuna kombora lilirushwa kwa makosa na kuiangusha ndege hiyo.”

Rais huyo anadai kwa sasa uchunguzi unafanyika waliohusika waadhibiwe kwa kosa hilo lisilokubalika, lakini wachunguzi wa habari duniani kote, wanasema hapakuwapo tofauti na utawala wa Saudia kuchunguza mauaji ya mwanahabari, Jamal Khashoggi, katika ubalozi wake mdogo jijini Istanbul, Uturuki.

Ni ‘kesi ya ngiri anapelekewa nguruwe.’ Bado Marekani, ilikuwa inaangalia ushahidi uliopo, ila ikatanguliza vibano zaidi kuhusu mashambulizi ya awali.

Watu 175 waliokuwapo katika ndege hiyo waliuawa, ambako sehemu kubwa kiasi walikuwa raia wa Canada, waliofika 67 na labda ndiyo eneo la vilio kuhusiana na tukio hilo lilionyeshwa zaidi vyombo vya habari.

Ni Waziri Mkuu wa Canada Pierre Trudeau, aliyeondoa pazia la ajali kwa kutoa taarifa katika mkutano na waandishi wa habari kuwa ‘intelijensia’ ya Canada na vyanzo vingine vinaonyesha kuwa ndege hiyo iliangushwa, jambo ambalo halikuwa gumu wa watazamaji wa televisheni kukisia.

Ndege ilianguka kwa hitilafu inafika chini nzima, halafu labda ilipuke, lakini hii ilitawanyika tu.

Hitilafu nyingine ya dhamira ya Iran ilikuwa katika kuwezesha uchunguzi na kuacha mabaki ya ndege kwa muda unaotakiwa hadi kiongozi rasmi wa uchunguzi, hasa kutoka nchi husika na hata kampuni ya watengenezaji ndege waridhike kuwa hawahitaji tena kubaki kwenye eneo la tukio.

**TAARIFA INTELIJENSIA**

Mhusika wa siku nyingi wa Idara ya Usalama wa Safari za Anga nchini Marekani alisema katika televisheni ya CNN kuwa, kwa kawaida inahitaji saa 72 au zaidi kuanzia tukio litokee hadi wachunguzi wakamilishe majukumu yao eneo la tukio, lakini Iran ilianza kuondoa mabaki ya ndege mapema tu.

Alisema katika kazi ya uchunguzi wa mikasa ya ajali za ndege, kuna chembe ya diplomasia, lakini wachunguzi wa nchi mbalimbali kabisa wasingeweza kwenda Iran kuisaidia tu kufunika kilichotokea, kama inavyonuia.

Baada ya Waziri Mkuu Trudeau kuongea na waandishi wa habari, jijini Washington, Marekani ukawepo mkutano na waandishi wa habari uliofanywa na Waziri wa Mambo ya Nje Mike Pompeo na Waziri wa Fedha Steven Mnuchin.

Walikuwa wakielezea vikwazo vipya dhidi ya Iran kutokana na kushambulia kambi mbili za kijeshi za Marekani nchini Iraq, ambako Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Mohamed Javad Zarif, Marekani imemzuia visa kuhudhuria kikao cha Umoja wa Mataifa, jijini New York.

Alisema kuwa Iran imemaliza kujibu mapigo baada ya shambulio la Marekani dhidi ya Jenerali Qassem Soleimani, akimaanisha Marekani isijibu shambulio hilo. Kumbe kuna kete alikuwa ameificha.

Katika maelezo yake kwa wanahabari, Waziri Pompeo alisema endapo itathibitika ndege hiyo iliangushwa na Iran, basi Marekani na dunia kwa jumla watachukua hatua zinazopasa.

Ina maana ukuaji wa mgogoro kati ya nchi hizo mbili bado unaendelea na siyo ajabu ukue kwa kasi, kuelekea vita na taarifa ya Jeshi la Iran ndiyo ilishangaza zaidi katika maelezo yake, ikionyesha ndege hiyo ilipigwa kwa makusudi.

Dai lililopo ni paligeuka eneo nyeti la ‘Walinzi wa mapinduzi ya Iran’ (Revolutionary Guards) na hivyo ikadhaniwa huenda ni kombora la Marekani liitwalo ‘cruise missile.’

Sasa inaleta mshangao, ndege ya abiria yenye watu 167 inafananishwa na kombora katika kiwewe ambacho amri inatolewa kuwa kombora lirushwe kuizuia, wakati kombora na ndege ya abiria ni vitu tofauti sana.

Alichokisema Rouhani, ni kama kuna mtu alijifyatulia tu hilo kombora, na si wasiwasi halisi kuhusu ndege na ndio maana kuna chembe ya kuchezea akili za Wamarekani ambao kwa wingi hawataki sera za Trump kuhusu Iran.

Katika hilo wanajitahidi kila wawezavyo kujibu maelezo ya watendaji wa Trump kama Pompeo, kwa mfano katika mkutano wake na waandishi wa habari, alibanwa atoe maelezo ‘intelijensia’ iliyoonyesha Jenerali Soleimani alikuwa na mpango kushambulia balozi za Marekani.

Ni hoja yenye maana, shambulio dhidi ya ubalozi wa Marekani hadi kuvunja milango, halikuwa sababu ya kutosha kumpiga kamanda huyo wa vikosi maalum vinavyopigana kote Iraq, Lebanon na Syria.

Wakati huo huo, mbunge mwenye vituko vingi mpinzani mkubwa wa Israel aliyezaliwa Somalia na kuhamia Marekani na wazazi wake akiwa na umri wa miaka minne, Ihlan Omar, mvaa hijabu muda wote, alisema kuwekewa vikwazo Iran ni ‘vita vya kiuchumi.’

Yuko mwanaharakati mwingine aliyeandika katika gazeti la ‘mrengo wa kushoto’nchini Israel, Haaretz, akisema Rais Trump akiingia vitani na Iran ndiyo utakuwa mwisho wa urais wake, kwani hatapita katika uchaguzi mkuu baadaye mwaka huu.

Ni makundi ya wanasiasa na wanahabari kama hayo ambayo yatatenda mapenzi ya Iran, kuiaminisha Marekani nje ya kila ushahidi uliopo, kuwa ndege hiyo iliangushwa kwa makosa na kuwa Marekani isichukue hatue, iache mambo yapoe. Ila haitazamiwi kuwa ndiyo mwelekeo wa Trump.



Namna uchunguzi wa ndege ya Ukraine iliyolipuliwa hivi karibuni, ulivyokuwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



“Baada ya muda ikabadili mkondo wa maelezo, kudai kupitia Rais Hassan Rouhani kuwa: “Jeshi la Iran limefanya uchunguzi na kugundua kuna kombora lilirushwa kwa makosa na kuiangusha ndege hiyo.”

“Wakati huo huo, mbunge mwenye vituko vingi mpinzani mkubwa wa Israel aliyezaliwa Somalia na kuhamia Marekani na wazazi wake akiwa na umri wa miaka minne, Ihlan Omar, mvaa hijabu muda wote, alisema kuwekewa vikwazo Iran ni ‘vita vya kiuchumi.’



Rais Tayyep Erdogan wa Uturuki na mwenzake wa Russia, Vladimir Putin, mjini Ankara, Uturuki. **PICHA: MTANDAO.**

HISTORIA MPYA

# Uturuki, Russia zaua vita za Libya na Syria

HATIMAYE kuna makubaliano yaliyofikiwa kati ya Rais Tayyep Erdogan wa Uturuki na mwenzake wa Russia, Vladimir Putin mjini Ankara, Jumatano kusutisha mapigano katika nchi za ugenini nchini Libya.

Viongozi hao ambao kila mmoja anaunga upande mwingine, pia walikubaliana kusitisha mapigano nchini Syria na akatoa wito pande zinazogombana kuanza mazungumzo katika nchi zote mbili.

Ilikiwa ni sherehe nchini Libya kusikika wanasherehekea tangazo la kiongozi wa Jeshi la Taifa la Libya, la LNA, Jenerali aliyeasi Khalifa Haftar, kwamba anasitisha mapigano magharibi ya nchi yao, kuanzia Jumapili iliyopita.



Awali, Jenrrali Haftar, alipinga makubaliano hayo ya kusitisha mapigano lakini alibadili msimamo wake Jumamosi.

Msemaji wa LNA, Ahmed Mismari (pichani), alitangaza uamuzi huo kwa masharti kwamba upande wa pili unaheshimu mkataba huo.

Mismari anasema: “Uongozi wa Jeshi la Taifa la Libya, unatangaza usitishaji mashambulizi magharibi ya nchi kuanzia usiku wa manane wa Januari 12, 2020.”

Alitamka kwamba hilo linafanyika kwa sharti kwamba, upande wa pili unatekeleza usitishaji mapigano wakati huo huo na ukiukaji wowote wa makubaliano hayo, yatajibiwa vikali.”

Siku ya Jumapili iliyopita, Rais Erdogan amekuwa na mazungumzo mjini na Fayez al-Sarraj, Waziri Mkuu wa serikali inayoitambuliwa na Umoja wa Mataifa, ambayo anaiunga mkono.

Jeshi linaloongozwa na haftar, lililoanza mashambulizi makali ya kuuteka mji mkuu wa Tripoli Aprili 4, inasaidiwa na Russia, Misri na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Huko Syria nako, usitishaji mapigano unatarajiwa kuanza kutekelezwa Jumapili, ingawa Shirika la Kutetea Haki za Binadamu la Syrian Observatory for Human Rights, linalofuatia vita huko, linaripoti vifo.

Kwa mujibu wa shirika linaripoti kwamba watu 17 waliuawa Jumamosi iliyopita, na wengine 40 walijeruhiwa baada ya Jeshi la Anga Syria kushambulia miji minne katika Jimbo la Kaskazini Magharibi la Idlib.

Haijajulikana bado, ikiwa serikali ya Damuscus inayoungwa mkono na Russia na Iran, itaheshimu makubaliano hayo.

Harakati za kusitisha mapigano Libya na Syria, zimekuwa zikifanyika wiki nzima kati ya nchi za Ulaya na Mashariki ya Kati, ambao viongozi wa mataifa mbalimbali wamekuwa wakikutana na pande zinazozozana katika nchi hizo mbili.

Siku ya Ijumaa iliyoishia, Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel, alitangaza kutakuwapo na mkutano wa amani wa Libya mjini Berlin, Ujerumani hivi karibuni baada ya kukutana na Rais Putin mjini Moscow, Russia.

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, nalo liliidhinisha siku ya Ijumaa kuongeza muda wa kupeleka msaada wa dharura nchini Syria, ikiwa pia kuelekea jimbo la upinzani la Idlib.

Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.

# Fumbo linalowatesa Waingereza mwanamfalme kuhamia uraiani

Na Mwandishi Wetu

- Mama Malkia: Basi tutafanyaje
- Waziri Mkuu: Tuendelee kujadili
- Wenyewe wafurahia kuhamia Canada



Mwanamfalme Harry na mkewe Meghan. **PICHA: MTANDAO**

NDOTO ya mwanamfalme Harry na mkewe Meghan, kutaka kujiondoa katika maisha ya kifalme, imeanza kuleta mwanga mpya baada ya Malkia Elizabeth wa Uingereza, kukubali ombi lao hilo.

Maisha ya wanandoa hayo yatakuwa katika nchi mbili za Canada na Uingereza katika kipindi cha mpito, wakati mchakato wa kujitoa ukiendelea.

Ni jambo lililoleta mshtuko kuanzia kwa ndugu na jamaa zao na hata nje ya jamii yao, hasa ikimaanisha Waingereza likaendana swali 'kuna nini?'

Hata hivyo kuna suala la ulinzi ambalo ni la lazima, nalo linabaki na swali itakuwaje? Kuna hasa kipengele cha ulinzi wao na gharama zake, watakapokuwa katika maisha mapya nchini Canada.

Ni jambo lililobaki tete, kiasi kwamba Waziri Mkuu wa nchi hiyo, Justin Trudeau, ametaka lijadiliwe, huku akiongeza inaenda mbali hata kwenye gharama za ulinzi wao huko ughaibuni utagharimiwaje?

Kupitia kikao kilichofanyika Jumatatu iliyopita, Malkia Elizabeth, amekubali kuwapo kipindi cha mpito wakati mwanamfalme Harry na mkewe Meghan, watakuwa wakiishi Canada na Uingereza.

Pia Malkia Elizabeth anaunga mkono hatua yao kuanza kujitegemea, lakini anashauri kwamba ingekuwa vyema zaidi iwapo wangeendelea kutekeleza majukumu yao ya kifalme kwa muda.

Katika taarifa baada ya mazungumzo yaliyofanyika kwenye makazi ya Malkia Norfolk, Jumatatu iliyopita, ambayo ilihusisha wanamfalme waandamizi, malkia alisema anatarajia kwamba uamuzi wa mwisho utafanyika hivi karibuni.

Hatua hiyo imeibua maswali mengi ndani na nje ya ufalme wakihoji nani atawajibika kuwalinda na vyanzo vya kuwapatia mapato vitakuwa nini?

Trudeau anasema, raia wengi wa Canada wanaunga mkono hatua ya Harry na Meghan kuishi huko, lakini bado majadiliano zaidi yanahitaji kufanyika kuhusu gharama zilizopo.

Anaongeza kwamba hadi sasa serikali ya Canada bado haijahusishwa kuhusu kitakachohitajika katika hatua ya wanandoa kuishi nchini humo.

"Bila shaka tunaunga mkono hatua yao, lakini kuna wajibu wa kufanywa vilevile," anasema Malkia, katika mazungumzo yaliyomhusisha wanamfalme wa Charles na William.

"Japo tungependa wangeendelea kutekeleza majukumu yao ya kifalme kikamilifu, tunaheshimu na kuelewa matakwa yao ya kuishi maisha ya kujitegemea kama familia, wakiendelea kuwa sehemu muhimu ya familia yangu," anasema.

"Tumekubaliana kuwa watakuwa na kipindi cha mpito ambapo wawili hao wataishi Canada na Uingereza baada ya Harry na Meghan kuweka wazi hawataki kutegemea pesa za umma katika maisha yao mapya," anasema Malkia Elizabeth.

Ni mazungumzo ya dharura yaliyopangwa baada ya Harry na Meghan kutoa taarifa iliyoishangaza familia ya kifalme wiki iliyopita, hatua kuzua kizungumkuti.

Hivi karibuni, Harrry na Meghan, waliibua mjadala mkali, baada ya kuzungumzia changamoto za maisha ya kifalme, ikiwamo hofu yao kuandamwa na vyombo vya habari.

Alionyesha wasiwasi wake huenda mkewe akakutana na yale ambayo mama yake Princess Diana alikutana nayo, hata kusababisha kifo chake.

**MALKIA ANAJUTIA**

Pamoja na uamuzi huo kutoka ukoo wa kifalme, Malkia anaonekana dhahiri kujutia hatua ya Harry na Meghan kuwa huru na ndio maana, anataka waendelee kuwa na majukumu yao ya sasa.

Lakini, anajipa moyo kwa kueleza wao bado ni watoto wa kifalme na kwamba wataendelea kuthaminiwa wakati wanaendelea kujitegemea.

Inaonekana, Malkia anachukua hatua hii kama mchakato wa awali na wala siyo jambo la kumalizwa kwa siku moja na ndio maana anazungumza wapo katika kipindi cha mpito, huku suluhu yake haiwezi kupatikana 'kesho' wala miezi michache inayokuja.

Mkutano wa kujadili kujitoa mmoja wa wanamfalme ni wa kwanza kufanyika ndani ya himaya ya ufalme, baadhi ya Waingereza wanaona ni jambo lisilo la kawaida kulisikia.

**MAOMBI YAO**

Watu wengi wanaona mambo ya wanamfalme hao yanatokana na kuzidiwa na maisha ya kisasa, kwani tangazo lao walilitoa kupitia mtandao wa Instagram, jambo ambalo si la kawaida.

Meghan akiwa Canada na mtoto wake wa miezi nane na Archie, walifanya majadiliano hayo wakati wa Krismasi, kabla ya kurejea Uingereza kwa ajili ya majukumu ya kifalme.

**RIPOTI 'PORI'**

Kumekuwapo na ripoti kwamba ndugu hao wawili hawana uhusiano mzuri baada ya Willium kuonekana kuwanyanyasa wanandoa hao.

Hata hivyo, Harry na Willium, wamejitokeza haraka kukana madai hayo na kueleza taarifa hizo zimewaumiza kama ndugu.

Hata hivyo kwa mujibu wa chomho kimoja cha habari, unadaiwa mwanamfalme huyo alikuwa amekasirishwa na nduguye kuhusu mahojiano aliofanya na wanahabari.


Chaazo kingine kutika nyumba ya kifalme, kilisema kuliwapo na sababu tofauti ndani ya jengo la kifalme.

• **KWA MSAADA WA MTANDAO**

UCHAMBUZI

# BURIANI QABOOS AL SAID

- Miaka 29 amng'oa baba, akaa miaka 50
- Sultani, Waziri Mkuu, Nje, Ulinzi, Fedha
- Aliunda Oman mpya barabara kwa elimu
- Hana mtoto, amerithiwa na ndugu yake
- Ndugu damu wa Seyyid Said wa Unguja


Sultani Qaboos Bin Said Al Said, katika kiti. Picha nyingine ni mazishi yake. Aliyezungushiwa pichani ndiye mrithi wake. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi wetu**

SULTANI Qaboos bin Said Al Said wa Oman, mtawala wa muda mrefu katika nchi za Kiarabu ameaga dunia wiki iliyopita, akiwa na umri miaka 79.

Huyo alimng'oa madarakani baba yake katika mapinduzi ya amani, kwa ushrikiano na Uingereza mwaka 1970, hatua iliyoiweka Oman pahala pazuri.

Wakati wa utawala wake, anasifika kuifanya nchi hiyo kuwa juu, katika kufurahia uchumi wa matunda ya utajiri wa mafuta yake.

Ndugu yake Haitham bin Tariq Al Said, sasa ameapishwa kurithi kiti chake, ambaye alikuwa Waziri wa Utamaduni ameapishwa Jumamosi iliyopita, baada ya mkutano wa Baraza la Familia ya Kifalme.

Kwa mujibu wa mfumo wa utawala na sheria za Oman, Sultani ndiye mwenye uamuzi mkuu na anashika wadhifa wa Waziri Mkuu, Amiri Jeshi Mkuu, Waziri wa Ulinzi, Fedha na Mambo ya Nje.

Kabla ya kifo chake, Sultan Qaboos, aliyekuwa nchini Ubelgiji wiki nzima akipata matibabu ya saratani, hakuwa na mrithi kwa sababu ya kukosa mtoto.

Kwa kipindi cha miaka 50 ya utawala wake, anaelezwa staili yake ya utawala ni ya 'kuuma na kupuliza' katika dola hiyo yenye wakazi wastani wa milioni 4.6 na inakaribia nusu yao (asilimia 43) ni wageni.

**ALIMPINDUA BABA**

Akiwa na umri wa miaka 29 tu, Sultani Qaboos alimpindua baba'ke, Said bin Taimur, mfalme anayekumbukwa kwa msimamo mkali, ikiwamo kupiga marufuku mambo kadhaa, ikiwamo kusikiliza radio, kuvaa miwani ya jua na kuamua muoaji, kupata elimu na alifukuza sana watu nchini humo.

Baada ya mapinduzi, Qaboos alitangaza kuunda serikali ya kisasa na kutumia pesa alizopata kutokana na utajiri wa mafuta kuendeleza nchi yake.

Wakati anachukua madaraka, nchi ilikuwa na barabara nzuri umbali wa kilomita 10 tu na shule tatu pekee, hivyo katika miaka ya kwanza ya mapinduzi yaliyosaidiwa na vikosi maalum vya Uingereza, alifanikiwa kukandamiza wanamgambo waliokuwapo Kusini mwa mji wa Dhofar na makabila yaliyoungwa mkono na Jamhuri ya Yemen.

Anatajwa alikuwa na maono kitaifa na aliamua kuchukua siasa za kutounga mkono upande wowote, katika zama hizo kambi mbili za dunia zilichachamaa.

Inaelezwa, mwaka 2013, alifanya mazungumzo ya siri na Marekani na Iran hata kufikiwa kwa makubaliano ya kihistoria yanayohusu nyuklia miaka miwili baadaye.

**ALIVYOTAWALA**

Naye alianza kuonja makali ya msukosuko wa kisiasa katika utawala mwaka 2011, wakati wa vuguvugu la Mapinduzi ya Uarabuni, maelfu ya watu walikusanyika barabarani kudai mishahara juu, nafasi zaidi za ajira na kumalizwa ufisadi.

Baada ya muda, vikosi vya usalama vilivamia waandamanaji kumaliza maandamano hayo, lakini baadaye vilianza kutumia gesi ya kutoa machozi, risasi za mpira na kufyatua risasi hewani kutawanya waandamanaji.

Hata hivyo, maandamano hayo hayakufanikiwa kuleta mabadiliko makubwa, japo Sultani Qaboos, alichukua hatua ya kuwaondoa madarakani mawaziri kadhaa waliokuwa wamedumu kwa muda mrefu, kwa madai ya ufisadi.

Shirika la Haki za Binadamu la Human Rights Watch, linadai tangu wakati huo, mamlaka za kiserikali zimekuwa zikizuia magazeti na majarida huru yanayokosoa serikali na vitabu pinzani.

> Kwa kipindi cha miaka 50 ya utawala wake, anaelezwa staili yake ya utawala ni ya 'kuuma na kupuliza' katika dola hiyo yenye wakazi wastani wa milioni 4.6 na inakaribia nusu yao (asilimia 43) ni wageni.

**ANAIJUAJE UNGUJA?**

Kuna historia inayojenga undugu, kati ya pande hizo mbili, Oman na Zanzibar, kwani mwaka 1832, Sultani wa Oman, Said al-Said, alihamisha makao makuu yake kutoka Muscat, Oman mpaka Zanzibar.

Huo ukawa mwendelezo wa mwingiliano baina ya Oman na Afrika Mashariki, uliokwishaanza.

Qaboos ni kizazi cha sita kutoka kwa Seyyid Said, aliyepafanya Zanzibar kuwa kitovu cha dola ya Oman, katika zama hizo, huku mrithi mpya, Sultan Harith al-Said, naye anaangukia kizazi cha sita kutoka kwa Seyyid Said.

Anatajwa aliingia madarakani Oman mwaka 1806 na mwaka 1832, anatajwa kuhamia Zanzibar, ambako alihamasisha kilimo cha karafuu, zao kuu la biashara Zanzibar mpaka leo.

Sultani Seyyid Said alifariki mwaka 1856, kisiwani Shelisheli akiwa katika safari zake kati ya Zanzibar na Oman.

Ni moja ya historia yenye mnyororo wa uhusiano, hata kufanya Kiswahili kusikika katika mitaa ya jijini Muscat.

> Shirika la Haki za Binadamu la Human Rights Watch, linadai tangu wakati huo, mamlaka za kiserikali zimekuwa zikizuia magazeti na majarida huru yanayokosoa serikali na vitabu pinzani.

JENERALI SIAD BARRE

# Tangu ang'olewe Somalia, mzimu amani haujawahi kudumu kamwe

• Swahiba wa Warusi, mjamaa kindakindaki

**Na Mwandishi Wetu**

IMEFIKIA miaka 29 tangu utawala wa Jenerali Mohamed Siad Barre, kuanguka lakini nchi ya Somalia hajapata amani ya kudumu.

Kiongozi huyo ambaye alikuwa na mrengo wa kijamaa aliiongoza Somalia kuanzia mwaka 1969 mpaka 1991 alipong'olewa kwa nguvu na makundi ya wapiganaji.

Tangu utawala wake ufurushwe madarakani nchi ya Somalia imekuwa eneo tata lililotawaliwa na vita kila mahali, huku kikundi cha kigaidi cha Al Shabab kikiihangaisha serikali ya nchi hiyo ambayo si imara kijeshi.

Wapo wanaosema, mzimu wa jenerali hiyo unaiandama, licha ya vikosi vya Umoja wa Mataifa kuingilia kati kwa kulinda usalama, lakini bado kila kukicha umwagaji wa damu unaendelea.

BARRE NI NANI?

Jenerali Mohamed Siad Barre, alizaliwa Oktoba 6 mwaka 1919 katika kijiji cha Shilavo, Jimbo la Ogaden, Magharibi mwa Somalia, aliyepoteza wazazi alipokuwa na umri wa miaka 10, hivyo alianza kuishi maisha ya yatima.

Jenerali Barre alianza elimu yake ya sekondari katika mji wa Liquu Kusini mwa Somalia na baadaye mwaka 1940 aliendа mjini Mogadishu kujiunga na sekondari.

Akiwa huko utaratibu ulimtaka kupitia kwanza jeshini ma akahamasika kujiunga nalo, chini ya ukoloni wa Italia. Mwaka 1939, Barre alipelekwa kushiriki Vita ya Pili ya Dunia, akiwa kwenye jeshi la Italia na Ujerumani dhidi ya Uingereza na Ufaransa.

Mwaka 1952 alipata nafasi ya kuhudhuria mafunzo katika Chuo cha Kijeshi cha Carabinieri nchini Italia kwa miaka miwili na aliporudi Somalia, ilikuwa neema kwake kijeshi kupanda vyeo hadi kufikia mwaka 1960 Somalia ilipopata uhuru, Barre aliteuliwa kuwa Mkuu wa Kikosi cha Anga, pia Mkuu wa Majeshi Msaidizi.

Muda wote alipokuwa jeshini, Jenerali Barre hakuacha kuonyesha mapenzi yake makubwa kwa mfumo wa kisoshalisti wa Urusi (USSR), hali iliyochochea ukaribu wake na maofisa mbalimbali wa jeshi wa taifa.

Mwaka 1969 mwanajeshi wa cheo cha chini alimpiga risasi Rais wa pili wa Somalia, Abdirashid Ali Shermarke, ni tukio lililomfanya Jenerali Barre, kutokana na tabia tena kuongea bila woga mbele ya wenzake. Alipewa nafasi hiyo.

Oktoba 21 mwaka 1969 jeshi lilitwaa nchi katika mapinduzi yasiyomwaga damu na Jenerali Mohamed Siad Barre, akawa rasmi Rais wa Tatu wa Jamhuri ya Somalia na Kiongozi wa Baraza la Mapinduzi.



Marehemu Jenerali Siad Barre. **PICHA: MTANDAO.**

Kuingia kwake katika kuongoza taifa hilo, kulibadili historia ya Somalia, kwani kutokana na tabia yake ya kujiamini kupindukia, alitangaza rasmi mkakati wake wa kuijenga upya Somalia huku akidai nataka iwe taifa kubwa liogopwe ndani na nje ya Afrika.

Mwaka 1970 Barre aliitangaza Somalia kuwa Taifa la Kijamaa, huku mwenyewe akiipachika jina 'The Great Socialist Somali' na akajiegemeza kwa Urusi.

Alianzisha matumizi ya lugha ya Kisomali shuleni na vyuoni huku akipinga lugha za kigeni, hususani Kiingereza na Kiitaliano.

Mwaka 1973, Barre alikwea kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) na anaelezwa kutumia vizuri kuimarisha jeshi lake kwa kujipatia silaha za kisasa kutoka Urusi.

Alianzisha vijiji vya ujamaa, akajenga barabara na kupiga marufuku ukabila nchini humo kwa kile alichodai Wasomalia ni wamoja.

Mwaka 1976 aliingia kwenye mgogoro na marafiki zake Warusi, ili kuwaonyesha yeye si mtu wa kutishwa aliwatimua wataalamu wote wa Kirusi waliokuwa nchini Somalia huku akisisitiza kuwa hawezi kutishwa wala kumwogopa mtu.

Mwaka 1977 Barre alianza vituko vyake pale alipotaka kuongeza eneo la Jimbo la Ogaden hali iliyomfanya kuvamia eneo la Ethiopia, hii ilichochea kile kilichoitwa vita ya Ogaden ambapo Urusi waliamua kuisaidia Ethiopia ili kumkomoa Barre, mwanzoni vikosi vyake vilipata ushindi hata hivyo mwaka 1978 alizidiwa na kuamua kuliachia eneo hilo.

Mikosi katika maisha yake ilianza mwaka 1986, pale Barre alipopata ajali ya gari mjini Mogadishu na kukimbizwa nchini Saudi Arabia, ambako alilazwa kwa miezi miwili akipatiwa matibabu.

Baada ya kurejea nchini Somalia, Barre alijitahidi kuonyesha bado anaweza kuendelea kuwatumikia Wasomalia, hata hivyo tayari vuguvugu la nani atamrithi lilipamba moto nchini humo huku wengi wakiamini hana uwezo tena wa kuendelea kuongoza taifa hilo.

Mwaka 1988 uasi uliongezeka nchini Somalia, hali iliyofanya maisha kuwa magumu, mwishowe kiongozi huyo alianza kuua watu ovyo na kuongeza chuki dhidi yake.

Januari 26 mwaka 1991 vikosi vya 'Bwana wa Vita' aliyefahamika Mohamed Farrah Aidid, vilifanikiwa kumpindua Barre.

Mohamed Farrah Aidid hakufanikiwa kutwaa madaraka, badala yake ukazuka mzozo kati yake na Ali Mahdi Muhammad.

Baada ya kupinduliwa Barre, alikimbilia kwenye Jimbo la Ogaden, kisha alienda nchini Kenya, baadaye akaelekea Nigeria.

Alifariki Januari 2 mwaka 1995 na kuzikwa kwenye Mji wa Gezo Magharibi mwa Somalia.

***KWA MUJIBU WA TAARIFA ZA KIMATAIFA**



# 'Janja' ya viongozi wa bodi ushirika yaanikwa

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

SHIRIKA la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (Coasco) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, limebainisha kuwa baadhi ya viongozi wa bodi za ushirika wanakwepa kuwasilisha taarifa za ukaguzi na kulipa ada za vyama vyao vya ushirika kwa makusudi.

Kutokana na kitendo hicho Coasco imelazimika kuvikagua jumla ya vyama vya ushirika 356 kwa mwaka 2018/2019 kwa kutimia gharama za ofisi ili kuvibaini vyama vinavyokwema kulipa ada na kutokaguliwa na kisha kuvichukulia hatua kali.

Hayo yalibainishwa jana na Mkaguzi wa Ushirika wa Coasco Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Peter Lema, wakati akizungumza na gazeti hili jijini Mbeya.

Alisema kulingana na sheria ya ushirika ni kuwa Bodi za Vyama vya Ushirika zina wajibu wa kutunza kumbukumbu na kuhakikisha kumbukumbu hizo zinawasilishwa kwa mkaguzi baada ya kufanya mahesabu ya chama husika cha ushirika.

Alibainisha kuwa endapo hesabu za chama hazitakuwa zimewasilishwa kwa wakati ndani ya miezi mitatu baada ya kufanya mahesabu kwa mwaka ni wazi kuwa wajumbe wa bodi za ushirika hizo watakuwa na wajibu wa kupoteza nafasi zao.

"Unajua wajumbe wa bodi za ushirika watapoteza nafasi zao za ujumbe iwapo watashindwa kuwasilisha hesabu zao za mwaka baada ya miezi mitatu kuisha," alisema. Alisema licha ya sheria kuelekeza, lakini baadhi ya wajumbe wa bodi za vyama vya ushirika wamekuwa wakichelewesha kuwasilisha taarifa za vyama vya vyao vya ushirika kwa makusudi, pamoja na kushindwa kulipa ada za vyama vyao vya ushirika kwa wakati. "Coasco kanda imekuwa ikifanya ukaguzi ndani ya vyama hivyo vya ushirika bila ya kujali iwapo chama cha ushirika kimelipa ada au hakijalipa," alisema Mkaguzi wa Ushirika wa Coasco Kanda.

Alisema bodi za ushirika zinatakiwa kuwasilisha taarifa za ushirika kila baada ya mwaka kuisha kwa lengo la kuweza kufanyiwa ukaguzi na kuwa kila bodi ya ushirika itakayoshindwa kuwasilisha wajumebe wa bodi hiyo wanakosa sifa kuendelea.



Meya wa Jiji la Mbeya, Mchungaji David Mwashilindi (kulia), akisalimiana na mmoja wa wanafunzi wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Mwansekwa, wakati wakuu wa shule na waratibu elimu wa kata zote za jiji hilo, walipoenda kukabidhi vifaa walivyochanga kwa ajili ya kuisaidia shule hiyo, jijini juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Watumishi Mbeya-WSSA wapanda miti 200

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

WATUMISHI wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), wamepanda miti 200 katika chanzo kipya cha maji cha Mwansekwa ambacho kimeharibiwa kutokana na shughuli za kilimo.

Akizungumzia mkakati huo jana, Mkurugenzi wa Mbeya-WSSA, Mhandisi Ndele Mengo, alisema kuwa hatua ya mamlaka hiyo kupanda miti katika chanzo cha Mwansekwa ni kuhakikisha vyanzo vyote vinahifadhiwa kikamilifu.

Alisema jitihada zilizofanywa na watumishi za kupanda miche katika chanzo kipya cha Mwansekwa kilichopo jijini Mbeya, ni mwanzo tu na kuwa kuna mkakati wa kupanda miche ya miti katika vyanzo vyote.

"Kinachofanywa na watumishi kupanda miche ya miti katika vyanzo mbalimbali kikiwamo chanzo kipya cha Mwansekwa... kunalenga kukabiliana na vitendo vya uharibifu wa vyanzo hivyo vinavyofanywa na baadhi ya watu wanaojihusisha na shughuli za kilimo," alisema.

Mhandisi Mengo alisema mamlaka hiyo ina jumla ya vyanzo 15 na kuwa chanzo cha Mwansekwa ni chanzo kipya cha maji ambacho kitakuwa ni msaada mkubwa katika kutoa huduma za maji katika Jiji la Mbeya na miji ya jirani.

Alisema kuwa imefika wakati kwa wananchi wakawa mstari wa mbele wa kuhakikisha wanahifadhi mazingira hususani vyanzo vya maji katika maeneo wanayoishi, ili kuchangia kukabiliana na vitendo vya uharibifu wa mazingira unaofanywa na baadhi ya wananchi.

Mandisi Mengo alisema kuwa kuanzia sasa kutakuwa na mkakati wa upandaji wa miti katika vyanzo vyote kwa muda wa mwezi mmoja kuanzia sasa, sambamba na kutoa elimu kwa wananchi wanaoishi karibu na vyanzo hivyo ili waweze kuwa mabalozi wazuri katika kukabiliana na uharibifu wa vyanzo hivyo.

Alisema umefika wakati mamlaka zinazohusika na uhifadhi wa mazingira kuhakikisha zinachukua hatua kali ili kukabiliana na uharibifu wa vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali kutokana na wananchi wengi kuharibu vyanzo hivyo kutokana na shughuli za kilimo na ufugaji. Alisema wananchi waliopo karibu na vyanzo vya maji wanawajibu wa kuhakikisha wanajenga utamaduni wa kuhifadhi vyanzo hivyo kwa ajili ya manufaa ya wananchi wote ambao wataweza kupata huduma nzuri za majisafi.

# EWURA yawapa somo walalamikaji huduma

**Innocent Ng'oko,** MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imewataka wananchi kuacha utamaduni wa kulalamika mitaani kuhusiana na huduma mbovu zinazotolewa na baadhi ya watoa huduma.

Mbali na majukumu mengine EWURA imebainisha kuwa imekuwa ikifanya jitihada za kutatua migogoro kati ya mtumiaji na mtoa huduma ili kuboresha huduma kwa mtumiaji katika sekta za maji na nishati.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Meneja wa EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Karim Ally, na kuwataka wananchi kuacha kulalamika mitaani kuhusiana na huduma mbovu zinazotolewa na baadhi ya watoa huduma waliochini ya mamlaka hiyo na badala yake wafike katika ofisi hizo kwa lengo la kupatiwa ufumbuzi.

Alisema mlaji ana wajibu wa kufuatilia malalamiko yake kwa mtoa huduma na kuwa akishindwa kupata msaada anapaswa kufika katika ofisi za Ewura kwa lengo la kupatiwa huduma za usuluhishi na utatuzi wa migogoro husika.

Maneja huyo alisema kumekuwapo na tabia ya watumiaji wa huduma zinazotolewa na watoa huduma walio chini ya mamlaka hiyo, ambao wamekuwa na utamaduni wa kutoa malalamiko mitaani badala ya kuchukua hatua kwa lengo la kutatua migogoro husika na kuboresha huduma.

Alisema kuwa watumiaji wa huduma ndiyo wenye wajibu wa kupeleka malalamiko yao EWURA kwa lengo la kupatiwa ufumbuzi na kuboresha huduma katia ya mtoa huduma na mtumiaji wa huduma.

"Malalamiko lazima yahusiane na utoaji wa wa huduma au bidhaa zinazodhibitiwa na EWURA, na kuwa malalamiko yanayoshughulikiwa ni yale tu yanayohusiana na utoaji wa huduma," alisema Karim Ally.

Alisema kuwa lengo kuu la utatuzi wa migogoro hiyo unalenga kumlinda mtumiaji wa huduma kwa kuhakikisha anapata huduma bora na nafuu, pamoja na kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi kuliko kesi.



# Uniti 10,000 zahitajika Tanzania ya viwanda

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKURUGENZI wa Shirika la Umeme (Tanesco), Dk. Tito Mwinuka, amesema ili kufikia Tanzania ya viwanda, zinahitajika uniti 10,000 za umeme.

Kutokana na mahitaji hayo, Dk. Mwinuka amesema Tanesco imejipanga kimkakati ili kufanikisha azma hiyo ya serikali.

Aliyasema hayo jana alipofungua mafunzo elekezi kwa baadhi ya wafanyakazi wapya wa shirika hilo, akibainisha kuwa liliajiri watumishi wapya 958 hivi karibuni.

"Tanesco tumejipanga vilivyo kushiriki katika miradi ya serikali ili Tanzania ya viwanda ifikiwe na pia kutoa huduma ya umeme kwa wawekezaji na wananchi kwa ujumla," alitamba na kuongeza:

"Kuelekea Tanzania ya viwanda, tunahitaji kufikia uniti 10,000, hivyo ni vyema mikakati yetu tuiweke sawa ili tufikie malengo tuliojiwekea."

Mkuu wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Dk. Emmanuel Shindika, aliwataka wafanyakazi hao wapya kuhakikisha wanasimamia maadili waliyofundishwa ili kufanya kazi kwa uadilifu.

Alisema hakuna sababu ya kupindisha sheria zilizowekwa kazini, badala yake kuzifuata kama maadili ya utumishi wa umma yanavyoelekeza.

"Nawaomba zingatieni yale mliofundishwa, hakuna sababu ya kufanya kinyume cha maadili elekezi ya kazi," alishauri.

Alisema wamefundishwa kila walichostahili kufanyiwa na mamlaka husika hivyo nao wanapaswa kutendea haki na si kubweteka.

Wafanyakazi wamepewa mafunzo elekezi ya siku sita kabla ya kuanza kazi ili kwenda sambamba na kasi ya shirika hilo katika utendaji wao.



Baadhi ya wakazi wa Jiji la Dodoma wakiwa kwenye foleni kwa ajili ya kupata vitambulisho vya Taifa, katika viwanja vya Nyerere Square, jana, huku zikiwa zimebakia siku tano kufungwa kwa usajili wa laini za simu kwa mfumo wa vidole. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Chuo chaanika mbinu wahitimu wake kujiajiri

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

CHUO cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRDP), kimeweka moduli ya ujasiriamali kwa kila programu ili wanafunzi wanapohitimu masomo yao, wajiajiri wenyewe badala ya kusubiri kuajiriwa na serikali.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Fedha na Utawala, Dk. Vedastus Timothy, aliyasema hayo alipozungumza kwa niaba ya Mkuu wa Chuo na Menejimenti na Wafanyakazi Kampasi Kuu Dodoma na Kampasi ya Kanda ya Ziwa – Mwanza.

Alisema lengo ni kuwafanya wanafunzi kuwa na hamu ya kujiajiri na kuwaajiri vijana wengine.

Kiongozi huyo alisema wanafunzi wengi wa chuo hicho wanapata fursa ya kuajiriwa serikalini, sekta binafsi na wengine wamejiajiri.

"Hata hivyo, sekta binafsi na ajira binafsi sasa zinachukua nafasi kubwa zaidi na zina mchango mkubwa wa kuisaidia serikali kufikia Dira ya Taifa 2025 ya kuipeleka nchi katika uchumi wa kati.

"Kwa kutambua hilo ndiyo maana chuo kimeweka msisitizo wa masuala ya ujasiriamali, kila programu ina moduli ya masuala ya ujasiriamali," alisema.

Aliahidi kuwa chuo kitaendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

"Jukumu lenu wanafunzi ni kusoma kwa bidii ili kufanya vizuri katika masomo yenu, na pia kutokana na kukua kwa sayansi na teknolojia, suala la kusoma vitabu mtandaoni halikwepeki, jengeni utamaduni wa kusoma vitabu katika mifumo yote," alisema.

Aliishukuru serikali ya awamu ya tano kwa kuongeza fedha kwa ajili ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na hivyo kupanua wigo kwa wanafunzi wengi kunufaika na mikopo ya elimu ya juu wakiwamo wa chuo hicho.

Pia, aliwataka wanafunzi kuchukua tahadhari kuhusu maambukizo ya Virusi vya Ukimwi (VVU) ili kulinda nguvu kazi ya taifa.

"Mjiepusheni na tabia mbaya ikiwamo matumizi ya dawa za kulevya, zitasababisha kupata matatizo na hivyo mkashindwa kumaliza masomo yenu," alionya.

# Ujenzi shule ya Sekondari Bunge waiva

**Na Mwandishi wetu,** BAHI

BUNGE linatarajia kujenga Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Bunge katika eneo la Kikombo jijini Dodoma kabla ya kumalizika kwa Bunge la 11.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mratibu wa Kamati ya Ujenzi wa Shule hiyo, Neema Kiula, katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Bahi.B Mratibu huyo alikuwa ameambatana na baadhi ya wajumbe wanne wa kamati hiyo kujifunza jinsi Wilaya ya Bahi ilivyofanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa mfumo wa 'Force Account'. Alisema ujenzi wa shule hiyo utakapokamilika, shule hiyo itakabidhiwa kwa serikali Juni mwaka huu, ikiwa ni siku chache kabla ya kabla ya kumalizika kwa kipindi cha miaka mitano ya Bunge la 11. "Ofisi ya Bunge imetoa Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Bunge ambayo itakabidhiwa serikalini mwezi Juni 2020 kabla ya kumalizika kwa Bunge la 11, hivyo lengo la kuja Bahi ni kupata uzoefu wa kutumia mfumo huo ili tuutumie kukamilisha mradi huu mkubwa," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, aliishukuru kamati hiyo kwa kuichagua wilaya hiyo kujifunza, akieleza kuwa hatua hiyo imeonyesha serikali na Bunge wanatambua kazi nzuri ya usimamizi wa miradi inayofanywa na wataalamu wake.

"Kubwa kuliko yote hapa ni ushirikiano na mshikamano tuliokuwa nao baina yetu, mfano katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Bahi, baada ya kupokea fedha, tuliutambulisha mradi kwa wananchi na waliupokea vizuri sana na wakatoa ushirikiano," alitamba.

Munkunda alisema kuwa jambo lingine lililofanya miradi hiyo itekelezwe vizuri, ni uwazi katika ununuzi wa vifaa, hali iliyojenga morali kwa wataalamu na wananchi kujituma zaidi.

"Pia, pamoja na mwongozo wa usimamizi wa ujenzi uliotolewa, sisi tulijiongeza, tukayagawa majengo yote kwa wakuu wa idara, hivyo kila jengo katika majengo yote saba, lilisimamiwa na wakuu wa idara wawili, kukawa na ushindani wa ndani," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Charles Mduma, aliwaeleza wajumbe wa kamati hiyo kuwa jambo lililopunguza gharama ni kuwatumia mafundi wa kawaida kwa kila hatua ya ujenzi ambao walisimamiwa na mhandisi badala ya kumweka fundi mmoja.

"Mkakati huu ulisaidia kuokoa Sh. milioni 70, yaani angetumika fundi mmoja malipo yaliyokuwa yanahitajika ni Sh. milioni 300, lakini kwa mfumo huo zilitumika Sh. milioni 230," alisema.

Mduma alisema kuwa ununuzi wa vifaa ulifanywa kwa kwenda viwandani moja kwa moja bila kutumia mawakala, hatua iliyopunguza pia gharama za ujenzi.

Alitolea mfano ununuzi wa madirisha ya vioo, bei zilitafutwa na kamati tatu tofauti na kushuka kwa bei kutoka Sh. milioni 60 kwa madirisha 306 hadi Sh. milioni 48 hivyo kuokoa Sh. milioni 12 katika eneo hilo.





# SMZ yaguswa kifo mtawala wa Oman

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, ametia saini kitabu cha maombolezo kufuatia kifo cha aliyekuwa Mtawala wa Oman Qaboos Bin Said Al Said, kilichotokea usiku wa kuamkia Jumamosi iliyopita kwenye Qasri yake ya Beit Al Baraka nchini Oman.

Qaboos Bin Said Al Said aliyefariki akiwa na umri wa miaka 79, aliitawala Oman kwa miaka 50, ambapo utawala wa nchi hiyo binamu yake, Haitham Bin Tariq aliyekuwa Waziri wa Mirathi na Utamaduni wa Oman, ndiye aliyerithi kiti hicho na kutengasiku tatu za maombolezo.

Balozi Seif alitia saini kitabu hicho kwenye ofisi ya ubalozi mdogo wa nchi hiyo uliopo Migombani Mjini Zanzibar.

Akimpa pole Balozi mdogo wa Oman, aliyepo Zanzibar, Dk. Ahmed Al Hafi Hamid. Kufuatia kifo hicho, Balozi Iddi alisema kimewagusa watu wengi wa visiwa vya Zanzibar na Oman kwa ujumla.

Balozi Iddi alisema Oman na Zanzibar zimekuwa na uhusiano wa kihistoria kwa muda mrefu unaotokana na mwingiliano mkubwa wa damu kati ya wananchi wa pande hizo mbili.

Aliwataka wananchi wa Oman kuendelea kuwa na moyo wa subra katika kipindi hichi kigumu cha msiba kwa kuondokewa na kiongozi wao aliyesimamia kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi ndani ya Taifa hilo la Ghuba.

Kwa upande wake Balozi Mdogo wa Oman aliyepo Zanzibar, Dk. Ahmed Al Hafi Hamid, alisema wananchi wa Oman wamezipokea salamu hizo za rambi rambi kutoka kwa ndugu zao wa Zanzibar akiamini kwamba msiba huo kwa njia moja au nyingine pia umewagusa Wazanzibari walio wengi.

Mfalme mpya wa utawala wa Oman Haitham bin Tariq mbali ya kuwa waziri aliyeshughulikia masuala ya mirathi na utamaduni, lakini alikuwa mjumbe wake maalumu wa marehemu Qaboos katika shughuli muhimu na aliwahi kufanya kazi ndani ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Oman.

# Z'bar watakiwa kuchangamkia NHIF

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI wameshauri kujiunga na Mfuko wa Bima za Afya (NHIF), ili kufaidika na huduma za matibabu kwa uhakika pindi watakapokuwa wagonjwa.

Akizungumza jana na waandishi wa habari katika maonesho ya biashara Maisara Mjini Zanzibar, Meneja wa NHIF ofisi ya Zanzibar, Ismail Nuhu Kangeta, alisema wameanza kuimarisha huduma zake na kutoa huduma mbalimbali za afya ili kuwasaidia wananchi kupata matibabu bora yenye unafuu. Kuhusu vifurushi vipya vya Najali Afya, Wekeza Afya na Timiza Afya, alisema huduma hizo zimetoa nafuu kwa wananchi kulingana na umri wake na idadi ya familia.

Meneja huyo aliwataka waajiri wa taasisi binafsi kuona umuhimu wa kuwaunga wafanyakazi wao kwenye huduma za bima ili kuwapunguzia gharama wakati wa kutaka huduma za afya.

Aidha, alibainisha wanakabiliwa na matatizo ya baadhi ya wateja kukosa uaminifu na kwenda kinyume na sheria za mfuko huo.

Alizitaji kuwa ni wateja hao hutumia kadi ya bima hiyo kwa kuwapatia watu wengine ambao siyo wanufaika ambao huzitumia kwenda hospitali ili kupata matibabu. Kwa upande wake mwanachama wa NHIF, Ali Mwajiri, alisema bila kadi ya afya huduma za matibabu zingemshinda na kwamba bima hiyo imekuwa nafuu kwa wanachama kwa kuwa wanapata huduma bora.

"Kwa kweli bima ya afya ni mkombozi kwangu maana hapa sasa nimeshakuwa mtu mzima na nasumbuliwa na maradhi mengi kila mwezi naenda Hospitali ya Oceon Road Dar es Salaam na kwamba gharama ninazotumia ni zaidi ya Sh. 500,000 kama nisingekuwa na bima fedha hizo zingezitoa wapi," alifafanua.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (kulia), akizungumza na msanii maarufu wa kizazi kipya Tanzania, Ali Kiba (kushoto), mjini Zanzibar juzi. Kiba yupo kisiwani humo kwa ajili ya kampeni yake ya 'Un Forgettable.' **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Teknolojia, mitandao lawamani kuharibu vijana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMISHNA wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Mohamed Haji Hassan, amesema kuwa ukuaji wa teknolojia na matumizi ya mitandao ni sababu mojawapo ya kuongezeka kwa makosa ya udhalilishaji Zanzibar.

Aidha, jumla ya makosa 826 ya udhalilishaji yaliripotiwa kwa mwaka 2019 ikilinganisha na makosa 786 yaliopotiwa mwaka 2018. Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, alisema kwa kipindi cha mwaka 2019 matukio ya uzalilishaji hayo yameongezeka lakini hali hiyo inatokana na wananchi kufahamu madhara ya matokeo hayo.

Alisema wananchi baada ya kupata elimu ya vitendo vya ukabaji, ulawiti na unajisi wamekuwa wakiripoti tofauti na siku za nyuma waliyanyamazia na kuyamaliza kifamilia. Kwa mujibu wa Kamishna huyo, watuhumiwa 787 wa makosa hayo kwa mwaka 2019 walikamatwa na mjalada ya kesi hizo baadhi yake yapo mahakamani.

Alibainisha kuwa miongoni mwao wapo waliokutwa na hatia, zilizofutwa na kuondolewa mahakamani, kwa Mkurugenzi wa Mashtaka na mengine yapo katika hatua mbalimbali za upelelezi.

Aidha, alieleza sababu zinazochangia kuongezeka kwa matukio hayo kutotolewa kwa adhabu stahiki na kwa muda mwafaka kwa wakosaji wa makosa hayo na kuwamo kwa mmomonyoko wa madili katika jamii.

Alitaja sababu nyingine ni baadhi ya watu kushindwa kuzuwia matamanio yao na jamii kukosa elimu ya kutosha kuhusu madhara ya makosa hayo pamoja na imani za kishirikina.

Kwa mujibu wa kamishna huyo, Jeshi la Polisi litaendelea kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na kuona vinakomeshwa kwa watuhumiwa kufikishwa mbele ya vyombo vya dola.

Alisema moja ya kazi kubwa itakayofanywa na Jeshi la Polisi ni kukamilisha kwa uchunguzi wa matukio hayo haraka na kufikishwa mahakamani.

# Watendaji wawili kijijini waibua mkanganyiko

**Na Futuna Seleman,** MKURANGA

WAKAZI wa Kijiji cha Picha ya Ndege wilayani Mkuranga mkoani Pwani, wameiomba serikali kumhamisha mtendaji mmoja wa kijiji hicho kutokana na uwapo wa watendaji wawili, hivyo kuwachanganya katika kupata huduma stahili.

Mmoja wa wakazi hao, Bakari Chilumba, alisema watendaji hao wamekuwa ni kero kutokana na kila mmoja kudai ndiye mtendaji halali wa kijiji.

Alisema wamekuwa wakipokea maagizo tofauti kutoka kwa watendaji hao kila wanapokwenda kufuata huduma. "Kawaida ya kijiji mtendaji ni mmoja, kwanini asitolewe mmoja akaenda kwingine?" Alihoji.

Mtendaji wa Kata ya Vikindu, Shaaban Mponda, alikiri kuwapo kwa changamoto hiyo na kuwataja watendaji waliopo ni Hadija Mosha na Rhoda Charge na kuwa wapo katika ofisi moja, na kwamba suala hilo limeshafikishwa katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo.

Jitihada za kumtafuta Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Mhandisi Mshamu Munde, zinaendelea kwa vile simu yake ya mkononi ilikuwa ikiita kila mara bila kupokelewa.

Hata hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Fillberto Sanga, alisema suala hilo amelichukua na litafanyiwa kazi muda si mrefu kwa kuwa si busara watumishi wawili kuwa katika ofisi moja wakati maeneo mengine yana uhitaji wa watumishi kama hao.

Wakati huohuo, akizungunza katika mkutano wa wananchi juu ya mradi wa mpango wa urasimishaji wa makazi ya wananchi katika kijiji cha Kisemvule na Picha ya Ndege Kata ya Vikindu, Sanga aliwataka watendaji na kamati zilizoteuliwa kusimamia zoezi la urasimishaji ardhi na kufanya kazi kwa weledi ili kupunguza migogoro ya ardhi.



Baadhi ya wananchi wakisaidia kushusha magodoro ya msaada yaliyotolewa na Kampuni ya Coca Cola, kwa watu walioathiriwa na mafuriko Wilaya ya Mvomero, mkoani Morogoro, mwishoni mwa wiki. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Takukuru yarejesha mil. 217/- za malipo yenye utata mazao

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Pwani, imefanikiwa kuokoa na kurejesha kiasi cha Sh. 217,481,498, ambazo zililipwa kwa makosa na baadhi ya viongozi wa Bodi ya Vyama vya Ushirika (AMCOS) Mkoa wa Pwani na Bodi ya Mazao Mchanganyiko.

Akitoa taarifa ya miezi mitatu ya Taasisi hiyo kwa waandishi wa habari, Kaimu Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Pwani, Sadiki Nombo, alisema, fedha hizo zimerejeshwa katika Wilaya za Mkuranga, Kibiti, Rufiji na Kisarawe.

Nombo alisema kati ya fedha hizo zilizookolewa, kiasi cha Sh. 67,908,958, kimelipwa kwa wakulima waliostahili wa Wilaya ya Kibiti.

Alisema, kiasi cha Sh. 16,275,000 zililipwa kwa wakulima wa Wilaya ya Rufiji, hivyo kufanya jumla ya Sh. 84,183,958 ambazo zimerejeshwa kwa wakulima, huku uhakiki ukiendelea kwa wakulima walioonewa waweze kulipwa stahili zao kwa wilaya zote.

Nombo alisema mbinu zilizotumika kufanya ubadhirifu wa fedha hizo ni pamoja na kuwalipa baadhi ya wakulima malipo mara mbili kwa mzio mmoja wa korosho.

"Lakini kuna baadhi ya wakulima waliopeleka mazao yao kwenye vyama vya msingi na hawakulipwa fedha zao kwa kutoonekana kwa nyaraka za mapokeo ya mazao yao katika ofisi za vyama vya msingi," alisema. Aidha, alisema, katika kipindi cha miezi mitatu miradi 13 ya maendeleo yenye thamani ya Sh. 2,537,912,252.30 ilikaguliwa ambapo miradi mitatu ilibainika kuwa na mapungufu na hivyo kuanza kuchunguzwa.

"Katika ufuatiliaji wa miradi hii ya maendeleo, baadhi ilibainika kuwa na upungufu kama, kutokamilika kwa sababu mbalimbali ikiwamo ya kuhamishwa fedha na kupelekwa kwenye miradi mingine kinyume cha taratibu, na mingine kuwa na gharama kubwa za utekelezaji ukilinganisha na uhalisia wa kazi.

Katika Wilaya ya Mafia kuna choo cha nje kimejengwa katika jengo la Ikulu ndogo ya wilaya kwa Sh. milioni 32, lakini ukiangalia thamani ya fedha iliyotumika na kazi iliyofanyika si sawa kutokana na upungufu kama huo miradi mitatu uchunguzi wake umeshaanzishwa," alisema.

Alisema miradi iliyobaki wamefanya vikao na wadau kwa lengo la kuweka mikakati ya kurekebisha kasoro zilizobainika.

# Matatani tuhuma kutafuna fedha malipo pamba

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Shinyanga imeokoa kiasi cha Sh. 30,503,650 kati ya Sh. 109,497,130 za wakulima wa pamba, ambazo zimedaiwa kutafunwa na viongozi wa vyama vya msingi vya ushirika (Amcos) wilaya za Kishapu na Shinyanga.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Shinyanga, Hussen Mussa, wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa taasisi hiyo kwa kipindi cha kuanzia Oktoba - Desemba 2019, na kuwa wamefuatilia fedha za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, zikiwamo za wakulima wa pamba.

Alisema wameokoa kiasi cha fedha Sh. 30,503,650 kati ya Sh. 109,487,130 fedha za wakulima wa pamba, ambazo zimetafunwa na viongozi wa Amcos, walizopewa na kampuni kwa ajili ya kwenda kuwalipa wakulima.

"Tunawashikilia baadhi ya viongozi wa Amcos, ambao wametafuna fedha za wakulima, shilingi 109,497,130 walizopewa na kampuni za kununua pamba kwa ajili ya kuwalipa wakulima, na baada ya kuwakamata ndipo wakalipa shilingi 30,503,650 na kubaki na deni shilingi 78,993,480," alisema Mussa.

"Amcos hizi saba ambazo zimetafuna fedha za wakulima ni Ng'washinong'ela shilingi 16,625,000, Nyenze shilingi 6,323,150, Lagana shilingi 23,794,730, Kalitu shilingi 27,718,800, Muhenze Buluba 3,839,050, Ibadakuli 24,834,000, pamoja na Kweli Balimi shilingi 6,362,400, tunaendelea kufuatilia ili fedha zote walipwe wakulima," aliongeza.

Katika hatua nyingine, alisema katika kipindi hicho wamepokea taarifa za rushwa 69 ambazo baadhi zimekamilika uchunguzi wake na zingine zinaendelea, huku akibainisha idara zilizolalamikiwa kwa rushwa ni Polisi, Elimu, Mahakama, Afya, Ardhi, Tasaf, Kilimo, Michezo,Tarura, Bima, Ushirika, TRA, vyama vya siasa na Serikali za Mitaa.

Aidha, alisema kati ya kesi hizo 69, kesi 20 uchunguzi wake umeshakamilika na zipo mahakamani, ambapo zilizosalia zinaendelea kuchunguzwa na zitakapokamilika wahusika watafikishwa mahakamani.

HABARI KIMATAIFA

# Rais Kenyatta sasa afanya mabadiliko Baraza Mawaziri

**NAIROBI, Kenya**

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta, jana, alifanya mabadiliko katika Baraza la Mawaziri wakati akitoa hotuba yake ya kwanza kwa mwaka 2020.

Kwenye mabadiliko hayo, Rais Kenyatta alimteua Monica Juma kuwa Waziri wa Ulinzi huku Raychelle Omamo akiwa Waziri wa Mambo ya Nje.

Rais Kenyatta pia alimteua Ukur Yatani kuwa Waziri wa Fedha, Mutahi Kagwe kuwa Waziri wa Afya huku Betty Maina akichukua Wizara ya Viwanda na Sicily Kariuki akiwa Waziri wa Maji.

Vilevile, alimteua Esther Koimett kuwa Waziri wa Habari na Mawasiliano, Simon Chelugui kuwa Waziri wa Leba.

Aidha, Rais Kenyatta alimteua Peter Munya kuwa Waziri wa Kilimo huku Mwangi Kiunjuri akiondolewa na wengineo.

Wakati wa hotuba yake Rais alisema kwamba wanaweka mipango ya kukwamua uchumi na kusema kuwa asilimia 70 ya madeni yamelipwa.

Pia Rais Kenyatta alisema serikali yake imeweka kipaumbele katika biashara na kusema kuwa juhudi zinafanywa kusaidia biashara ndogo ndogo.

Rais Kenyatta alisema anaamini hakuna utawala ambao umekabiliana na ufisadi kama alivyofanya kwenye utawala wake.

Alisema kuanzia mawaziri mpaka magavana, maofisa wakuu serikali, maofisa wa ununuzi, amekuwa mstari wa mbele kudhibiti vitendo vya rushwa.

Rais Uhuru alisema kuwa ufisadi umewaogopesha wezi wa mali ya umma na kuacha mfumo wa mahakama akiitaka iwajibike kuhakikisha kuwa nchi inashinda vita dhidi ya ufisadi.

Mambo mengine aliyoyazungumza ni utoaji wa fedha za ujenzi wa viwanda viwili vya maziwa.

***BBC***

## Khaftar akataa makubaliano kusitisha vita

**MOSCOW, Urusi**

WAZIRI wa Mambo ya Nje ya nchi ya Urusi, Sergey Lavrov, amesema kuwa mbabe wa kivita wa Libya, Jenerali Khalifa Haftar ameondoka Urusi bila kutia saini makubaliano ya kusitisha vita.

Hapo awali waziri wa wizara hiyo, Sergey Lavrov alisema kuwa sehemu kubwa ya wahusika katika machafuko ya Libya wametia saini makubaliano ya kusitisha mapigano isipokuwa Jenerali Haftar na rafiki yake Aguila Saleh ambaye ni Spika wa Bunge la Mashariki mwa Libya lililojitenga.

Lavrov alisema Haftar na Aguila walitaka wapewe muda zaidi hadi asubuhi ya Jumanne ndipo waweze kutia saini makubaliano hayo ingawa kwa sasa mbabe huyo anadaiwa ameshaondoka Urusi tayari.

Jenerali Haftar ambaye anaongoza jeshi linalojiita jeshi la kitaifa la Libya ni sehemu muhimu ya machafuko hayo.

Pande hizo zinazozana zinatarajiwa mjini Berlin Ujerumani baadaye mwezi huu ingawa msemaji wa serikali ya Ujerumani, Stffen Seibert alisema tarehe ya mkutano huo haijawekwa.

Vikosi vya Jenerali Haftar vimekuwa vikipigania kudhibiti mji mkuu Tripoli ambao uko chini ya serikali inayoungwa mkono na Umoja wa Mataifa (UN).

**DW**



Jenerali Khalifa Haftar kiongozi wa Jeshi la Taifa la Libya (LNA) ambaye amekataa kusitisha vita nchini humo. **Picha AFP**

## Marekani kupunguza askari Afrika, Mashariki ya Kati

**WASHINGTON, Marekani**

MAREKANI iko katika mkakati wa kupunguza idadi ya wanajeshi wake barani Afrika.

Ofisa wa juu wa nchi hiyo, Jenerali Mark Milley, alisema suala hilo linaweza kutokea au wanajeshi hao kuhamishwa katika maeneo mengine.

Waziri wa Ulinzi, Mark Esper hata hivyo hajafanya uamuzi huo ili kufahamu ni hatua gani zitachukuliwa.

Rais wa Marekani, Donald Trump amekuwa akitaka Jeshi la Muungano wa Nato, kuchukua jukumu la kupambana na ugaidi katika eneo la Mashariki ya Kati.

Wakati huo huo, wakuu wa nchi tano za ukanda wa Sahela waliokuwa wakishiriki mkutano na Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, walibaini kwamba wanathamini msaada muhimu wa Marekani na wana matumaini kwamba msaada huo utaendelea.

Jenerali Mark Milley yuko mjini Brussels tangu juzi na kesho atakuwa kwenye mkutano wa kamati ya jeshi la Nato pamoja na wenzake.

Jenerali Milley amethibitisha kuwa vikosi vya Marekani vitapunguzwa barani Arika na Mashariki ya Kati na kuhamishwa katika Ukanda wa Pacific.

"Vikosi vya Marekani barani Afrika na Mashariki ya Kati vitapunguzwa kisha kuhamishwa au kutumwa katika Ukanda wa Pacific.

Jeshi la Marekani barani Afrika, AFRICOM, lilianzishwa mnamo mwaka 2007. Makao yake makuu yapo Ujerumani, lakini wanajeshi 7,000 wanapiga kambi barani Afrika, nusu yao wakiwa katika mji wa Djibouti.

Askari wengine 2,000 wamepelekwa kwenye ujumbe wa mafunzo kwa maslahi ya majeshi ya kitaifa. ***RFI***

## Mataifa yaliyopoteza raia ajali ya ndege kukutana

**LONDON, Uingereza**

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Ukraine, amesema mataifa matano ambayo raia wake wamefariki katika ajali ya ndege wiki iliyopita yatakutana mjini London kujadili uwezekano wa kuchukua hatua za kisheria.

Wakati huo huo, msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje Ujerumani alisema wananchi wa Iran wanapaswa kuruhusiwa kufanya maandamano ya amani na huru, baada ya maofisa nchini humo kukiri kuiangusha ndege ya abiria ya Ukraine.

Akizungumza nchini Singapore jana, Waziri wa Mambo ya Nje wa Ukraine, Vadym Prystaiko, alisema nchi hizo pia zitajadili kulipwa fidia na uchunguzi kuhusiana na ajali hiyo.

Abiria wote 176 waliokuwamo katika ndege hiyo walifariki katika ajali hiyo iliyotokea wiki iliyopita dakika chache baada ya ndege hiyo kuruka kutoka katika uwanja wa ndege wa Tehran.

Prystaiko alisema maelezo kutoka Iran yanaeleza kuwa ndege hiyo ya shirika la ndege la Ukraine iliangushwa wakati ikiruka na eneo nyeti la kijeshi wakati wa kipindi cha wasiwasi wa hali ya juu hayakuwa na maana.

Alisema Terhan imekubali kukabidhi visanduku vyeusi vya ndege hiyo kwa Ukraine ili kufanya uchunguzi zaidi.

Waziri wa Mambo ya Nje ya Ujerumani, Heiko Maas, akiwa nchini Jordan katika ziara aliitaka Iran kuacha kuingilia kati mizozo katika eneo hilo.

***DW***

# CCM yawatumia salamu wapinzani

**Na Dege Masoli, HANDENI**

CHAMA Cha Mapinduzi CCM kimevitumia salamu vyama vya upinzani kwamba vikae sawa kwa kuwa chama hicho hakikamatiki katika uchaguzi mkuu utakaofanyika baadaye mwaka huu.

Salamu hizo zilitolewa juzi na Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, kwa nyakati tofauti alipokuwa akizungumza na wanachama na wananchi Kata ya Mkata baada ya kupokewa kimkoa kwa ajili ya ziara yake ya siku nne mkoani Tanga.

Dk. Bashiru alirudia hayo hayo kwenye kikao cha ndani na wanachama wa chama hicho kilichofanyika mjini Handeni.

Pamoja na mambo mengine, aliwakumbusha Watanzania asili ya CCM kuwa ni chama cha wakulima na wafanyakazi ambao alisema bado hawajapewa heshima inayowastahili.

Akizungumzia uchaguzi mkuu wa mwaka huu, Bashiru aliwataka wana-CCM kutokuwa na hofu na kudai chama hicho si jino bovu linalotaka kung'olewa kama wanavyodai wapinzani na kwamba wasijidanganye.

Dk. Bashiru alivikumbusha vyama hivyo matokeo ya uchaguzi wa serikali za mitaa na kwamba hiyo ilikuwa mvua za rasharasha na mvua ya masika ni Oktoba, mwaka huu.

Alieleza sababu na misingi ya kujivunia ushindi kwa chama hicho kuwa ni mvuto kilicho nacho kwa Watanzania na kwamba kinakubalika kutokana na utekelezwaji wa mambo mbalimbali ambayo hayajawahi kufanyika kabla ya hapo.

"Wana CCM tembeeni kifua mbele kwani mambo yaliyofanywa na awamu ya tano yamekipa mvuto mkubwa chama chetu na hatuna sababu ya kutiwa hofu," alisisitiza Dk. Bashiru.

Alipuuza kauli ya chama kimoja kinachodai uchaguzi ni namba na kwamba hiyo ni dharau kwa kura ya mwananchi na kuweka bayana kuwa hakuna kura ya namba kwenye uchaguzi ila wapigakura watakichagua chama kutokana na kile kilichowafanyia na ambacho kimekidhi mahitaji yao.

Dk. Bashiru alisema CCM ni cha wakulima na wafanyakazi, hivyo ni jukumu lake la kuhakikisha makundi hayo mawili yanapata yalichokitarajia jambo ambalo alikiri kuwapo kwa upungufu katika utekelezwaji wa mambo hayo kwa baadhi ya maeneo.

Alitaja maeneo mawili ambayo hayakufanywa vizuri kuwa ni kilimo na serikali za mitaa kutokana na kutokuwa na watendaji wazuri wenye mipango na mikakati ya kuwatumikia watu na badala yake hufikiria maslahi binafsi.

"Pamoja na kufanya vizuri katika maeneo mengi, lazima tukiri pale ambapo hatukufanya vizuri na huo ndio uungwana. Wakulima wetu bado hatujawakomboa na iko sababu ya makusudi kutekeleza hayo," alisema.

Katibu Mkuu huyo alitaka wakulima na wafanyakazi nchini wasibugudhiwe na kwamba chama hakitakubaliana na kiongozi yeyote atakayekwenda kinyume cha maelekezo hayo.

Aliwapongeza wananchi kwa ushindi mnono na wa kishindo uliotokana na uchaguzi wa serikali za mitaa na kuwaeleza kuwa wembe ni ule ule katika uchaguzi mkuu ujao.

"Matokeo ya uchaguzi wa serikali za mitaa ndiyo dira ya chama kwenye uchaguzi mkuu, hivyo picha ya ushindi iko wazi," alisema.

Dk. Bashiru yuko mkoani Tanga kwa ziara ya siku nne katika wilaya za Handeni, Kilindi, Korogwe, Lushoto, Muheza, Pangani na Tanga.



Wafanyausafi wakifagia barabara ya Sam Nujoma, eneo la Mwenge, jijini Dar es Salaam jana. Hata hivyo, baadhi yao hukumbana na changamoto nyingi zikiwamo za vitendea kazi duni pamoja na baadhi ya madereva kutowajali na kuwasababishia ajali. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Asaka fedha miradi ya maji

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MBUNGE wa Viti Maalum anayewakilisha vyuo vikuu, Esther Mmasi, ameanza awamu ya pili ya kutafuta fedha za kusukuma miradi ya maji katika vitongoji vitatu vya Kata ya Kibosho Mashariki, Wilaya ya Moshi.

Miradi ya majisafi na salama inayotekelezwa kwa nguvu ya wananchi na wadau mbalimbali inavihusisha vitongoji vya Kichau, Mweka Juu, Mweka Chini na Olele.

Akizungumza jana na wananchi wa vitongoji hivyo, Mmasi alisema dhamira yake ya kuwatumikia Watanzania inalenga kuonyesha kuwa uongozi ni vitendo na siyo uzushi, fitina na uchonganishi.

Jana, Mmasi alifanikiwa kuendelea na awamu ya pili ya miradi ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama bure katika vitongoji vitatu vinavyokabiliwa na tatizo la maji kwa muda mrefu.

Akiwa kwenye ziara yake, Mmasi pia aliambatana na viongozi wa serikali akiwamo Ofisa Maendeleo Patrice Otieno kutoka Bonde la Mto Pangani, Ofisa Mazingira Mkoa wa Kilimanjaro, John Emmanuel, wenyeviti wa vitongoji vitakavyonufaika na mradi huo.

Katika ziara hiyo, wakazi zaidi ya 1,000 walioshiriki walijitokeza kusikiliza njia zitakazotumika kutafuta mwarobaini wa tatizo hilo la muda mrefu.

Ili kuunga mkono jitihada hizo na kuvutia wadau wengine wa maendeleo kujitokeza kuchangia mradi huo, Mmasi alikabidhi jora la mabomba ya nchi 1.5 mawili na jora la mabomba ya nchi moja matatu.

Pia alikabidhi mifuko 70 ya saruji, mifuko 40 ya water proof, mchanga lori mbili, fedha za mafundi wa kujenga matangi ya kuhifadhia maji.

Kwa mujibu wa Mbunge huyo, vifaa hivyo vyote vimegharimu zaidi ya Sh. 3,995,000.

# Magereza yafichua wanafunzi mahabusi walivyofaulu kidato 4

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

JESHI la Magereza katika Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, limesema liliwaandalia mazingira mazuri ya kufanya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne wakiwa gerezani, wanafunzi sita wa Shule ya Sekondari Katoro Islamic Seminary wanaoshtakiwa kwa kumuua mwanafunzi mwenzao.

Jeshi hilo limesema lengo ni kuwawezesha kufaulu vizuri.

Akizungumza na wanahabari kwa niaba ya Mkuu wa Magereza mkoa wa Kagera, Mkaguzi wa Magereza na Mkuu wa Gereza la Bukoba, Jasson Kaizilege, alisema baada ya kupata kibali kutoka Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) cha kuwaruhusu wanafunzi hao kufanya mtihani wakiwa gerezani, mbali na kuandaa mazingira ya kufanyia mtihani, pia waliwaandaa wanafunzi hao kisaikolojia ili kuwaweka tayari kufanya mtihani huo.

Kaizilege alisema walipopata taarifa kutoka kwa ofisa elimu mkoa na mkuu wa mkoa huo, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, ikaonekana kweli kuna hitaji la washtakiwa hao kufanya mtihani huo wakiwa gerezani na kuanza maandalizi.

"Tuliandaa vyumba kwa mfumo wa madarasa, madawati na vitendea kazi vyote vinavyohusiana na mitihani...pia tuliwaandaa wafungwa walioko gerezani ili wawe katika hali ya utulivu, huwezi kuamini siku za mitihani wafungwa wote walitulia," alisema.

Alisema kuwa walizungumza na wanafunzi hao mara kwa mara, na kuwa yeye ilimchukua muda mwingi kama kiongozi, lakini kama mzazi kuzungumza na hao vijana, ili kuwapanga, kuwatunza na kuhakikisha kwa akili zao wametulia na kupenda kufanya mtihani.

Alisema baada ya kukamilisha taratibu zote za mitihani alipewa hadhi ya kuwa mkuu wa shule katika kituo cha mtihani cha Magereza, na kuwa vijana hao waliwatengea muda mzuri, kujiandaa.

Alisema katika gereza hilo kuna wafungwa zaidi ya 800 na kuwa walijitahidi kuweka mazingira ya kubadilisha magereza kuwa chumba cha darasa.

Alisema kituo hicho pia kilipewa wasimamizi kama ilivyokuwa katika vituo vingine, na kueleza alivyopata faraja baada ya matokeo ya mtihani kutoka na vijana hao kufaulu vizuri.

"Mmoja alipata daraja la tatu la pointi 25, mwingine daraja la tatu la pointi 23, wengine watatu wakapata daraja la pili la pointi 21 na mwingine akapata daraja la pili la pointi 19, nimefarijika sana na kuona kumbe haya yanawezekana," alisema.

Alisema wanafunzi hao, matokea hayo wameyapokea kwa furaha kwa sababu mwanzoni kabisa walikuwa wamekata tamaa, walisema wapo gerezani, hivyo hawawezi kufanya mitihani.

Kesi hiyo ya mauaji namba 18/2019 inayosikilizwa na Hakimu Flora Kaijage katika Mahakama ya Wilaya Bukoba mkoani Kagera, inaendelea kutajwa na Wakili wa Serikali, Juma Mahona, alisema upelelezi unaendelea.

Washtakiwa katika kesi hiyo ya mauaji ni wanafunzi Sharifu Amri (19), Fahadi Abdulazizi Kamaga (20), Husama Ramadhan (17), Sharifu Huled (19), Abdalah Juma (19) na Hussein Mussa (20), Majaliwa Abdul (35) mwalimu na Badru Issa Tibagililwa (27) mlinzi wa shule hiyo.

Mauji hayo ya Muddy Muswadick aliyekuwa akisoma kidato cha nne katika shule hiyo yalitokea Aprili 14, mwaka jana katika Shule ya Sekondari ya Katoro Islamic Bukoba Vijijini mkoani Kagera.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA /MASHAMBA

**TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSITUTE:** Inatangaza mhula mpya wa masomo Certificate na Diploma za kilimo na maendeleo ya jamii.maelezo zaidi tembelea tovuti yetu www.tracdi.ac.tz Simu**:0714404491/0746995144**

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi **piga 0758 112 332. Karibu EFL**.

**WAHUDUMU WA HOTELI WANAHITAJIKA** Hoteli ndogo Bagamoyo inatafuta wahudumu, wapishi, usafi, bartender wenye vyeti. Kwa mawasiliano zaidi **Piga 0757 129 546.**


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 12/2020**

**Ombi la JOSEPH PETER MAHANGULA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu PETER HENRISH MAHANGULA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 18/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/01/2020

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115584902

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA
KAGERA LILILOPO BUKOBA
MAOMBI RUFAA NA: 67/2019

LONGINOIYOLORIMO...............MKATA RUFAA
DHIDI YA
1, PRISCA SIMON..................... WAJIBU RUFAA
2, GODIFREY EVARIST BUBERWA
3, GERAZI GERVASE

KWA: GODIFREY EVARIST BUBERWA
(POPOTE PALE MLIPO)

Mnaarifiwa/ unaarifiwa kuwa Rufaa Na: 67/2019 yamepangwa kutajwa tarehe 24.02.2020 mbele ya mwenyekiti wa baraza , R.Mtei saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa baraza hili leo tarehe 16.12.2019

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

215584502

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**Kuitwa Shaurini Mdaiwa**

**Mahakama ya mwanzo..................Chamwino**

**Wilaya ya Dodoma**

**Madai nambari 947/2019**

**Mdai..........................Remima Business Co. LTD**

**Mdaiwa........................................Luis Chikokoto**

**Kwa...........................................Luis Chikokoto**

**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta madai yake kwamba : Madai Tshs. 445,000**

Kwahiyo unahitajika kuhudhuria bianfsi katika Mahakama hii siku ya 17//1/2020 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri Hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohisu shauri Hilo kwa ajili ya kujitetea katika shuri Hilo.

Angalia Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibisha Kama umepokea kuitwa Shaurini hii, utaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii Leo tarehe 13/1/2020.

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo.

115584302

---

**NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION**

**(Rules 13 (Civil Procedure of Summons and pleadings) Rules. 1955 G:No....**

**Cap.2 Supp. 64**

**IN RHE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**MISC CIVIL APPL NO.46 OF 2019**

**HADIJA MAYALA...APPLICANT**

**VERSUS**

**HIBRAHIM MRUSHO NGASA.. RESPONDENT**

**To.. IBRAHIM MRISHO NGASA**
**DODOMA**

Take Notice, the mention of the above case suit has been set down on the 15th Day of 01, 2020.

You must produce on that day all the witness upon whose evidence and all the documents upon you intend to support of your case.

Given under my hand seal of the Curt this 11 day of 12.2019.

RESIDENT MAGISRATE
DODOMA

115584402


Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie
0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MARQUINHOS ASAINI MKATABA MPYA PSG

**PARIS, Ufaransa**

PARIS Saint-Germain imempa mkataba mpya wa miaka minne na nusu mlinzi wake, Marquinhos.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil amesaini mkataba na mabingwa hao wa Ufaransa ambao utamweka klabuni hapo hadi mwaka 2024, akiwa ameongeza miaka miwili kutoka kwenye mkataba wake wa sasa.


Marquinhos ni nahodha msaidizi pamoja na beki mwenzake wa kati Thiago Silva.

Alijiungana na klabu hiyo kutoka Roma Julai mwaka 2013 na ameisaidia PSG kutwaa mataji matano ya Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1.

Klabu imethibitisha Jumatatu, wakimwita yeye "mmoja wa wachezaji wenye mafanikio makubwa kwenye historia ya Paris Saint-Germain".

Marquinhos alisema: "Paris na PSG wamefikia makubaliano na mimi kubakia hapa na nimeongeza mkataba.

"Ni malengo ya klabu kwamba wanataka vitu vikubwa na kwa ajili ya kuweka historia katika klabu hii."



## MULLER ATAKIWA KUFANYA UAMUZI

**MUNICH, Ujerumani**

THOMAS Muller hatafanya maamuzi yoyote kuendelea kukaa kwa muda mrefu na Bayern Munich hadi mwishoni mwa msimu huu.

Mchezaji huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Ujerumani ametumia muda wake wote wa kucheza kwenye klabu hiyo ya Allianz Arena, ambako ameshinda mataji nane ya Bundesliga, matano ya DFB-Pokals na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya.


Hata hivyo, Muller alibainisha Oktoba mwaka jana ataangalia uwezekano wa kuondoka baada ya kutokuwa na nafasi ya kucheza mara kwa mara chini ya kocha Niko Kovac.

Huku sasa timu hiyo ikiwa chini ya kocha, Hansi Flick hadi mwishoni mwa msimu, mambo yamebadilika, ingawa uvumi unasema kwamba, Muller bado atakabiliwa na changamoto mpya.

Akizungumza na Sport1, alisema: "Majaliwa yangu bado hayajaamuliwa na nimekuwa kwenye msimu wenye mafanikio makubwa.

"Nini kitakachotokea kipindi hicho cha majira ya joto hakijajulikana, zitazungumza na klabu kuhusu nini kitakachotokea."





# JUVENTUS
## KUTOFANYA USAJILI JANUARI

**TURIN, Italia**

MKURUGENZI wa Juventus, Fabio Paratici, amesema mabingwa hao wa Ligi Kuu Italia, Serie A, hawapo kwenye nafasi ya kuongeza mchezaji mpya wakati huu wa kipindi cha majira ya baridi, huku akikataa uwezekano wa kuondoka kwa mlinzi Daniele Rugani.

Nyota wa Tottenham, Christian Eriksen amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Juve, ambao tayari wamemsajili kiungo Dejan Kulusevski na kumtoa kwa mkopo kule Parma hadi mwishoni mwa msimu huu.

Kumekuwa na uvumi kwamba Emre Can, Adrien Rabiot na Rugani wanaondoka, huku Paratici akiwa hatarajii kuona usajili mwingine ukifanyika kipindi hiki.

"Mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ni ngumu na kuna timu zinapambana ikiwamo Lazio na Inter. Inter tayari ina wachezaji kama Romelu Lukaku, Alexis Sanchez, Nicolo Barella na Stefano Sensi.

"Kwa sasa inakuwa ngumu kwa upande wetu kuongeza tena wachezaji," alisema Paratici akiiambia Sky Sport Italia.




# DORTMUND HAIJAAMUA MAJALIWA YA GOTZE

**DORTMUND, Ujerumani**

MKURUGENZI wa Michezo wa Borussia Dortmund, Michael Zorc, amesisitiza hakuna uamuzi uliofanyika kuhusu hatima ya Mario Gotze kwa klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Gotze mwenye umri wa miaka 27, mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu na amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka, akiwa ameanza katika mechi tano tu za Bundesliga msimu huu.

Nyota huyo aliyeichezea Ujerumani mechi 63 yupo katika msimu wake wa pili pale Dortmund, lakini Zorc amesema pande zote mbili zitasubiri kufanya maamuzi juu ya majaliwa ya mshambuiaji huyo.

"Hakuna kilichoamuliwa hadi sasa," alisema Ruhr Nachrichten.

"Bila shaka yeye mwenyewe anataka kucheza kwa dakika nyingi zaidi. Tunazungumza na Mario.

"Nilizungumza na baba yake kabla ya Krismasi. Nilizungumza nae pia kule Marbella. Naamini tutakaa tena pamoja na kufanya maamuzi."

Mchezaji mwingine ambaye anahusishwa kuondoka hapo Dortmund ni Achraf Hakimi, ambaye amekuwa na kiwango cha kuvutia anakocheza kwa mkopo kule Real Madrid.

# Mourinho: Sina wivu na City, Liverpool

**LONDON, England**

JOSE Mourinho amesisitiza hana "wivu" na vikosi vya Liverpool na Manchester City, akisema Tottenham ni kazi tofauti.

City imetoka kushinda taji la Ligi Kuu England mara mbili mfululizo, huku Liverpool wanaongoza msimamo kwa tofauti ya pointi 14 kileleni huku wakiwa wamecheza mechi moja pungufu.

Mourinho alichaguliwa kuwa kocha wa Spurs Novemba mwaka jana, na kikosi chake kinapambana kikiwa nafasi ya nane kwenye msimamo.


Lakini kocha huyo raia wa Ureno amesema hawawezi kulinganishwa na City pamoja na Liverpool, ingawa akabainisha hawezi kulaumu hilo.

"Hivyo ndivyo ilivyo. Hatuwezi kuwa na kikosi kama timu nyingine. Sio sisi," alisema Mourinho.

"Nilikuwa nawatazama Manchester City (dhidi ya Aston Villa) na niliangalia benchi kuna – (Raheem) Sterling, Bernardo Silva, (Ilkay) Gundogan, (Nicolas) Otamendi. unajua?

"Liverpool, unawaona kwenye mechi pia wachezaji wakali. Na wana majeruhi (Joel) Matip, (Dejan) Lovren, (Naby) Keita, Fabinho.

"Sina wivu, nina kazi ya kuvutia, lakini ni kazi tofauti. Hivi ni klabu mbili tofauti."



# BARCELONA WAMTEMA RASMI VALVERDE



**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona imethibitisha imeachana na kocha wake, Ernesto Valverde na nafasi yake amepewa, Quique Setien.

Valverde alipigwa picha akiwa mazoezini Jumatatu kabla ya kukutana na bodi ya Barca.


Baada ya kukamilika kwa mazungumzo hayo, Barca ilitangaza kufikia mwisho wa huduma ya Valverde ambaye alisaini mkataba wa miaka miwili na nusu hapo Camp Nou, huku kocha wa zamani wa Real Betis, Setien akichukua nafasi yake na amesaini mkataba utakaomweka hapo hadi Juni 2022.

"FC Barcelona na Ernesto Valverde wamefikia makubaliano ya kukatiza mkataba kwa pande zote mbili," taarifa ya Barcelona ilisema.

"Klabu inapenda kumshukuru Ernesto Valverde kwa kazi yake nzuri na kufanya vizuri majukumu yake. Tunamtakia kila la heri."

Setien amechukua nafasi ya Valverde licha ya Barca kuwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Hispania, La Liga na bado wapo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA AJIPANGA KUMSAJILI STONES

Anatarajia kumtumia wakala wao ili kurahisisha mchakato wa kumnasa beki huyo...

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amekaririwa akisema anajiandaa kufanya mchakato wa kumsajili kwa mkopo beki wa Manchester City, John Stones (25).

Uamuzi wa The Gunners kuhitaji huduma ya beki huyo inatokana na timu hiyo kuhitaji kujiimarisha kwenye safu ya ulinzi baada ya kuruhusu idadi kubwa ya mabao msimu huu.

Arteta anaangalia uwezekano wa kumpata nyota huyo kwa kumtumia wakala wake ambaye amekuwa na mahusiano na Stones, gazeti la The Sun limeandika.

Kocha huyo na Stones wanamtumia wakala mmoja, na anaamini hiyo itasaidia kufanikisha mazungumzo ya uhamisho wa beki huyo.

Watu hao wamekuwa wakifanya kazi kwa karibu kwa misimu kadhaa, tangu Arteta alipokuwa Kocha Msaidizi chini ya Kocha Mkuu, Pep Guardiola.

Stones anahitaji kupata nafasi ya kupandisha kiwango chake kuwa bora kuelekea mashindano ya Kombe la Ulaya kwa ajili ya kuitumikia Timu ya Taifa ya England katika kipindi cha majira ya joto.

Mtu mmoja aliye karibu na mchezaji huyo aliliambia gazeti la The Sun kuwa: "Wiki iliyopita alikuwa London kuonana na wakala wake na anatarajia kurejea tena wiki hii kwa ajili ya kuonana naye kwa mara nyingine.

"Anajua kama anahitaji kuendelea kuitumikia England anapaswa kupata muda zaidi wa kucheza.

"Arteta anahitaji sana mabeki na kwa faida ya pande zote mbili ni muhimu kukamilika kwa mchakato huo."

## KWA UFUPI

**MOURINHO KUSAJILI WATATU**

KOCHA wa Spurs, Jose Mourinho anataka kusajili mastraika wapya wawili ili kuziba pengo la Harry Kane. Straika wa AC Milan na Timu ya Taifa ya Poland, Krzysztof Piatek (24), mshambuliaji wa Hispania na Napoli, Fernando Llorente (34) na mshambuliaji Mbelgiji wa Crystal Palace, Christian Benteke (29), wanatajwa kuanza mawasiliano na Spurs. ***(Independent)***

**MULLER ANUKIA UNITED**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Thomas Muller anatarajia kuondoka Bayern Munich baada ya kukaa klabuni hapo kwa muda wa miaka 20, huku Manchester United ikiwa tayari kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 30 katika majira ya joto. ***(Sport 1, via Sun)***

**ERIKSEN KIMEELEWEKA INTER**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen (27), anakaribia kuondoka Tottenham baada ya kufikia makubaliano ya kutua Inter Milan ambayo itamlipa mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki. (Times, subscription needed)

**LACAZETTE ATAKIWA ATLETICO**

ATLETICO Madrid imesema inataka kumsajili mshambuliaji wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Alexandre Lacazette (28), baada ya kushindwa mchakato wa kumnasa straika wa Paris St-Germain, Edinson Cavani (32). ***(Express)***

**COBBAUT AKARIBIA SHEFFIED**

SHEFFIED United inajipanga kutoa ada ya pauni milioni 10 ili kumsajili beki wa Anderlecht Mbelgiji Elias Cobbaut (22) na beki wa kati wa Ipswich, Luke Woolfenden, ambaye ana umri wa miaka 21. ***(Sun)***

**SHAQIRI MAMBO MAGUMU**

LIVERPOOL imekacha kuendelea na mchakato wa kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa Roma na Timu ya Taifa ya Uswisi, Xherdan Shaqiri (28). ***(Star)***

**ASHLEY, BRUCE KUTETA**

KOCHA Mkuu wa Newcastle, Steve Bruce anatarajia kufanya mazungumzo na mmiliki wa timu hiyo, Mike Ashley ili kujadili mipango iliyobakia kuhusiana na dirisha dogo la usajili la Januari linaloendelea. ***(Guardian)***

**GAYLE AKARIBIA NEWCASTLE**

MABOSI wa Newcastle wamempa ofa ya kumsajili kwa mkopo straika Dwight Gayle, ambaye ana umri wa miaka 29. ***(Telegraph)***

**BENTEKE KURUDI VILLA**

ASTON Villa inajiandaa kumfanya mchakato wa kumsajili kwa mara ya pili straika wa Crystal Palace Mbelgiji Christian Benteke, ambaye ana umri wa miaka 29. ***(Express)***

**LIVERPOOL YAMWANIA CAKIR**

LIVERPOOL imewasilisha ofa ya pauni milioni 12.8 kwa klabu ya Trabzonspor ili kumnasa golikipa wa Uturuki, Ugurcan Cakir (23). ***(Sabah, via Sport Witness)***

**DANGOTE AITAKA ARSENAL**

BILIONEA raia wa Nigeria, Aliko Dangote (62), amesema anaangalia uwezekano wa kuinunua Arsenal ifikapo mwakani. ***(Evening Standard)***

**OLSSON AJIFUA WEST**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Blackburn na Timu ya Taifa ya Sweden, Martin Olsson (31), anajiandaa kwenda kufanya mazoezi na klabu inayoshiriki Ligi ya Championship, West Brom. ***(Lancashire Telegraph)***

HABARI MICHEZO

# KATWILA AFURAHIA REKODI MTIBWA IKITWAA KOMBE

**Na Isaac Kijoti, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, ameeleza kufurahia kuandika rekodi ya kulitwaa Kombe la Mapinduzi akiwa mchezaji na sasa kocha wa timu hiyo.

Mtibwa Sugar juzi usiku ilitwaa ubingwa huo kwa kuifunga Simba bao 1-0 kwenye mechi ya fainali iliyopigwa Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

Bao pekee katika mechi hiyo ambayo Simba ilikuwa ikipewa nafasi kubwa ya kutwaa ubingwa, lilifungwa na Awadh Salum katika dakika ya 38 akipokea pasi kutoka kwa Jaffar Kibaya.

Hiyo ni mara ya pili kwa Mtibwa Sugar kutwaa ubingwa huo baada ya kuutwaa mwaka 2010 kwa kuifunga Ocean View katika mchezo wa fainali wakati huo Katwila akiwa mchezaji wa 'Wanatamtam' hao.

Akizungumza na Nipashe baada ya mechi hiyo, Katwila alisema ni furaha kwake kuweka rekodi hiyo Mtibwa kwa kuifunga timu bora kama Simba.

"Nilitwaa ubingwa huu nikiwa mchezaji na timu hii ya Mtibwa na leo nimelitwaa tena kombe hili nikiwa kocha wa timu hii, najisikia furaha sana kwa rekodi hii," alisema.

Alisema ilikuwa fainali ngumu hasa kwa kuwa alikutana na timu bora ambayo inaundwa na wachezaji wengi wenye uwezo wa juu.

"Simba ni timu bora na ndiyo inayoongoza Ligi Kuu Bara, hivyo kwanza tuliiheshimu kwa hilo, lakini tulipambana na kupata ushindi, nawapongeza sana wachezaji wangu kwa kufuata maelekezo niliyowapa," alisema.

Kwa ubingwa huo Mtibwa imelamba Sh. milioni 15, kombe na medali za dhahabu wakati Simba ikiambulia Sh. milioni 10 na medali za fedha.

# Serikali Zanzibar yampongeza Kiba

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amewataka wasanii kutambua jukumu lao ndani ya jamii la kuelimisha kwa kutumia sanaa ili kusaidia maendeleo na mabadiliko muhimu ya taifa.

Balozi Iddi alisema licha ya sanaa kuchukua nafasi kubwa katika kutoa burudani na ujumbe wake kuifikia jamii kirahisi, lakini bado anaamini haijatumika vema.

Kiongozi huyo alisema hayo jana ofisini kwake Vuga Mjini Zanzibar wakati akizungumza na Msanii maarufu wa Bongo Fleva nchini, Ali Kiba aliyepo visiwani hapa kwa ajili ya kusaidia jamii katika kampeni yake ya Ali Kiba 'Unforgettable'.

"Itapendeza zaidi kama jamii itaendelea kushuhudia sana, inatumiwa vyema katika kuelimisha kwa vile ni moja ya sehemu inayoweza kufundisha kwa urahisi," alisema Balozi Iddi.

Alisema wasanii wengi wa kikazi kipya wanajishughulisha na nyimbo zinazokiuka maadili hasa mavazi jambo ambalo ni hatari kuigwa na watoto ambao ni Taifa la baadaye.

Kiongozi huyo alimpongeza na kumshukuru msanii huyo kwa kampeni yake ya kusaidia jamii kupitia mapato yake na kuwahidi kumpa ushirikiano zaidi katika kazi hiyo anayoifanya.

Kwa upande wake, Kiba alisema aliamua kuunda kampeni hiyo kwa lengo la kuondoa dhana iliyojengeka kwa baadhi ya watu kufikiria kwamba muziki ni sehemu ya uhuni. Kiba alisema muziki hutoa ajira nyingi kwa kundi kubwa la vijana walioamua kuendesha maisha yao kupitia sanaa hiyo na ndani yake kuna ujasiriamali.

Kuhusu kampeni hiyo, alisema inalenga kutoa huduma za afya katika upimaji bure pia huwatembelea wanafunzi wa vyuo vikuu, ili kuwajengea uwezo wa kutumia vyema elimu wanayoipata.



Mchezaji wa tenisi kutoka Kenya, Melissa Mwaka, akipiga mpira kuurudisha kwa mpinzani wake (hayupo pichani), katika mchezo wa fainali wa mashindano ya Afrika uliochezwa katika viwanja vya Gymkhana jijini, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kombe la FA Z'bar lakaribia

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limetangaza mashindano ya Kombe la FA yataanza rasmi Januari 20, mwaka kwenye Visiwa vya Unguja na Pemba.

Katibu wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Hussein Ahmada, alisema mashindano hayo yataanza kwa kushirikisha timu 32 kutoka Unguja na katika hatua ya awali yatacheza kwa mfumo wa mtoano.

Ahmada alisema timu zitakazoshiriki ni za Ligi Kuu Zanbibar, Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja pamoja na timu za madaraja ya mikoa mitatu ya Unguja.

Aidha, alisema Pemba itatoa idadi ya timu sawa na zile zitakazoshiriki kutoka Unguja na kuelekeza bingwa wa michuano hiyo atapata tiketi ya kuiwakilisha Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Hata hivyo aliziomba timu zinazoshiriki michuano hiyo kuzingatia kanuni za mashindano pamoja na kupeleka timu uwanjani kwa wakati ili kupata bingwa atakayekuwa amepata pointi za uwanjani.

# Klabu zahimizwa kukamilisha usajili

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI dirisha dogo la usajili linatarajiwa kufungwa rasmi leo usiku, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limezitaka klabu zote za Ligi Kuu, Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili na Ligi Kuu ya Wanawake kukamilisha mchakato wa usajili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Cliford Ndimbo (pichani), alisema hakutakuwa na muda wa ziada wa kukamilisha usajili huo na TFF haitakuwa na huruma kwa klabu ambayo haitakamilisha usajili wake.

**"Dirisha la usajili litafungwa kesho (leo) usiku, hakutakuwa na muda wa ziada kwa klabu kufanya usajili, tuna zikumbusha klabu zote kukamilisha usajili kwa wakati, na wale wanaohamisha wachezaji pia wahakikishe wanafuata taratibu," alisema Ndimbo.**

Ndimbo alisema TFF inazitaka klabu kukamilisha taratibu za kusajili wachezaji wanaotoka nje ya nchi kwa kuingia kwenye mtandao ili wapate vibali (ITC).

Tayari timu ambazo zimekamilisha taratibu za wachezaji wapya, zimeanza kuwatumia katika mechi za Ligi Kuu Bara na mashindano ya Kombe la Mapinduzi yaliyomalizika juzi.



Michezo
Jumatano Januari 15, 2020
Nipashe



Arteta ajipanga kumsajili Stones

HABARI UK 30

# Gonjwa linaloitesa Simba ni hili hapa

●●●Kikosi kipana 'shoo gemu' tatizo, Mo Dewji 'achafua' hali ya hewa, abadilisha uamuzi wake...

Na Isaac Kijoti, ZANZIBAR

KWA mara ya pili mfululizo mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara wameukosa ubingwa wa Kombe la Mapinduzi baada ya usiku wa kuamkia jana kukubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Mtibwa Sugar.

Muda mchache baada ya kupoteza mchezo huo, mwekezaji wa klabu hiyo, Mohammed Dewji 'Mo' alitoa tamko la kujiondoa katika nafasi ya Uenyekiti wa Bodi na kubakia mwekezaji, lakini jana asubuhi alibadilisha kauli hiyo na kusema ataendelea na nafasi yake.

"Kilichotokea jana katika akaunti yangu (Twitter), ni bahati mbaya. Tunarejea katika Ligi Kuu tukiwa imara. Tunajipanga kwa ajili ya ligi, nawapongeza Mtibwa kwa kuchukua kombe. Mimi ni Simba damu damu. Nitabaki kuwa Simba," alisema Mo.

Mwaka jana pia, Simba iliukosa ubingwa huo kwenye mechi ya fainali dhidi ya Azam FC baada ya kukubali kipigo cha mabao 2-1.

Katika mchezo huo wa fainali uliopigwa kwenye Uwanja wa Amaan, Mtibwa ilipata ushindi kwa bao la dakika ya 38 kupitia kwa Awadh Salum akipokea pasi mpenyezo kutoka kwa Jaffar Kibaya.

Matokeo hayo yanaifanya Azam kulipa kisasi cha mwaka 2015, ambapo timu hizo zilikutana fainali ya michuano hiyo na Simba kutwaa ubingwa kwa kushinda kwa mikwaju ya penalti 4-3.

Hata hivyo, mechi hiyo ya juzi, Simba iliweza kumiliki mpira kwa asilimia kubwa tatizo lilikuwa kuziona nyavu za Mtibwa ambayo ikipata mpira ilikuwa ikishambulia kwa kasi.

Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck licha baada ya mechi hiyo kugoma kuzungumza lolote, mwenzake wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, alikiri wapinzani wao kuwa bora.

Katwila aliliambia Nipashe kuwa, alifahamu ubora wa kikosi cha Simba na ubora wa mchezaji mmoja mmoja, hivyo kwanza akawaheshimu kama timu kubwa.

"Niliiheshimu Simba kama timu kubwa na bora, nikijua kwamba lazima watamiliki mpira zaidi, na mipango yetu ikafanikiwa, tukapata bao na kuweza kulilinda," alisema Katwila aliyeweka rekodi ya kutwaa ubingwa huo akiwa mchezaji na sasa kocha.

Alisema kutokana na kubaini ubora huo wa Simba, aliwataka wachezaji wanapokuwa na mpira kushambulia kwa kasi na kupanda na kushuka wote jambo ambalo liliwapa matokeo chanya.

Hata hivyo, mchambuzi wa soka, Colman Emily anasema, tatizo kubwa linaloonekana kuitafuna Simba ni wachezaji wake kuamini wanaweza kufunga wakati wowote na hivyo kuzidisha kucheza soka la burudani zaidi badala ya kutafuta mabao.

"Wachezaji wanapenda sana kucheza 'shoo gemu' kwa kufurahisha mashabiki jukwaani na wanaposhtuka wanajikuta muda umeenda na hawawezi kupata tena bao ama kurudisha.

"Kingine makocha wa Simba bado hawajawa na kikosi cha kwanza ama cha ushindi na wamekuwa wakichezesha wachezaji kwa kupokezana kama alivyokuwa akifanya Unai Emery pale Arsenal na ikamgharimu.

"Tazama timu kama Liverpool ama Barcelona, zina vikosi vipana, lakini huwezi kukuta kunafanyika mabadiliko ya wachezaji sita katika kikosi cha kwanza. "Mchezo mkubwa kama huo wa fainali, kwa Simba ambayo imekamilika ilibidi kuchezesha kikosi kamili, lakini kocha anaendekeza suala la kutoa nafasi kwa kila mchezaji," alisema Emily.

Kwa kutwaa ubingwa huo, Mtibwa Sugar ililabidhiwa kombe na medali za dhahabu sambamba na Sh. milioni 15 huku Simba ikiambulia Sh. milioni 10 na medali za fedha.



Kiungo wa Real Madrid, Luka Modric (kushoto), akiwania mpira dhidi ya beki wa Atletico Madrid, Renan Lodi katika mechi ya fainali ya Kombe la Mfalme Hispania iliyochezwa kwenye Uwanja wa King Abdullah jijini Jeddah, Saudi Arabia Jumapili. Madrid ilishinda kwa penalti 4-1. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga, Kagera vitani Ligi Kuu

Na Somoe Ng'itu

TUMEJIPANGA! Hii ni kauli ya Kocha Msaidizi wa Yanga, Boniface Mkwasa, kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Mkwasa aliliambia gazeti hili kuwa wamejiandaa kufanya vizuri katika mechi hiyo na watacheza kwa tahadhari kutokana na kuwaheshimu wapinzani wao.

Kocha huyo alisema Kagera Sugar imekuwa na matokeo mazuri msimu huu na kasi waliyonayo wanatarajia kuiendeleza kwa sababu wanataka kukaa katika nafasi ya juu kwenye msimamo wa ligi.

"Haitakuwa mechi rahisi, tunajuana na tunafahamu ugumu wa Kagera Sugar, haitaki kurudia makosa ya misimu miwili iliyopita, inapambana kusaka ushindi, lakini sisi Yanga pia tumejipanga kuondoka na pointi tatu," alisema Mkwasa.

Naye Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, alisema wamejiandaa kupambana katika mchezo wa leo ili kupata matokeo chanya.

Maxime alisema kuwa kikosi chake kilitua jijini mapema na hana majeruhi, hivyo anaamini mipango yake iko katika nafasi nzuri ya kutekelezeka.

"Tunawaza ushindi, ingawa nakiri tangu nimetua Kagera nimekuwa nikisumbuka sana, wananivuruga, ila kesho (leo), ni wakati wangu wa kuvunja mwisho, sasa hivi upepo utawageuka," Maxime alisema.

Yanga itashuka katika mchezo wa leo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Tanzania Prisons wakati wageni Kagera Sugar wao walikumbana na kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Polisi Tanzania katika mchezo uliochezwa Uwanja wa Ushirika, Moshi.

Yanga iko katika nafasi ya saba ikiwa na pointi 25 na imecheza michezo 12 wakati Kagera Sugar yenye pointi 24 inafuata kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 24 baada ya kushuka dimbani mara 16.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >